UKWELI ULIOPOTEA

الحقيقة الضائعة
رحلتى نحو مذ هب اهل البيت

Msafara Wangu Kuwaelekea Ahlul Bayt

Sehemu ya Kwanza

Je, Ahlul Bayt ni Nani?

Kimeandikwa na Mwandishi wa Kisudani:
Shaikh Mu'tasim Sayyid Ahmad

Kimetarjumiwa na:
Shaikh Harun Pingili

ترجمة

الحقيقة الضائعة

"رحلتي نحو مذهب آل البيت (ع)"

(القسم الأوّل)

تأليف

الكاتب السوداني

الشيخ معتصم سيّدأحمد

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 - 65 -2

Kimeandikwa na Mwandishi wa Kisudani:
Shaikh Mu'tasim Sayyid Ahmad

Kimetarjumiwa na:
Shaikh Harun Pingili

Kimehaririwa na:
Hemedi Lubumba Selemani

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Hajat Pili Rajab

Toleo la kwanza: Juni, 2010
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.alitrah.org

Katika mtandao: www.alitrah.info

Kwa kushirikiana na:
Orison Charitable Trust
P.O.Box - 704
Harrow HAZ 7BB
UK

Yaliyomo

Mlango wa kwanza

Dondoo kutoka katika maisha yangu.....2
Siku za Utoto.....2
Mwanzo ulikuwaje.....5
Chuoni.....12

Mlango wa Pili

Upotovu umefichuka..... 25
Vyanzo vya Hadithi..... 29
Ukweli wa kihistoria na hadithi (na sunna yangu)..... 32
Maongezi na mwana hadithi wa Damascus, Abdul-Qadir Al-Arnutiy.....42
Tatizo la masunni halitanzuki kwa hadithi mbili.....50

Mlango wa Tatu

Hadith: “kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu katika rejea za Kisunni.....57
Hoja dhidi ya hadithi ya “Vizito Viwili”.....69
Hadithi hii ni dalili ya Uimamu wa Ahlul Bayt.....79
Je, Ahlul-Bayt ni Nani?.....83
Ahlul-Bayt katika Aya ya Tohara.....84
Ahlul-Bayt katika Aya ya Mubaha.....92

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho *al-Haqiqatu ‘dh-Dha’i’ah* kilichoandikwa na Sheikh Mu’tasim Sayyid Ahmad. Sisi tumekiita, *Ukweli Uliopotea*. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, sisi tumekigawa katika juzuu tano ili kiwe chepesi kusomwa na wasomaji wetu wa Kiswahili. Hiki ulichonacho mkononi mwako ni juzuu ya kwanza.

Kitabu hiki ni utafiti uliofanywa na mwanachuoni huyo wa Kiislamu kuhusu madhehebu za Kiislamu. Utafiti wake huu ulihusisha pia mahojiano na mijadala baina yake na na masheikh wa Kiwahabi na maustadh wake katika chuo alikosoma.

Kama kawaida katika utafiti wake, ametumia sana vitabu vya historia ya Kiislamu na vya hadithi vilivyoondikwa na wanavyuoni wa Sunni na Shia, kisha akahitimisha kwa Qur’ani Tukufu na Sunna. Baadhi ya vitabu hivyo ameviorodhesha ndani ya kitabu hiki ili msomaji aweze kuvirejelea. Lakini bahati mbaya sana mengi ya matoleo mapya ya vitabu hivyo yamefanyiwa mabadiliko na baadhi ya sehemu kuondolewa, hususan zile zinazounga mkono madai ya Shia. Ufuatao hapa chini ni mfano mdogo tu wa yanayofanywa katika vitabu hivyo:

Katika ukurasa wa 301 wa juzuu ya 3 ya *Tafsir al-Kashshaaf* iliyokusanywa chini ya maelekezo ya Sheikh Mustafa al-Halabi (toleo la pili, 1319 A.H. liliochapishwa na Main Government Printing House ya Amiriah Bulaq ya Misri), beti zinazojitokeza ambazo kwazo Jarallah Zamakhshari, mfasiri wa *al-Kashshaaf,* alitangaza wazi imani yake katika uhalali wa

Ushia. Lakini katika toleo la mwaka wa 1373 A.H. kutoka Printing House Istiqamah bi ‘l-Qahara, shairi lililotajwa halionekani tena.

Marehemu Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi katika kitabu chake kiitwacho, *Uimamu,* ukurasa wa 37, anaandika kushangazwa kwake kutokana na maneno yaliyoondolewa katika kitabu cha *at-Tarikhat-Tabari,* chapa ya Leiden (ya mwaka 1879 Miladia). Chapa hii ya Leiden imeyanakili maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliyoyatumia wakati wa karamu mashuhuri ya ndugu wa karibu aliyoitayarisha ambapo katika khutba yake alisema: “Enyi watu wangu! Huyu Ali ni ndugu yangu, Wasii wangu na Khalifa wangu miongoni mwenu; msikilizeni na mtiini.” Lakini katika chapa ya Misri ya mwaka 1963, (chapa inayodaiwa kuwa imechekiwa na ile ya Leiden) maneno haya muhimu: “Wasii wangu na Khalifa wangu” yamebadilishwa na kuandikwa “kadha wa kadha” na kusomeka hivi: “Huyu Ali ni ndugu yangu na kadha wa kadha.” Huu ni msiba mkubwa.

Huu ni mchezo umefanywa na unaendelea kufanywa mpaka leo. Na lengo ni kuficha ukweli. Lakini hata hivyo, ‘ukweli siku zote unaelea’; matoleo ya zamani yapo mengi na yamehifadhiwa kwenye maktaba zetu. Ni muhimu kufikia kila aina ya maoni katika kujaribu kuamua ukweli. Uislamu kimsingi uko dhidi ya kufuata kibubusa. Utafiti huu umefanywa ili kuwaelemisha Waislamu kwa ujumla juu ya madhehebu za Kiislamu ili kujenga maoni yao kuhusu mtazamo mzuri wa mtu mwenyewe, na ni muhimu mtu kuelewa hoja za wale ambao hakubaliani nao. Inawezekana kusemwa kwamba wale ambao hawaelewi kabisa mtazamo wa maoni tofauti, hawaelewi kwa ukamilifu (mtazamo) wa kwao wenyewe.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake

yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Sheikh Harun Pingili kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

SAFARI YANGU KUELEKEA

MADHEHEBU YA AHLUL- BAYT

HADIYA

Kwa aliyezaliwa kwenye ngome ya umaasumu na uchaMwenyezi Mungu, na mashukio ya wahyi na uongofu, na mrithishwa wa fadhila tukufu na ukarimu.

Imwendee mwanamke mwema, na mpambanaji mtoa nasaha, aliye huru mkataaji, na ni muujiza Muhammadiyah, na ni hazina Haydaria, na ni amana Fatmiyah.

Imwendee aliyekuwa mtii wa Mwenyezi Mungu, katika hali ya siri na ya wazi, na aliyetoa changamoto kwa msimamo wake dhidi ya wanafiki na wafitini.

Imwendee aliyewatia hofu masultani wakorofi kwa msimamo wake thabiti, na alizishangaza akili kwa umadhubuti wa moyo wake, na alifanana na baba yake Ali kwa ushujaa wake, na alishabihiana na mama yake Zahra'a kwa utukufu wake na balagha yake.

Imwendee aliye nasibika na ukoo wa kinabii na uimamu, aliyetunukiwa shani ya cheo, utukufu na karama.

Imwendee shujaa wa Karbalaa bibi wa kibani Hashim. *Sayyidatiy wa Maulatiy Zaynab (a.s.).*


بسم الله الرحمن الرحيم

MLANGO WA KWANZA

DONDOO KUTOKA KATIKA MAISHA YANGU

﴿ أَفَمَن شَرَحَ ٱللَّهُ صَدۡرَهُۥ لِلۡإِسۡلَٰمِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٖ مِّن رَّبِّهِۦۚ فَوَيۡلٞ لِّلۡقَٰسِيَةِ قُلُوبُهُم مِّن ذِكۡرِ ٱللَّهِۚ أُوْلَٰٓئِكَ فِي ضَلَٰلٖ مُّبِينٖ ٢٢ ﴾

“Ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kuukubali uislamu, naye yuko katika nuru itokayo kwa Mola wake. Basi adhabu kali kwa wale wenye nyoyo ngumu kumkumbuka Mwenyezi Mungu, hao wako katika upotovu ulio bayana.” (*Sura Az-Zumar* : 22).

“Mwenyezi Mungu akimtakia kheri mja wake hufanya nukta nyeupe moyoni mwake, hivyo moyo huzunguka ukitafuta ukweli kisha anakuwa mwepesi mno kuielekea amri yenu kuliko ndege kuelekea kiota chake.”[1] (Imam Jafar Swadiq (a.s).

Siku za utoto:

Upendo ulikuwa unaniandama toka utoto wangu. Na hali ya kimaumbile ilikuwa inanifunga kuelekea kushikamana na dini, na sura iliyokuwa ikizunguka akilini mwangu na kupitia humo ikiuangalia mustakbali wangu haikutoka nje ya wigo wa kuwa mwanadini. Hivyo nilikuwa najiona binafsi kupitia njozi kuwa ni mtu niliye macho, shujaa, na askari wa kiislam mpambanaji, nairudishia dini heshima yake na Uislamu nguvu zake. Hapo nilikuwa sijaivuka daraja ya kwanza katika masomo yangu ya akademia. Kwa minajili hiyo fikra zangu zilikuwa fupi, na uelewa wangu kuhusu his-

1 *Biharul’anwar.* Juz. 5, Uk. 204.

toria ya waislam na maendeleo yao ni haba. Nilikuwa sijui isipokuwa baadhi ya visa kumuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) na vita vyake na makafiri, na ushujaa wa Imam Ali (a.s.) na uhodari wake.

Na baada ya kusoma kwetu historia ya dola ya Al-Mahdi katika nchi ya Sudan, nilivutiwa na shakhsia ya Uthman Deqnah, naye alikuwa mmoja miongoni mwa wakuu wa kijeshi wa jeshi la Al-Mahdi walioasi Mashariki ya Sudan. Mapambano yake yalikuwa yananivuta wakati ustadhi wetu wa somo la historia alipokuwa anatufanyia taswira ya ukakamavu wake na adhama ya shaksia, naye akiwa mpiganaji katika milima na mabonde. Kama hivyo moyo wangu uliungana naye, na nilijenga matarajio yangu niwe kama yeye.

Hapo nilianza kufikiri kulingana na akili yangu ya udogo, njia ya kulifikia lengo hili. Hivyo basi njia yangu pekee ambayo ilikuwa ninaifanyia taswira ni niwe mtu aliyehitimu chuo kikuu cha kijeshi, ili nipate kujifundisha fani za kivita na matumizi ya silaha, niliishi katika upendaji wa ukichaa kama huu miaka kadhaa katika umri wangu, mpaka nilipofikia sekondari hapo nilifunguka kifikra, na maarifa yangu yalizidi. Hapo niliwajua viongozi wa ukombozi katika ulimwengu wa kiislam, mfano wa Abdur Rahman Al-Kawakibiy, na As-Sanusiy, na Umar Mukhtar…na Jamalu din Afghaniy, naye ni mwanamageuzi stadi wa kivita, mwanafikra aliyechomoza kutokea Afghanistan na kuingia katika miji mikuu ya dola za kiislam na zisizo za kiislam akieneza fikra hai ambayo inagusa umbali wa kuchelewa katika ulimwengu wa kiislam na jinsi ya kuutibu.

Na kilichotilia nguvu mzinduko wangu ni zile mbinu zake alizokuwa akizifanya katika shughuli zake za kimapambano, miongoni mwa hekima na busara na kueneza taaluma na kutoa mwongozo kifikra kwa umma wa kiislam, bila ya kushika silaha…!

Nilikuwa naamini kuwa kila atakaye kufanya mapambano na kuwalinda waislam, hapana budi anyanyue upanga na aingie vitani na apigane, lakini

mbinu zake zilikuwa kinyume kabisa na nilivyokuwa nafanya taswira. Hivyo mbinu ya neno na taaluma ya uelewa ni kitu kipya kilichojitokeza katika fikra zangu za kidini, lakini mimi sikuweza kuachia kwa urahisi ambalo nililokuwa nimezijengea fikra zangu na utashi wangu, japokuwa niligundua kuwa tatizo la umma ni tatizo la elimu ya kiujumbe iliyoiva. Kwa kuwa taaluma ndio iwezayo kumbebesha kila mmoja jukumu lake.

Huyu ndie Jamaludin, amezunguka ulimwengu akieneza nuru yake na baraka zake, na anayeeneza fikra na elimu ambayo waislamu waliipokea kwa shangwe na taathira, kwa sababu ilikuwa inatatua matatizo yao na ilikuwa inaendana na hali yao halisi, hilo likazitisha nguvu za kikoloni zenye hikdi, na *Al-Urwatul'wuthqa*[2] pekee ndilo lilikuwa linawainulia sauti, ndio maana walifanya juhudi kuliwekea vikwazo na kulizuia kabisa lisitoke.

Hivyo kujiuliza ambako kulikuwa kunanishawishi ni: Vipi huyu mtu mmoja pekee aliweza kubadilisha ule uwiano wa uzito, na vipi alizitisha nguvu hizi zenye kiburi?!

Na ili kujibu swali hili, mbele yangu kulifunguka mlango mkuu wa maswali, baadhi yalikuwa rahisi na baadhi hayakuwa na jibu katika hali halisi ya Sudan, ni miongoni mwa ambayo yalinifanya mimi nijaribu kujikomboa mbali na hali hii halisi, na nifungue kila vifundo na vifungo ambavyo vilikuwa vinaniita nisalimu amri na niwe mnyenyekevu kwenye hali hii halisi ya kidini, ili niweze kwenda katika maisha haya kama walivyokuwa baba zangu na babu zangu, lakini kutambua kwangu jukumu na kumpenda kwangu Jamaludin ilikuwa ni kengele yagongwa kwenye kamba ya maumbile yangu. Nilikuwa najiuliza:
Vipi nitaweza kuwa mfano wa Jamaludin?! Na je dini ambayo nimeirithi itaweza kunibeba mimi kuifikia daraja ile? Kisha nasema: Kwa nini isiwe

[2] Al-U'rwatul'wuthqa ni jarida alikuwa analitoa Jamalu-din na mwanafunzi wake Muhammad Abduh huko London.

hivyo? Hivi Jamaludin alikuwa na dini isiyokuwa hii dini yetu? Na ni Uislamu wa aina nyingine sio huu wetu?

Ili kujibu niliduwaa miaka mingi na lote nililofikia ni kubadilisha uelewa wangu wa dini kabisa, hivyo nilifikia kumuona Jamaludin ni uongozi na ni mfano ikiwa hapo kabla alikuwa Uthman Deqnah, na nilibadilika kwa njia hiyo, hivyo badala ya kuwa chuo cha kijeshi ndiyo tumaini langu, ikawa tumaini langu ni njia iliyo salama itakayo nitambulisha mimi fikra na taaluma asili ya kiislam ambayo kupitia hiyo mwamko wa kiislamu utakuwa.

Mwanzo ulikuwaje:

Ilikuwa kutafuta utaratibu na fikra iliyowiva na taaluma itakiwayo ni vigumu, na daraja hii ilikuwa chungu, japokuwa utafiti wangu ulikuwa kwa sura ya msamaha na wa kimaumbile. Katika maisha yangu ya kawaida nilikuwa nauliza na kujadili na vinginevyo, wala hapakuwa na utayarifu wa kutafiti na kuhimili. Na baada ya uvamizi mkali wa mawahabi kuivamia Sudan, na kushika kasi malumbano na mijadala na kukithiri kwa harakati za kidini, ukweli mwingi ulifichuka, na zikajitokeza tofauti na mifarakano mingi ya kihistoria, kiitikadi na kifiq'hi. Na tendo la kuvikufurisha baadhi ya vikundi na kuvitoa nje ya tanzi la uislamu ilianza, ni miongoni mwa mambo ambayo yalisababisha mfarakano wa kimadhehebu na safu kutengana. Pamoja na uchungu wa yaliyotokea, nilipata utashi wangu na udadisi wangu ulizidi, na nilikuwa naona uhalisi wa yale maswali yaliyokuwa yanaishawishi akili yangu.

Hapo basi hima yangu ya kuutilia maanani uwahabi ilizidi, nilikuwa nafuatilia mijadala yao na mikusanyiko yao ambayo ilikuwa inanifunga mimi. Na ambalo ni la muhimu nililojifunza kutoka kwao katika ngazi ile, ni ujasiri na kuukabili ukweli na kuukinza, nami nilikuwa naamini kuwa ukweli ni kitu kitakatifu na ni mwiko kuuhujumu au kuupinga, japokuwa uangalizi wangu ulikuwa mwingi kuuhusu, ambapo aghlabu nilikuwa sian-

galii kupitia dhati yangu na umbile langu, hivyo basi nilikuwa najizuia sana matendo na zoezi za jamii ya kidini.

Niliendelea nao, na ilijiri kati yangu na wao mijadala mingi, ambayo ukweli wake ulikuwa yale maswali ambayo yalikanganya akili yangu, baadhi yake nilipata majibu yaliyoniridhisha katika ngazi ile, na kulikuwa na maswali sikupata majibu yake kutoka kwao, hilo lilikuwa dhamana tosha kwangu kuwaelemea na niwaunge mkono, japokuwa kulibaki baadhi ya mazingatio ambayo yalikuwa kizuizi kati yangu na kujihusisha moja kwa moja na mwendo wa kiwahabi. La kwanza na la muhimu ni kuwa mimi sikupata kwao nitoshekalo nalo, ambalo laweza kuwa jibu la matamanio yangu ya kiujumbe. Na wakati mwingine wasiwasi ulikuwa unanichukua kwa kauli yake:
Kwa kweli unalolifikiria na kulitafiti ni kitu cha mfano tu hakina ukweli, na uwahabi ni sampuli bora ya uislamu na hapana kitu badala yake….

Nilikuwa nasukumwa na wasiwasi huu na kuusadiki kwa kutokuwa kwangu na maarifa na fikra za vyuo vingine, lakini haraka nilikuwa na'ngamua kuwa ambalo Jamaludin amelifanya haiwezekani liwe ndio hii fikra ya kiwahabi. Kwa hiyo nilikuwa nasema waziwazi: Kwa kweli Uwahabi ni njia ilio karibu mno kuelekea Uislam, kwa sababu yale wayafanyayo kuonyesha dalili, na matamko rasmi ya kisheria ili kuthibitisha ukweli wa madhehebu yao, ni jambo ambalo sijaliona katika vikundi vingine humu (nchini) Sudan. Lakini tatizo lao ni kuwa madhehebu hii waliojijengea yashabihiana mno na kanuni za hisabati, kwani yenyewe ni desturi na kanuni iliyoganda, hutekelezwa bila ya kuwa na akisi ya kimaendeleo iliyo wazi katika maisha ya mwanadamu. Na katika fani ya kuamiliana na dunia hii katika nyanja tofauti za mtu mmoja au za kijamii au ya kiuchumi au kisiasa… na hata jinsi ya uhusiano na Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Bali ni kinyume kabisa mara nyingi humfanya mtu awe mkiwa mwenye kujitenga mbali na jamii, kwa aliyonayo miongoni mwa ufinyu wa fikra katika kila mikato yake. Mtu miongoni mwao hawezi kuishi na jamii bali

huwa ni mwenye kujipambanua mbali nao kwa vazi lake na mwenendo wake na katika kila sehemu ya maisha yake, na hata jinsi ya uongeaji wake, hazoeani ila na watu wa aina yake. Nilikuwa nahisi kuwa wameghurika na wenye kiburi na dharau kwa kuwa wao huwaangalia watu wengine wakijiona wao wako juu, hawana maingiliano nao wala hawashirikiani nao katika maisha yao.

Vipi watashirikiana nao?! Hali kila lifanywalo na jamii – ya kiislamu - kwao ni bidaa na upotovu. Mimi nakumbuka vyema ulipoingia mvuto wa kiwahabi kijijini petu katika muda mfupi na bila ya darasa lolote wala uelewa, kundi kubwa la vijana walijiunga kwenye uwahabi, hawakuendelea muda mwingi wote walijitoa, na hili lilikuwa ndio tazamio langu, kwa sababu madhehebu mpya imewazuia kuchanganyika na jamii na iliwaharamishia kawaida nyingi ambazo walilelewa nazo, hali zikiwa haziendi kinyume na dini.

Na jipya nikumbukalo ni kuwa, miongoni mwa vitu ambavyo vijana waliojiunga na uwahabi walikuwa wanataabika navyo, ni kwamba ilikuwa ni kawaida kijijini petu vijana zama za usiku wa mbaramwezi hujumuika na kuketi kwenye mchanga ulio safi wanapitisha wakati wao huko, nao ni wakati pekee wa kuonana vijana wa kijijini ambao wanafanya kazi mchana kutwa katika mashamba yao na katika shughuli zao walizozizoea, basi Sheikh wao alikuwa anawazuia kufanya hivyo na kuwaharamishia tendo hilo kwa hoja ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ameharamisha kukaa njiani, japokuwa sehemu hizi hazizingatiwi kuwa ni njia.

Na la pili, nalo ni tatizo la kila wahabi, kuwa mmoja miongoni mwao kwa muda mdogo wa kuwa mwanadini na kwa elimu ndogo aliyonayo, mara anakuwa mufti anayo haki ya kutoa fatwa kuihusu mas'ala yoyote iwayo. Nakumbuka siku moja mmoja wao alikuwa ameketi na mimi nikijadiliana naye katika mambo mengi, katikati ya mjadala aliinuka aliposikia sauti ya adhana ya magharibi kutoka msikiti wao, nilimwambia: Tulia hebu tukamilishe mazungumzo yetu. Akasema: Hapana maongezi, umeingia

wakati wa swala, haya twende tuswali msikitini. Nilimwambia: Mimi nitaswali nyumbani mwangu. Japokuwa nilikuwa nadumisha kuswali nao, lakini akasema kwa sauti ya juu kabisa: Swala yako ni baatili. Nilisitushwa na kauli hii, na kabla sijapata tafsiri aligeuza mgongo wake aondoke, nilimwambia: Ngoja kidogo, nini sababu ya kubatilika kwa swala yangu nyumbani? Alisema (kwa fahari kabisa na kujisikia): Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: “Hapana swala kwa aliye jirani na msikiti ila ndani ya msikiti.”

Nilimwambia: Hapana tofauti juu ya ubora wa swala ya jamaa msikitini, lakini hilo halimaanishi kuondoa usahihi wa Swala mahali pengine, na Hadith inalenga kutilia nguvu ubora huu, hailengi kubainisha hukumu ya swala nyumbani, na dalili juu ya hilo ni kwamba hatujaona katika fiq’hi kuwa miongoni mwa yabatilishayo swala ni kuswali nyumbani, wala mwanachuoni yeyote hajatoa fatwa katika mas’ala hii. Pili ni kwa haki gani uliyonayo inayokufanya utoe hukumu kama hizi?! Je hivi wewe ni mwanachuoni?! Na ni vigumu sana mtu atoe fatwa na abainishe hukumu ya maudhui maalum, mwanachuoni huzifanyia darasa nususu zote mfano wa mahali hapa, na apaswa atambue dalili ya amri na katazo katika nassu, je amri hii yajulisha wajibu au istih’babu, na katazo je lajulisha uharamu au ni makuruhu, dini hii ina kina kirefu basi ingia humo polepole.

Alianza kutetereka usoni kwake, alikunja uso na alifura kisha akasema: “Wewe unaifanyia tafsiri Hadith na tafsiri ni haram.” Na alikwenda.

Jambo langu niliacha hesabu yake kwa Mwenyezi Mungu kutokana na mpumbavu huyu ambaye hafahamu kitu. Akili hii ngumu kama jiwe, ilikuwa sababu ya pili ambayo ilinizuia nisiwe wahabi, japokuwa nil-iathirika sana na fikra zao, kwa hiyo nilikuwa ninashikamana nazo na kuz-ihami.
Nilibaki katika hali hii kwa muda nikiyumba sina kituo wala mwelekeo, nakuwa karibu na uwahabi wakati mwingine na najiweka mbali nao wakati mwingine, na niliona kuwa ufumbuzi pekee mbele yangu badala ya chuo

cha mafunzo ya kijeshi, nisome katika chuo au chuo kikuu cha kiislam ili niendelee na utafiti wangu kwa njia ya undani na mazingatio zaidi. Na baada ya mtihani wangu wa kujiunga na chuo kikuu, kulikuwa na mapendekezo sita kutoka vyuo vikuu na taasisi ambazo mwanafunzi angependa kusoma. Sikuchagua isipokuwa vyuo vikuu, na vyuo vya kiislam. Na nilikubaliwa katika kitivo miongoni mwa vitivo vya kiislam, (nacho ni kitivo cha masomo ya kiislam na kiarabu katika chuo kikuu cha *Wadi Nnil Sudan)*.

Niliruka kwa furaha, na nilijiandaa kwa ajili ya daraja hii mpya maishani mwangu. Na baada ya mazoezi ya kijeshi (Ulinzi wa raia) ambao haiwezekani kujiunga na chuo kikuu ila baada ya kumaliza mazoezi hayo, misafara ya wawakilishi ilianza kutoka pande tofauti za Sudan ikija chuo kikuu na mimi nilikuwa wa kwanza wao, na wakati wa mahojiano, mkuu wa chuo aliniuliza mtu ambaye nimevutiwa naye mno maishani mwangu? Nilimwambia: Jamaludin Afghaniy, na nilimfafanulia siri ya kuvutiwa kwangu naye… alionyesha kufurahiwa kwake na maneno yangu. Na baada ya maswali mengi nilikubaliwa rasmi chuoni. Na baada ya hapo niliingia maktaba ambayo ilikuwa na vitabu vingi na vitabu vya rejea vikubwa, kwa hiyo nikawa nimejiambatanisha nayo, lakini tatizo ambalo lilinikabili ni nianzie wapi? Na kitu gani nisome?!

Nilibaki na hali hii, natoka kitabu hadi kitabu, kabla sijajiwekea utaratibu, mmoja katika watu wa ukoo wangu alinifungulia mlango mpana na muhimu wa kutafiti na kuchimba. Nao ni somo la historia na kufuatilia madhehebu za kiislam ili kuitambua iliyo ya kweli kati ya hizo madhehebu. Na ufunguzi huu ulikuwa ni taufiki ya kiungu ambayo haikuwa katika hesabu yangu, nilipokutana na ndugu yangu wa ukoo wa Abdul Mun’imu, ambaye ni mhitimu wa chuo kikuu cha sharia, nyumbani kwa mtoto wa ammi yangu katika mji wa Atibarah.

Na kabla ya kuzama jua, nilimuona katika ukumbi wa nyumba akijadiliana na mtu mmoja miongoni mwa *Ikh’wanul’muslimina* ambaye alikuwa

mgeni nyumbani, nilisikiliza ili nione wanachojadiliana, niliharakia kuwaendea, hivyo nilipojua hali ya mjadala kuwa ni katika mambo ya dini. Niliketi karibu yao nikiangalia maendeleo ya mazungumzo ambayo Abdul'mun'im alitambulika kwa utulivu kabisa licha ya kuwepo kwa ghasia na hujuma upande wa pili, sikuwa najua aina ya mjadala kiukamilifu mpaka aliposema ndugu mwislamu: "Shia ni makafiri mazandiki!!"

Hapo nilitanabahi na niliangalia kwa makini, lilizunguka akilini mwangu swali la kushangaza: Shia ni akina nani? Na kwa nini wao wazingatiwe kuwa makafiri? Hivi Abdul Mun'im ni Shia? Na asemayo si usemi wa kawaida, je huo ndio usemi wa Shia?!.

Kwa ajili ya kuchunga insaafu kwa kweli Abdul'mun'imu alimkwamisha hasimu wake katika kila mas'ala iliyoletwa kwenye mjadala, achia mbali busara ya maneno yake na nguvu za hoja yake.

Na baada ya kumalizika mazungumzo, na kutekelezwa kwa swala ya magharibi nilijitenga na mwenzangu Abdul'mun'im, nilimuuliza kwa heshima zote: Hivi wewe ni Shia? Shia ni akina nani? Wapi ulijuana nao?

Akasema: Polepole..... swali baada ya swali.
Nilimwambia: Samahani, mimi ningali nimeshangazwa na niliyosikia toka kwako.

Akasema: Huu ni utafiti wa muda mrefu, na ni juhudi ya miaka minne kwa taabu na mashaka, na yasikitisha kuwa tija haijatumainiwa.

Nilimkatisha: Ni tija gani hii?
Akasema: Rundo za ujinga na kufanywa wajinga, tumeishi na hali hiyo maisha yetu yote tukikimbia nyuma ya jamii zetu bila ya kuuliza, je dini tuliyonayo ndiyo iliyokusudiwa na Mwenyezi Mungu (s.w.t.), nayo ndio Uislam? Na baada ya mjadala ilibainika kuwa haki ilikuwa upande wa njia ya mbali zaidi kwa kufanya taswira kwa mtizamo wangu, nao ni Shia.

Nilimwambia: Labda wewe umefanya haraka ..... au umechanganya mambo..!

Alitabasamu huku akisema: Kwa nini wewe haufanyi utafiti kwa kuzingatia na kuvuta subira? Na hasa ikizingatiwa kuwa ninyi mnayo maktaba hapo chuoni, itakusaidia sana kwa jambo hili. Nilisema katika hali ya (kustaajabishwa): Maktaba yetu ni ya kisunni, vipi niutafiti Ushia?!

Akasema: Miongoni mwa dalili za ukweli wa Shia wanatoa dalili ya kuwa kwake sahihi kutoka vitabu vya riwaya za wanavyuoni wa kisunni, humo ndio ukweli wao wadhihiri kwa sura ya wazi zaidi.

Nilisema: Hivi vyanzo vya Shia ni vilevile vyanzo vya Ahli Sunnah?!

Alijibu: Hapana, Shia wana vyanzo mahsusi vinavyovizidi mara kadhaa vyanzo vya Ahli Sunnah, riwaya zake zote zimeelezwa na Ahlul-Bayt (a.s.) kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), lakini wao hawatolei hoja kwa Ahli Sunnah kupitia riwaya zitokazo kwenye vyanzo vyao, kwa kuwa wao masunni hawana ulazima nazo, hivyo basi hapana budi watoe hoja dhidi yao kwa dalili wanazozikubali, yaani (kulingana na usemi mashuhuri): Walazimisheni kwa ambalo wamejilazimisha nalo wao wenyewe.

Yalinifurahisha maneno yake na mwitikio wangu kuuelekea mjadala ulizidi. Nilimwambia: Nitaanzaje? Akauliza je katika maktaba yenu kuna *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim*, *Musnad Ahmad*, *Tirmidhiy* na *Nasaiy*? Nilisema: Ndio, tuna kiwango kikubwa cha vyanzo vya Hadith.

Akasema: Anza na hivi, kisha baada ya hapo njoo kwenye tafsiri, na vitabu vya historia, kwa kuwa katika vitabu hivi kuna Hadithi zinazojulisha wajibu wa kuifuata madrasa ya Ahlul-Bayt. Alianza kuniorodheshea mifano, pamoja na kutaja chanzo na namba ya jalada na ukurasa.

Nilisimama nimeduwaa, nikizisikiliza Hadithi hizi ambazo sijapata kuzisikia hapo kabla, ilinifanya niingie shaka kuwepo kwake katika vitabu vya kisunni, lakini haraka sana aliikata shaka hii kwa kauli yake: Zisajili Hadithi hizi, kisha zitafute katika maktaba na tukutane siku ya Alhamisi ijayo kwa idhini yake Allah.

Chuoni:

Baada ya kuzifuatilia zile Hadithi katika *Bukhari*, *Muslim*, na *Tirmidhiy* huko maktaba ya chuo chetu, ulinithibitikia ukweli wa usemi wake, na nilisitushwa na Hadithi zingine zilizo zaidi ya hizi kwa dalili za wajibu wa kuwafuata Ahlu-Bayt, jambo lililonifanya niishi katika hali ya mshtuko. Kwa nini hatujasikia Hadithi hizi hapo kabla?

Nilizionyesha kwa baadhi ya wenzangu chuoni ili washirikiane na mimi katika wakati huu muhimu, baadhi waliathirika na baadhi hawakujali, lakini mimi niliazimia kuendelea na uchunguzi hata kama kufanya hivyo kutanigharimu umri wangu wote. Ilipowadia siku ya Alhamisi, nilikwenda kwa Abdul'mun'imu, alinipokea kwa mapokezi mema kwa utulivu na akasema: "Ni wajibu juu yako usiharakie na uendelee na utafiti kwa ufahamu wote."

Kisha tulianza uchambuzi wa mambo mengine mbalimbali, uliendelea mpaka jioni ya siku ya Ijumaa, nilifaidika na mengi na nilivijua vitu vingi ambavyo nilikuwa sivijui, na kabla ya kurejea kwangu chuoni aliniomba vitu vingi nivitafute. Iliendelea hali kama hii kwa muda, na hali ya mjadala kati yangu na yeye ilikuwa ikibadilika kati ya muda na muda, kwani wakati mwingine nakuwa mkali wa maneno kwake, na pengine nafanya inadi kwenye ukweli uliowazi. Kwa mfano nilikuwa ninaporejea baadhi ya Hadithi katika vyanzo na ninakuwa na uhakika kuwa ipo, huwa namwambia: "Kwa kweli Hadithi hizi hazipo." Mpaka sasa sijui ni kitu gani kilikuwa kinanisukuma nifanye hivyo ila ni kutambua kushindwa na utashi wa ushindi.

Kwa sura kama hii na kwa uchambuzi wa ziada mbele yangu ukweli mwingi ulifichuka mbele yangu ambao ilikuwa sikuutazamia, na nilikuwa katika muda wote huu nafanya mjadala sana na wanafunzi wenzangu, na wenzangu walipoona nawakera waliniomba nijadiliane na Dkt. aliyekuwa akitufundisha *Fiq'hi*, nikasema: Hapana kizuizi kwangu, lakini tu kuna vizuizi kati yangu na yeye ambavyo vinanizuia kuwa na uhuru wa kuongea. Hawakukinaika na hili, na wakasema: Kati yetu na wewe kuna Ustadh, ukimtosheleza sisi tu pamoja na wewe.

Nikasema: Mas'ala sio kutosheka, bali ni dalili na uthibitisho, na kutafuta ukweli. Na katika somo la kwanza la *fiq'hi* nilianza mjadala naye kwa sura ya maswali mengi, nilimuona hanipingi sana bali ni kinyume alikuwa anatilia mkazo kuwapenda Ahlul-Bayt (a.s.) na kuwa kuwafuata na kuzitaja fadhila zao ni lazima. Na baada ya siku nyingi aliniomba niende kwenye maktaba yake kwenye makao ya chuo na baada ya kwenda kwake alinipa kitabu chenye juzuu kadha nacho ni (*Sahihul-Kaafiy*), ambacho ni miongoni mwa vyanzo vya Hadithi vinavyoaminika mno kwa Shia. Aliniomba nisikipuuze kitabu hiki kwa kuwa ni turatha ya Ahlu-Bayt. Sikusema kitu kwa situkizo kama hili, nilichukua kitabu na nilimshukuru kwa hilo. Nilikuwa nakisikia kitabu hiki na sikupata kukiona, ni jambo ambalo lilinifanya nimshuku kuwa ni Shia Dr. huyu, pamoja na kuwa namtambua kuwa ni mfuasi wa Malik, na baada ya swali na kutaka tafsiri yake ilinibainikia kuwa yeye ni *Sufiy*, ni mwenye kujihusisha na kuwapenda Ahlul-Bayt (a.s.).

Na wenzangu walipotambua maafikiano haya kati yangu na huyu ustadh, waliniomba nifanye mjadala na ustadhi mwingine aliyekuwa akitusomesha mada ya Hadith, na alikuwa mtu wa dini sana mnyenyekevu mwenye tabia njema. Na nilikuwa nampenda sana, nilikubali ombi lao, na ilianza kati yetu mijadala mingi, na nilikuwa namuuliza usahihi wa baadhi ya hadithi, alikuwa anatilia mkazo kuwa ziko sahihi, na baada ya muda nilihisi kutopenda kwake na kutoridhika kwake na mjadala wangu, pia wenzangu walihisi hivyo, hapo niliwaza njia bora ya kuendelea na mjadala ni

maandishi. Hivyo basi nilimwandikia jumla ya Hadithi na riwaya ambazo kwa wazi zajulisha wajibu wa kufuata madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) na nilimwomba atafiti usahihi wake. Na nilikuwa namuuliza kila siku juu ya majibu, naye hutoa udhuru kuwa hajafanya utafiti. Nilimfuatilia kwa njia hii mpaka alihisi kuwa namdhiki.

Akaniambia zote ni sahihi. Nikasema kwa kweli ziko wazi zikihusu wajibu wa kuwafuata Ahlul-Bayt. Hapo hakujibu na aliondoka haraka kwenda maktaba.

Mwenendo huu ulikuwa ni situsho kwangu na ni jambo lililonifanya nione ukweli wa usemi wa Shia. Lakini nilipenda kwenda polepole na kutoharakia hukumu.

Na miongoni mwa ajabu ya tukio la bahati ni kwamba mkuu wa chuo naye ni ustadhi Ulwan, alikuwa anatusomesha somo la tafsiri, siku moja akasema katika kutafsiri kauli yake (s.w.t): “Kwa kweli Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alipokuwa Ghadiir Khum, alinadi kuwaita watu wakajikusanya, aliushika mkono wa Ali (a.s.) akasema: “Ambaye mimi ni mtawala wake hivyo Ali ni mtawala wake.”

Tukio hili habari zake zilienea nchini na zilimfika Al-Harith bin Nu’man Al-Fahri, huyu bwana alimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akiwa juu ya ngamia wake, alimsimamisha ngamia wake na aliteremka na akasema: “Ewe Muhammad, umetuamrisha kutoka kwa Mwenyezi Mungu tushuhudie kuwa hakuna miungu ila Allah na kuwa wewe ni Mjumbe Wake, hilo tulilikubali kutoka kwako, na ulituamrisha tuswali Swala tano tukakubali, na ulituamrisha kutoa Zaka tulikubali, na ulituamrisha tufunge mwezi wa Ramadhan tukakubali, na ulituamrisha kuhiji tukakubali, halafu haukuridhika na hayo mpaka umenyanyua mabega ya mtoto wa ami yako ukimfadhilisha juu yetu na ukasema: “Ambaye mimi ni mtawala wake hivyo Ali ni mtawala wake.” Je kitu hiki ni kutoka kwako au ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Nabii (s.a.w.w) akasema: “Naapa Mwenyezi Mungu ambaye hakuna miungu ila ni Yeye, kwa kweli hili ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka.”

Al-Harith aligeuka kumuelekea ngamia wake huku akisema: “Ewe Mwenyezi Mungu ikawa ayasemayo Muhammad ni haki, basi tutiririshie mvua ya mawe toka mbinguni, au tuteremshie adhabu iumizayo.” Hakuwahi kufika kwenye ngamia wake ila Mwenyezi Mungu alimtupia jiwe lililoanguka kichwani kwake na lilitoka kwenye tundu yake ya chini. Hapo Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliteremsha Aya:

﴿ سَأَلَ سَآئِلٌۢ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ۝١ لِّلْكَٰفِرِينَ لَيْسَ لَهُۥ دَافِعٌ ۝٢ مِّنَ ٱللَّهِ ذِى ٱلْمَعَارِجِ ۝٣ ﴾

“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Juu ya makafiri, hapana awezaye kuizuia. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye utukufu mkubwa.” (*Sura Maarij*: 1 -3).

Na baada ya kumaliza darasa, mmoja katika rafiki zangu alikutana naye, na alimwambia: “Kwa hakika uliyosema ni maneno ya Shia.” Ustadhi alisimama kidogo kisha alimwangalia huyu mpinzani na akamwambia: ‘Niitie *Muutaswim* aje kwenye ofisi ya idara..! Nilistaajabishwa na wito huu. Niliogopa kukutana na ustadh, lakini nilikata shauri na nilikwenda kwake, na kabla sijakaa akasema: “Wanasema kuwa wewe ni Shia!”

Nikasema: Mimi ni mtafiti tu.
Akasema: Kwa kweli kutafiti ni vizuri na hapana budi.
Ustadh akawa ananitajia mambo yenye utata kuwahusu Shia ambayo mara nyingi yalikuwa yanarudiwarudiwa, Mwenyezi Mungu alinisaidia kujibu kwa dalili na uthibitisho wenye nguvu mno, niliunguruma na Hadithi kwa nguvu zaidi kuliko nilivyokuwa ninategemea, na kabla sijahitimisha mazungumzo yetu aliniusia nisome *Al’Muraajaati*, na akasema: “Ni katika vitabu vizuri katika uwanja huu.”

Na baada ya kuwa nimesoma kitabu *Murajaati* na *Maalimul'madrasatayn* na baadhi ya vitabu vingine, ukweli uliniwia wazi na batili ilitanzuka, kwa dalili zinazong'ara na uthibitisho utoao mwanga kuthibitisha ukweli wa madhehebu ya Ahlu-Bayt katika vitabu viwili hivi. Nguvu zangu za mjadala na utafiti zilizidi, mpaka Mwenyezi Mungu alinifichulia nuru ya ukweli moyoni mwangu, nikautangaza Ushia wangu!

Baada ya hapo nilianza ngazi mpya ya mapambano, ya wale ambao walishindwa kupata njia kwenye mjadala, ila ni kebehi, matusi, shutma, vitisho na masingizio, na yasio hayo miongoni mwa mbinu za kijinga, lakini nilihesabia hili jambo langu kwa Mwenyezi Mungu na nikafanya subira kwa yaliyojiri, japokuwa mapigo yaliyolengwa kwangu yalikuwa ni kutoka kwa rafiki zangu wapendwa mno ambao walipiga marufuku kula, na kulala chini ya sakafu moja na mimi. Na nilitengwa kikamilifu, isipokuwa na baadhi tu ya ndugu waliokuwa na ufahamu zaidi na wenye kujizuia. Na baada ya muda niliweza kurudisha uhusiano wangu na wote na kwa sura nzuri zaidi kuliko ya kwanza bali nilikuwa naheshimiwa na kuthaminiwa kati yao, na baadhi yao walikuwa wananitaka ushauri kwa dogo na kubwa katika mambo ya maisha yao.

Lakini hali hii haikuendelea muda mrefu, moto wa fitna ulilipuka upya, baada ya wanafunzi watatu walipotangaza Ushia wao, zaidi ya hapo ni kuwa kundi kubwa la wanafunzi walidhihirisha kuelemea kwangu na kuuunga mkono Ushia, hapo kukaibuka mlolongo mwingine wa mapigo na mifadhaisho, katika yote hayo tulishikamana na tabia njema za kiujumbe na hekima, kwa hiyo tuliweza kuzifyonza ghadhabu haraka iwezekanavyo.

Kijijini kwetu:

Kijiji chetu ni Nudaa, ni miongoni mwa vijiji vidogo kaskazini mwa Sudan kwenye kingo za mto Nile, wengi katika wakazi wake ni wa kabila ya Rubaataab, kabila hili ni mashuhuri kwa werevu na haraka hudhihirikiwa, wakazi wake wanategemea mitende na kilimo cha mavuno ya msimu.

Mawahabi walifaidika na uzuri wa watu hawa kuieneza fikra ya kiwahabi, waliathiri kwa njia isio ya moja kwa moja akili zao na fahamu zao, kwa sababu ya kukithiri mihadhara na vikao wanavyofanya, mwanzo nilionyesha kujizuia, na wakati wangu niliutumia kwa kusoma na kutaka kujua na kuifanyia daawa madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) kati ya ndugu na watu wa karibu. Na ilijiri kati yangu na kaka yangu mijadala mingi na malumbano kiasi ilifikia akatae kusoma vitabu vya Shia na alinitishia kuwa ataviunguza, na baada ya mjadala niliweza kumwathiri, na alisoma baadhi ya vitabu mfano wa *Ahlul-Bayt Qiyadatur-Rabbaniyah*, *Al'murajaatu*, *Maalimul'madrasatayni* mpaka Mwenyezi Mungu alipomuongoza kwenye nuru ya Ahlul-Bayt (a.s.), hivyo aliutangaza Ushia wake. Ama kuhusu ahali wengine waliobaki, wengi wao wamedhihirisha kuelemea kwao na kuunga kwao mkono.

Kwa hiyo habari zangu zilienea kijijini, na nilianza kuifikisha madhehebu ya Ahlul-Bayt kwa wakazi wake wengi. Hivyo moto wa mawahabi ulikolea na ghadhabu ya wanaousambaza ikatokota, kwa hiyo ikawa kila mhadhara wao katika jambo lolote ni kuwatukana na kuwashutumu Shia na kuwasingizia, na wakati mwingine wananichokoza mimi mwenyewe, na yote hayo nilikabiliana nayo kwa uvumilivu na msamaha mwema.

Mjadala na Sheikh wa kiwahabi:

Kulifanyika mazungumzo kati yangu na Sheikh wao - Ahmad al-Aminiy na nilimuomba kutumia busara na kuacha utashi, batili na hujma bila ya faida, na baada ya kuzidi kipimo na kuzidi ghasia zao na kasumba zao nilikwenda msikitini kwao na niliswali nyuma yake Swala ya dhuhuri, na baada ya kwisha Swala nilimuuliza: "Je kuna siku yoyote nilikuchokoza muda huu wote, ambao wewe unawatukana Shia na unawakufurisha kwa kutumia kipaza sauti?!"
Akasema: Hapana.
Nikasema: Wajua kwa nini?!
Akasema: Sijui.

Nikasema: Kwa hakika maneno yako ni hujuma na ujinga, na uchokozi dhidi yangu, nilihofia kukupinga ingekuwa kujihami nafsi yangu na si kuuhami ukweli, kwa hiyo sasa nakuomba mjadala wa kielimu wenye nidhamu, mbele ya wote ili ukweli ufichuke.

Akasema: Hapana kizuizi kwangu.

Nikasema: Basi ainisha duru husika za mjadala.

Akasema: Kuibadilisha Qur'anii, na uadilifu wa Sahaba.

Nikasema: Vyema, lakini kuna mambo mawili ya dharura hapana budi yajadiliwe, nayo ni sifa za Mwenyezi Mungu, na unabii katika itikadi yenu na riwaya zenu.

Akasema: Hapana.
Nikasema: Kwa nini?
Akasema: Mimi ninaainisha mjadala, mimi nikikuomba mjadala, haki itakuwa yako kuainisha mjadala.
Nikasema: Hatutofautiani (kwa hilo)…lini ahadi yetu?
Akasema: Leo, baada ya Swala ya magharibi. - Akidhania atanitisha kwa muda huu mfupi wa ahadi - basi nilidhihirisha kuafiki kwangu kwa furaha kabisa, nikatoka msikitini.

Na baada ya kutekeleza Swala ya magharibi, mjadala ulianza, sheikh wao Ahmad Amiin alianza mazungumzo kama kawaida yao kwa hujuma na kuwatuhumu Shia kwa kuifanyia Qur'anii mabadiliko (*tahriif*). Mkononi mwake alikuwa ameshika kitabu *Al-Khututu Al-Ariidhwa* cha Muhibudin, na baada ya kumaliza maneno yake nilianza maneno yangu, nilianza kwa ufafanuzi kupinga yote aliyoyazua miongoni mwa tuhuma, na niliwatakasa Shia kwa kuwaweka mbali kabisa na usemi wa kuifanyia Qur'anii mabadiliko (*tahriif*), na baada ya hivyo, nilimwambia kama alivyosema Isa (a.s.): "Mwaliona kapi machoni kwa wengine na wala hamulioni gogo

machoni kwenu.”

Kwa kuwa riwaya ambazo zimo katika vitabu vya Hadithi vya masunni ni dhahiri zinaituhumu Qur’anii tukufu kuwa imefanyiwa mabadiliko (*tahriif*), basi kuinasibisha kauli ya mabadiliko (*tahriif*) kwa Sunni masafa yake ni ya karibu mno kuliko kuinasibisha kwa Shia. Nilitaja karibu riwaya ishirini pamwe na kutaja chimbuko, na namba ya ukurasa kutoka katika *Sahih Bukhari*, *Muslim*, *Musnad Ahmad*, *Itqaan Fii Ulumil’Qur’ani* ya Suyuti.

Mfano: Imam Ahmad bin Hanbal ametoa maelezo katika *Musnad* yake, kutoka kwa Ubayya bin Ka’ab, amesema: “Mnaisoma Aya ngapi Sura Ahzabi?” Akasema: “Aya sabini na kidogo.” Akasema: “Bila shaka niliisoma pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) mfano wa Baqarah au zaidi yake, ikiwemo Aya ya kupopoa mawe.”[3]

Na Bukhari ametoa maelezo katika *Sahih* yake kwa sanadi yake kutoka kwa Ibnu Abbas kuwa Umar bin Khattab alisema: “Kwa kweli Mwenyezi Mungu alimtuma Muhammad (s.a.w.w) kwa ukweli na alimteremshia kitabu ikawa miongoni mwa aliyoteremsha Mwenyezi Mungu ni Aya ya *rajmu* na tuliisoma na tuliitia akilini na tuliielewa ndio maana Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alifanya *rajmu* na tulifanya *rajmu* baada yake. Kwa hiyo naogopa muda ukiwa mrefu kwa watu asije kusema msemaji: Wallahi hatuikuti Aya ya *rajmu* katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, kwa hivyo watapotea kwa kuacha faradhi aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu….. Kisha sisi tulikuwa tukisoma katika tuyasomayo katika kitabu cha Mwenyezi Mungu:

[3] *Musnad Ahmad*, jalada,5,Uk.131.

أن لا ترغبوا عن آبائكم فإنّه كفر بكم أن ترغبوا عن آبائكم وإنّ كفرا بكم أن ترغبوا عن آبائكم.

(Msijitenge na baba zenu, kwani bila shaka ni ukafiri kwenu kujitenga na baba zenu. Na ahakika ni ukafiri kwenu kujitenga na baba zenu.)"[4]

Muslim ameeleza riwaya katika *Sahih* yake, amesema: Abu Musa alitumwa kwa wasomaji wa Qur'ani wa watu wa Basra, waliingia kwake watu mia tatu waliokuwa wamesoma Qur'ani, akasema: "Ninyi ni watu bora wa Basra, na wasomi wake, hivyo basi isomeni wala jambo lisiwe refu kwenu, nyoyo zenu zitakuwa ngumu kama zilivyokuwa ngumu nyoyo za waliokuwa kabla yenu, kwa kweli sisi tulikuwa tunaisoma Sura ambayo tulikuwa tunaifananisha na Surat al-Baraa kwa urefu na ugumu, na nimeisahau isipokuwa tu nimehifadhi katika hiyo:

لو كان لإبن آدم واديان من مال لبتغى واديا ثالثا ولا يملأ جوف ابن آدم إلّا التراب

"Lau mwanadamu angekuwa anamiliki bonde mbili za mali angependa awe na bonde la tatu wala tumbo la mwana wa Adamu halijai ila kwa udongo."

Na tulikuwa tunasoma Sura tuliyokuwa tukiifananisha na mojawapo kati ya sura za *Musabihati,* nimeisahau ila tu nimehifadhi katika hiyo:

يا أيها الذين آمنو لم تقولون ما لا تفعلون فتكتب شهادة في أعناقكم فتسألون عنها يوم القيامة

"Enyi mlioamini! Kwa nini mwasema msiyoyatenda, itaandikwa shahada katika shingo zenu, na mtakuja kuulizwa kwayo siku ya Kiyama."[5]

Nilipokuwa nazitaja riwaya hizi niligundua kuwa Sheikh alipepesa macho yake na alifungua kinywa chake na kulidhihiri hali ya kukanganyikiwa na

4 *Sahih Bukhari*, Juz.8. Uk. 26, Rajmul'hubla mina zina idha ahswanat.

5 *Sahih Muslim*, Juz. 3, Uk. 155, mlango wa Lau mwana adamu……

kuduwaa usoni kwake, niliposimama kusema tu akasema: “Mimi sijasikia hivyo na mimi sijaona hilo, nakuomba ulete vyanzo hivi mbele yangu.

Nilisema: Muda mfupi uliopita ulikuwa unawahujumu Shia na ukiwatuhumu kuwa wanafanya mabadiliko (*tahriif*), kwa nini hukuleta vitabu vyao ambavyo haujaviona maisha yako yote, wewe walazimika kuleta rejea zako na hii ni maktaba yako, kuna *Bukhari*, *Muslim* na vitabu vya Hadith, vilete nikutolee riwaya hizi kutoka humo!

Na alipokosa upenyo alirukia maudhui nyingine, nayo ni: Shia wanasema *Taqiya*, vipi tutasadiki maneno yao?! Alifanya fujo na vurugu mpaka mmoja wao aliposimama kutoa adhana ya Swala ya Isha, na baada ya Swala tuliahidiana tukamilishe mjadala siku zijazo, kwa sharti tuwe tunachagua maudhui tutakayojadili. Na kesho ilipowadia nilikuwa nimeketi mbele ya nyumba yetu asubuhi punde Sheikh alipita na alinisalimia kwa heshima zote na akasema: “Kwa kweli mijadala kama hii hawawezi kuelewa watu wa kawaida, ni bora tuongee na kujadiliana mimi na wewe tukiwa peke yetu.” Nikasema ninaafiki, lakini kwa sharti uache hujuma dhidi ya Shia, baadae hatukumsikia akiwahujumu Shia.

MAZINGATIO KWA MFANYA MJADALA AMBAYO HAPANA BUDI KWAKE

Kabla ya kuanza kusajili baadhi ya tafiti zangu katika kitabu hiki, napenda niashirie baadhi ya mambo ambayo yapasa kuzingatiwa, niliyofaidika nayo kutokana na uzoefu wangu wa hapo mwanzo kuhusu taratibu za mjadala.

1. Kujiamini na kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Na hiyo ndio nukta ya kuanzia katika mjadala. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amempa mwanadam nuru ya akili na elimu, na amejaalia suala la kufaidika navyo mkononi mwa binadamu mwenyewe, kwa hiyo mwenye kuzembea kwa kutofaidika na nuru hii wala asiing’arishe ili kufichua ukweli, ataendelea kuishi kwenye rundo za ujahilia na imani za kuwazika tu na potovu.

Kinyume na anayefaidika na akili yake na kuikuza.

Na tofauti kati ya mawili hayo yarejea kwenye sababu moja, nayo ni kujiamini na kutojiamini. Hivyo basi anayehisi udhaifu na kushindwa hawezi kufaidika na akili yake, ama mwenye kuwa na matumaini na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na kwa alichomtunukia miongoni mwa nuru ya akili, hufikia kilele cha maarifa na maendeleo. Kwa ajili hiyo wengi waliokuwa wanapinga njia yangu katika kufanya utafiti walikuwa wanatumia utaratibu huu ili kuangusha matumaini yangu, alikuwa (mtu) anasema: “Una uwezo gani wewe wa kufanya utafiti wa mambo haya?! Kwa kweli wanavyuoni wetu wakubwa hawakufikia ulipofikia, nini thamani yako mbele ya miamba ya wanavyuoni wenye maarifa makubwa?!” Na yasiyokuwa hayo miongoni mwa njia za kuharibu uwezo. Hawakuwa wananitaka zaidi ya kuwa niwe naingia waingiapo, na nipige kelele kama wapigavyo, amesema (s.w.t.) **“Yatutosha tuliyowakuta nayo baba zetu.” (*Maida*: 104).**

(2) Kujiepusha na hadaa ya utu uliyonayo, kwa maana ya kupuuzuia ukweli usipenye kwenye akili. Hilo laweza kuwa kwa kuzifunga penyo za nafsi chunguzi kuutambua ukweli wa nje. Hivyo (mtu) hujipendelea na hujizuia asisikilize maneno ya maarifa na fikra zingine na kusoma vitabu, na mengine yasiyo kuwa hayo. Hivyo basi kila aina ya wito unaoamrisha kujifungia na kutofanya utafiti na kujipatia maarifa, ni wito unaokusudia kuimarisha ujinga na kuwaweka watu mbali na ukweli. Kwa hakika yafanywayo na uwahabi, kule kujizatiti kwenye ngome ya kutotaka kujua yaliyomo ndani ya vitabu vya Shia na kutokaa na kuketi na yeyote miongoni mwa Shia na kujadiliana naye, ni njia ya mwenye kuhemewa na ni mantiki isiyo salama. Qur’ani tukufu imepinga fikra hii kwa kauli yake (s.w.t.): **“Sema: Leteni dalili yenu kama nyinyi ni wakweli.” (*Baqarah*: 111).**

(3) Kuukuza utashi mbele ya mawimbi ya matamanio na mistari ya mbinyo wa kijamii, ambapo kwa kawaida jamii humchukia kila anayekwenda

kinyume na inavyoona, au kuiasi, kwa hiyo hapana budi kuikabili mibinyo hii kwa subira na azma, kwa kuwa ukweli hauwi kwa kuendeleza hali ya kijamii na yatokanayo na tabia ya mwanadamu. Historia ya manabii wa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ni hiyo, wamekumbana na aina kali mno za adhabu kutoka kwa jamii zao. Waisraeli walikuwa wanawauwa kwa siku manabii sabiini wa Mwenyezi Mungu. Allah (s.w.t.) anasema: **"Na hakuwafikia Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli." (*Sura Zukhruf*: 7).**

(4) Kuna vizuizi vingi vinavyoweza kuzuia kuufichua ukweli, hivyo basi hapana budi kutanabahi na kuangalia ili ukweli uwe wazi zaidi na wenye mwanga zaidi, na miongoni mwa vizuizi hivi ni:

Kujipendelea mtu dhati yake, na huo ni ugonjwa mbaya mno unaomsibu kila mtu, na kutokana nao hupatikana akisi ya kila sifa mbaya mfano wa husuda, hikdi, ukaidi, pindi mtu anapozifanya fikra zake na itikadi yake kuwa sehemu ya dhati yake na utu wake. Japo ziwe potovu hatoweza kukubali zikosolewe imani na fikra zake hizo, kwa kuwa yeye anaamini kuzikosoa ni kuitangua dhati yake na utu wake. Hivyo kwa silika ya mtu kujilinda nafsi yake na kuipenda, anakuwa jasiri kuilinda bila uelewa au ufahamu, na pengine anajijengea upendeleo wa fikra fulani kwa kuwa yamletea manufaa au kumhami dhidi ya madhara, kwa hiyo hujibadilisha rangi na kuihami, kwa minajili hiyo huikataa kila fikra japo ukweli wake uwe dhahiri kwenye macho. Pia anaweza kuipenda fikra si kwa jingine ila tu kwa kuwa yalingana na utashi wa nafsi yake au wa jamii yake, kwa hiyo haepukani nayo.

Kuwapenda wazazi, hilo humfanya mtu kuwafuata bila kufikiri wala kuzingatia, hivyo basi chini ya dai la kuheshimu na kuogopa, ukiongezea kurithi na malezi, mtu husalimu amri mbele ya fikra zao na itikadi zao moja kwa moja. Na hiki ni kizuizi miongoni mwa vizuizi vikubwa mno ambavyo humzuia mtu kuugundua ukweli.

Kuwapenda waliopita. Kwa kweli mtizamo wa utakatifu kuwaelekea wanavyuoni waliopita na watu watukufu kunampelekea mwanadamu kuwafuata moja kwa moja na kuzitegemea fikra zao na itikadi zao. Hivyo basi kusalimu amri mbele ya ufuataji kama huu ni sababu miongoni mwa sababu za kupotoka mbali na ukweli. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) hakuzi-jaalia akili zao kuwa hoja juu yetu, bali akili ya kila mtu ni hoja juu yake, hivyo basi heshima zetu kwao zisituzuie kuhoji na kuzipembua fikra zao, ili tusiingie katika hukumu ya kauli yake (s.w.t.):

﴿ وَقَالُوا۟ رَبَّنَآ إِنَّآ أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَآءَنَا فَأَضَلُّونَا ٱلسَّبِيلَا۠ ﴿٦٧﴾ ﴾

“Na watasema: Mola wetu hakika tumewafuata mabwana wetu na wakubwa wetu, basi wao wametupoteza njia.” (*Sura Ahzab*: 67).

Na pia miongoni mwa sababu za makosa ni kufanya haraka. Na hiyo ni tija ya kupenda raha, hivyo mtu bila ya kujitaabisha binafsi, kutafiti na kuchimbua, hupenda kuharakia kutoa hukumu yake kwenye mtazamo wa kwanza. Kutokana na hali hiyo wanafikra wamekuwa wadogo ulimwenguni kwa sababu ya ugumu wa kufikiri na kutafiti. Hivyo basi, kwa autakaye ukweli hapana budi afanye juhudi mwenyewe katika kuutafiti.

Na yasio hayo miongoni mwa maono ya kielimu ambayo hapana budi mtafiti ayaweke kwenye mkazo wa macho yake kabla hajaanza utafiti. Hii iwe pamwe na kujiepusha na hayo kikamilifu, na kusalimu amri moja kwa moja endapo ukweli utadhihiri. Ukiongezea kuomba auni na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ili aung’arishe moyo wako kwa nuru ya haki: “Ewe Allah, tuonyeshe ukweli kama ulivyo na turuzuku kuufuata, na tuonyeshe batili kama ilivyo na uturuzuku kujiepusha mbali nayo.” (Hadith tukufu.)

MLANGO WA PILI

UPOTOVU UMEFICHUKA

Upotovu ulifichuka:

Kwa kweli Hadithi mbili:

عليكم بسنّتي وسنّة الخلفاء الراشدين من بعدي؛ تمسكوا بها وعضوا عليها بالنواجذ

"Ni juu yenu kuishika Sunna yangu na Sunna ya makhalifa baada yangu. Shikamaneni nazo na ziumeni kwa magego."

إنّي تارك ما إن تمسكتم به لن تضلوا كتاب الله وسنّتي

"Mimi ni mwenye kuacha kile ambacho endapo mtakishika hamtopotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu."

Kwangu mimi zilikuwa ni dalili zenye nguvu mno ambazo nilikuwa nazitolea hoja nilipokuwa naelemea kwenye fikra ya kiwahabi. Na nilipohifadhi hadithi mbili ambazo wanazuoni wao wanazirudiarudia sana katika vitabu na mihadhara, wala siku moja nafsi yangu haikupata kunisemesha nifanye rejea kwenye chimbuko lake la asili katika vitabu vya hadithi. Na nilikuwa nazitendea kazi utendeaji kazi wa hadithi zilizokubalika na zilizo dhahiri. Na hiki sio kitu cha ajabu, kwani hizo kwa kweli ni msingi wa kwanza ambao juu yake fikra ya kisunni hujengeka, na hasa fikra ya kiwahabi ambayo hujengwa na hadithi mbili hizi kwa uthabiti. Akilini mwangu hamkuwa na shaka ya kutosihi kwa hadithi hizo, kwa kuwa ni kituo ambacho natokea humo katika kujihusisha kwangu na madhehebu ya Sunni,

kwani kuzishakia Hadithi mbili hizo maana yake ni kujishakia mwenyewe kuhusu ujihusishaji wangu na madhehebu hayo.

Na fikra hii ambayo kwayo nilihadaika nayo haikuwa baada ya kuhakiki, na wala haikuwa ni matokeo ya zama au matokeo ya fikra ya kisunni, bali ni matokeo ya mpango uliodurusiwa, ulipangwa toka zamani ili kuifunika haki na kuikabili safu ya Ahlul-Bayt, ambayo inawakilisha Uislam kwa sura zake zilizo nzuri mno, na yasikitisha sana kuwa madarasa nyingi za kifikra, zimesimama juu ya mpango ule mbaya, zikajengea fikra zake juu yake kana kwamba wenyewe umeteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.), na wameueneza na kuuhami kwa njia na sababu zote. Na uwahabi si kitu kingine ila ni mfano wa wazi wa kujitoa muhanga kwa mpango huo ambao umeutumbukiza umma wa kiislam kwenye bonde lenye kina kirefu la kugawanyika na kufarikiana na mtawanyiko.

Tutajaribu kufichua kiasi kidogo cha vitimbi vyake katika kila mlango miongoni mwa milango ya kitabu hiki. La muhimu kwetu kuhusiana na mpango huo katika uwanja huu ni Hadithi mbili ambazo zilikuwa ndio hatua ya kwanza ya kuipotosha dini na kubadilisha mwelekeo wa Risala hii (Risala ya Uislam), na kuwaweka waislamu mbali na Hadithi hii ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w):

إنّي تارك فيكم الثقلين ما إن تمسكتم بهما لن تضلوا بعدي أبدا؛ كتاب الله وعترتي أهل بيتي

"Kwa hakika mimi nimeacha katika ninyi ambacho endapo mtashikamana nacho hamtopotea baada yangu kamwe: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu."

Hadithi hii ni *mutawatir*, ambayo imeelezwa na vitabu vya hadithi na rejea zake zimefikia idadi nyingi kwa Sunni na Shia, lakini mkono mdanganyifu na wenye khiyana ulifanya juhudi kuificha mbali na maono na badala yake uliitawanya Hadithi: "Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu." Na Hadithi: "Ni juu yenu kuishika suna yangu…" ambazo udhai-

fu uliomo ndani ya Hadithi hizo utafichuka punde tu.

Nilishtukizwa kwa mara ya kwanza niliposikia Hadithi: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu.” Hofu ilinishika, na nilitamani isingekuwa sahihi, kwa kuwa itabomoa kila nililokuwa nimejijengea katika fikra za kidini, bali itabomoa ngome ya madhehebu ya Sunni. Lakini pepo zimevuma kusiko elekea jahazi. Ilitokea kinyume kabisa nilipoziangalia Hadithi mbili hizi kwenye rejea zake za asili. Nilikuta Hadithi: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu,” ina usahihi na uthibitisho kwa kiwango ambacho mtu yoyote hawezi kuwa na shaka nayo, kinyume na hadithi: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.” ambayo si zaidi ya kuwa ni khabari ya *a’ahadi marfuan* ***au*** *mursala* ikiwa tupu na dhaifu, jambo ambalo lilifanya moyo wangu uvunjike.

Kutokea hapa ilikuwa ndio mwanzo wangu wa kufanya utafiti nilipohisi uchungu wa kushindwa, baada ya hapo muktadha na ishara zikaanza kujikusanya kwangu moja baada ya nyingine mpaka ukweli ulinifichukia kwa sura zake za wazi mno. Na tutathibitisha hapa udhaifu wa hadithi mbili: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.” Na “Ni juu yenu kuishika suna yangu…” Na pia usahihi wa Hadithi ya kizazi ambayo ni risasi ya kwanza ambayo huusibu moyo wa fikra ya kisunni.

Hadithi: “Ni juu yenu kuishika suna yangu…” ni hadaa potovu:

عليكم بسنّتي وسنّة الخلفاء الراشدين المهديين من بعدي؛ تمسكوا بها وعضوا عليها بالنواجذ

“Ni juu yenu kuishika Sunna yangu na Sunna ya makhalifa waongofu wenye kuongoza baada yangu. Shikamaneni nazo na ziumeni kwa magego.”

Mtazamaji wa hadithi hii kwa mtazamo wa kwanza atadhani kuwa ndio hoja yenye kuvunja na ni dalili ya wazi ya wajibu wa kufuata madarasa ya

makhalifa waongofu, nao ni: Abu Bakr Swidiq, Umar bin al-Khattab, Uthman bin Affan, na Ali bin Abi Talib. Hatoweza kuichukulia maana nyingine mbali na maana hii, ila kama kutakuwa na aina fulani ya ta'awili na moyo wa kasumba na kupenda mjadala. Kutokana na hali hiyo ndio zinapatikana nguvu za hadaa na werevu wa wapotoshaji, ndani ya hadithi hiyo wajikita usahihi wa madhehebu ya Ahlu Sunnah katika kuikabili madhehebu ya Shia. Kwa mujibu huo tunaweza kuifasiri hali ya kuibuka madrasa zinazoelekea kinyume na madhhebu ya Ahlul-Bayt, kwa sababu hayo madhehebu yamesimama juu ya msingi wa Hadithi hii na zilizo mfano wake.

Lakini kwa mtizamo wa kielimu na kwa juhudi kidogo ili kuchambua ukweli wa kihistoria, na yaliyofunikwa na hadithi hii na zilizo mfano wake, au kuangalia katika nyanja za elimu ya hadithi na fani za *jarhu* na *taadiil*[6] utadhihiri na kufichuka upotovu wa hadithi hii na ubatili wake.

Ni ujinga kwa Sunni yoyote amtolee hoja Shia kwa hadithi hii, kwa sababu ni Sunni peke yao wanashikamana na hadithi hii, na haitowezekana kuwalazimisha Shia kwa hadithi ambayo hawaielezi ndani ya rejea zao wanazoziamini. Lakini kwa kuwa mimi ni mtafiti wa kisunni hapana budi niwe naanzia katika vitabu na vyanzo vya kisunni, ili iwe lazima kwangu kuzifuata. Na hii ni nukta ya mfumo wa kiutendaji na mazungumzo katika utafiti.

Hapana budi tuangalie katika hoja zetu na mazungumzo yetu kwa sababu hoja haiitwi hoja ila endapo hasimu anashikamana nayo, ili iwe hoja dhidi yake, na hili ndilo ambalo walio wengi katika wanachuoni wa kisunni hawana mwamko nalo, wanapotoa hoja dhidi ya Shia kwa Hadithi hii kuikabili hoja ya Shia, ile ya Hadithi: "Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu."

6 *Jarhu* na *Taadiil* humaanisha hali za wapokezi wa hadithi, yaani kukubaliwa na kutokukubaliwa kwao.

Na tofauti kati ya hoja hizi mbili ni kubwa mno, nayo ni kwamba Hadithi ya 'Suna yangu' ni mahsusi kwa Sunni, kinyume na 'Kizazi changu' ambayo yakubalika na pande zote mbili.

VYANZO VYA HADITHI

Ishkali ya kwanza ambayo huelekezwa kwa Hadithi hii: "Ni juu yenu kuishika Sunna yangu" ni kwamba yenyewe ni miongoni mwa Hadithi walizoziacha masheikh wawili – Bukhari na Muslim – wala hawakuitia katika sahihi zao, na hii yamaanisha Hadithi hii ina dosari haikufikia kiwango cha daraja ya Hadithi sahihi. Hivyo ni kwa sababu Hadithi iliyo sahihi mno ni ile iliyoelezwa na masheikh wawili. Kisha ile aliyoieleza Bukhari peke yake, kisha ile aliyoieleza Muslim peke yake, kisha ile inayotimiza sharti za wawili hawa. Kisha iliyotimiza sharti za Bukhari, kisha iliyotimiza sharti za Muslim. Na sifa hizi teule hazipo katika hadithi hii. Hadithi hii ipo katika *Sunan Abi Daud, Sunan Tirmidhiy* na *Sunan Ibn Majah.*

Kwa kweli walioieleza Hadithi hii wote hawaepukani na udhaifu na kubezwa na wanazuoni wa *Jar'hu wa Taadiil.*[7] Na mwenye kufuatilia wasifu wao ataliona hilo vyema kabisa. Na sina nafasi katika haraka kama hii kuwadodosa waelezaji wa Hadithi hii mmoja baada ya mwingine, kwa njia zake mbalimbali, na kunakili rai za wanavyuoni wa *Jar'hu wa Taadiil*,[8] hivyo nitakomea kuonyesha udhaifu wa mwelezaji mmoja au wawili toka katika kila rejea. Na hiyo inatosha kuidhoofisha riwaya hiyo,

7 *Jarhu* na *Taadiil* humaanisha hali za wapokezi wa hadithi, yaani kukubaliwa na kutokukubaliwa kwao.

8 *Jarhu* na *Taadiil* humaanisha hali za wapokezi wa hadithi, yaani kukubaliwa na kutokukubaliwa kwao.

kama walivyokubaliana wanazuoni wa elimu ya *Jar'hu wa Taadiil* [9] juu ya hilo, kwani pengine muelezaji huyu dhaifu amejitengenezea riwaya hii!

Riwaya ya Tirmidhiy:

Tirmidhiy ameieleza Hadithi hii kutoka kwa: Baghyatu bin Al-Walid, na hizi hapa rai za wanavyuoni wa *Jarhu wa Taadiilu* kumhusu yeye: Ibnu al-Jawziy amesema kumhusu anapozungumzia Hadithi hiyo: "Tulikwishataja kuwa Baghyatu alikuwa anaelezea Hadithi kutoka kwa wasiojulikana na waelezao Hadithi dhaifu, na pengine anaacha kuwataja wao na hata wale waliomuelezea kutoka kwao."[10]

Na Ibn Haban amesema: "Haitolewi hoja kupitia Baghyatu." Na akasema: "Baghyatu ni mwenye kufanya hadaa katika Hadithi. Anaelezea Hadithi kutoka kwa waeleza Hadithi walio dhaifu, na swahiba zake hawazisawazishi hadithi zake na wanawaondoa walio dhaifu miongoni mwao."[11]

Na Abu Is'haaq al-Jawzijaniy amesema: "Mwenyezi Mungu amrehemu Baghyatu, alikuwa hajali aukutapo uzushi kwa ambaye kwake anazichukua Hadithi."[12]

Na yasiyo hayo miongoni mwa maneno ya wanahadithi na wanazuoni wa *Jarhu wa Taadiilu*. Tuliyotaja yanatosha katika mahali hapa.

---

9 *Jarhu* na *Taadiil* humaanisha hali za wapokezi wa hadithi, yaani kukubaliwa na kutokukubaliwa kwao.

10 *Maudhuatu ibn Jauziy*; Jalada 1, Uk.109.

11 *Maudhuatu ibn Jauziy*; Jalada 1, Uk. 151

12 *Khulaswatu Abakatul'anwar* J. 2, Uk. 350.

Sanad ya Hadithi kwa mujibu wa Abu Daud:

Al-Walid bin Muslim: Ameeleza habari kutoka kwa Thaur An-Naswibiy kulingana na usemi wa Ibn Hajar al-Asqalaniy: “Babu yake aliuawa siku aliochomwa mshale pamoja na Muawiyah, kwa hiyo Thaur alikuwa amtajapo Ali (a.s.) husema: “Simpendi mtu aliyemuua babu yangu.”[13]

Ama kumhusu al-Walid, Dhahabi amesema: “Abu Mas’har amesema: al’Walid ni mwenye kufanya hadaa katika Hadithi, na huwenda akahadaa kwa kunukuu toka kwa waongo.”[14]

Na Abdullahi bin Ahmad bin Hanbal amesema: “Baba yangu aliulizwa kuhusu yeye akasema: ‘Alikuwa mtu anayeirusha Hadithi kwa Mtume bila ya kutaja nyororo ya wapokezi.”’[15]

Na mengine yasio hayo, na hiyo yatosha kuidhoofisha riwaya yake.

Sanad ya Hadithi kwa mujibu wa Ibnu Majah:

Imeelezwa kwa njia tatu:

Katika njia ya Hadithi ya kwanza yumo Abdullahi bin Ala’u. Dhahabi amesema kumhusu: “Ibnu Hazmi amesema: ‘Yahya na mwingine wamemdhoofisha’[16] Naye ameieleza habari kutoka kwa Yahya naye ni mtu asiyejulikana kwa mujibu wa Ibnu Qattan.[17]

Ama katika njia ya pili yumo Ismail bin Bashir bin Mansur, alikuwa Qadiriya kama ilivyo katika *Tahdhibut-Tahdhib*.[18]

13 *Khulaswatu Abakatul’anwar* J. 2, Uk. 344.
14 *Mizanul’I’itidal* Juz.2. Uk. 347.
15 *Tahdhiibut-Tahdhiib* Juz. 4 Uk. 154.
16 *Mizanul’I’itidal*, Juz. 2, Uk. 343.
17 *Tahdhibut-Tahdhib*, Jalada 11, Uk. 280.
18 *Tahdhibut-Tahdhibu*, Jalada 1, Uk. 284.

Ama katika njia ya tatu kwa mujibu wa Ibn Majah: Habari amezieleza Abdul Malik bin Swabbahin kutoka kwa Thaur An-Naswibiy, na ilivyo katika *Mizanil-Iitidali* ni kuwa: “Ni mtuhumiwa wa wizi wa Hadithi.”[19]

Achilia mbali kuwa Hadithi hii ni habari ya mpokezi mmoja**,** riwaya zake zote zarejea kwa Swahaba mmoja naye ni Urbadh bin Saariyah. Na habari ya mpokezi mmoja haithibitishi kitu katika kutoa hoja, zaidi ya hapo ni kuwa Urbadh alikuwa miongoni mwa wafuasi wa Muawiyah na ni askari wake.

UKWELI WA KIHISTORIA NA HADITHI: ‘NA SUNNA YANGU’

Ama ukweli wa kihistoria pia unaikanusha Hadithi hii. Historia yasema kuwa Sunna takatifu haikuwa imeandikwa zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), bali kuna Hadithi kwa njia ya Ahlu Sunnah inaonyesha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anakataza kuandika Hadithi, mfano wa kauli yake (s.a.w.w): “Msiandike kitu kutoka kwangu, na aliyeandika kutoka kwangu ambacho si Qur’ani basi naakifute.” Kama ilivyo katika *Sunan Daarmiy*[20] na *Musnad Ahmad.*

Na katika riwaya nyingine ni kuwa wao waliomba idhini kwa Nabii (s.a.w.w) ili waandike, na hakuwapa idhini. Na zisizo hizo miongoni mwa riwaya zinazoonyesha kuzuia kuandika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Yote hayo yalikuwa ndani ya mpango ambao ulitekelezwa ili kuzuia kuenea kwa Hadithi na ziwe zimefichwa ili haki isidhihiri.

19 *Mizanul’I’itidal*, Juz. 2, Uk. 656.

20 Ameipokea Ahmad, Muslim, Daramii, Tirmidhi na Nasaaiy, wameieleza Hadithi hii kutoka kwa Abi Said al-Khidriy.

Hawakusimama hapo, bali Umar alifanya juhudi ya wazi kuifutilia mbali Sunna. Urwa bin Zubayr ametoa riwaya kuwa Umar bin Khattabi alitaka kuziandika Sunna, aliwataka ushauri kwa hilo swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), nao walimshauri aziandike, ikawa Umar anafanya istikhara kwa Mwenyezi Mungu kuhusu hilo mwezi mzima, kisha asubuhi moja aliamka akiwa amemwazimia Mwenyezi Mungu akasema: “Kwa hakika mimi nilitaka kuandika Sunna, na kwa kweli mimi nilikumbuka kaumu walikuwa kabla yenu waliandika maandiko na wakajishughulisha nayo na waliacha kitabu cha Mwenyezi Mungu, na kwa kweli abadan mimi sikifuniki kitabu cha Mwenyezi Mungu na kitu.”[21]

Na kutoka kwa Yahya bin Jaadata kuwa Umar bin Al Khattab alitaka kuandika Sunna halafu ikamjia asiiandike. Halafu aliandika katazo na kupeleka mikoani: “Mwenye kuwa na kitu - miongoni mwa Hadithi - naakifutilie mbali.”[22]

Ibnu Jarir ameeleza kuwa Khalifa Umar bin al-Khattab alikuwa kila amtumapo hakimu au liwali kwenye mkoa au nchi humuusia, katika jumla ya anayomuusia ni: “Itenge mbali Qur’ani, na fanya riwaya kutoka kwa Muhammad ziwe chache na mimi ni mshirika wenu.”[23]

Historia imehifadhi kuwa Khalifa alimwambia Abu Dharr na Abdullah bin Mas’ud na Abu Darda’a kuwa: “Hadithi gani hizi mnazieneza kutoka kwa Muhammad?!”[24]

---

21 Ameipokea Al-Bayhaqiy ndani ya *Al-Madkhali* kutoka kwa Ur’wat, na pia kaipokea Hafidhul-Maghrib bin Abdul-Bari.

22 *Jaamiu-Bayanil-ilmi wa fadhlihi*, Jalada 1, Uk. 64-65. *Tabaqati Ibn Saad* Uk. 3.s

23 *Tarikhut-Tabari* Jalada 3, Uk. 273.

24 *Kanzul Ummal*, Jalada 1, Uk. 293.

Kama ilivyoelezwa kuwa Umar bin al-Khattab alizikusanya Hadithi kutoka kwa watu, wao wakidhania kuwa anataka kuziangalia na kuzisawazisha ili jambo moja lisiwe na tofauti. Walimletea maandiko yao na yeye akayachoma moto, kisha akasema: “Tumaini kama tumaini la Ahlul’kitabi.” Kama alivyoeleza al-Khatib kutoka kwa al-Qasim katika kitabu *Taqyidul-Ilmi*.

Ama sababu alizozisema Umar za kuhalalisha kuiondoa Sunna, ni sababu ambazo hata mjinga hazikubali sembuse mwanachuoni, kwa kuwa ni kinyume na Qur’ani, na roho ya dini na akili, basi vipi aseme: “Itenge mbali Qur’ani, na fanya riwaya kutoka kwa Muhammad ziwe chache..” hali Qur’ani yenyewe yatilia mkazo kuwa hoja yake hutimia kwa Sunna, kwa kuwa Sunna ni muweka wazi na mfafanuzi, na Sunna ndio inayojulisha kuwa hukumu hii ya Qur’ani ni mahsusi na yenye kufungika na yasiyo kuwa hayo, na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema: **“Na tumeuteremsha kwako utajo (Qur’ani) ili uwabainishie watu walichoteremshiwa ili wawe wanafikiri.”**

Hivyo basi ni vipi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ataibainisha Qur’ani kama si kwa Sunna?! Na amesema (s.w.t.):

﴿ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ۝ وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ۝ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْىٌ يُوحَىٰ ۝ ﴾

“Kwamba mtu wenu hakupotea wala hakukosa. Wala hasemi kwa utashi binafsi. Hayakuwa haya ila ni Wahyi uliofunuliwa.” (*Surat Najmi*: 2 – 4).

Basi ni faida gani ya wahyi endapo tutaamrisha ufichwe na uunguzwe. Na hii Sunna muitoleayo hoja kuwa ni lazima kuifuata imepitiwa na mlolongo wa njama, mwendo huu umeanzia kutoka kwa Abu Bakr, yeye ameunguza Hadithi mia tano alizokuwa ameziandika kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) wakati wa zama za ukhalifa wake. Bibi Aisha amesema: “Baba yangu alikusanya Hadithi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w), zilikuwa Hadithi mia

tano, alikesha anajigeuzageuza alipopambazukiwa na asubuhi akasema: ‘Ee binti yangu zilete Hadithi zilizo kwako.’ Nilimletea na aliziunguza na akasema: ‘Nimeogopa nisijekufa nazo zipo kwako, hivyo hadithi kutoka kwa mtu niliyemwamini na nimemshiba zitakuwa kinyume na alivyonihadithia, kwa hiyo nitakuwa nimelibeba hilo.”’[25]

Na Umar aliandika barua akiwa katika enzi ya ukhalifa wake na alizituma sehemu za miji mbalimbali, katika barua hizo aliandika: “Aliyekuwa ameandika Hadithi na aifute.”[26]

Uthman naye alipita njia hiyo hiyo; kwa sababu alichukua ahadi kuwa atakwernda mwendo wa masheikh wawili – Abu Bakr na Umar – akasema akiwa juu ya mimbari: “Si halali kwa yeyote aieleze Hadith ambayo haikusikika katika zama za Abu Bakr wala zama za Umar.”[27]

Baada ya Uthman aliendeleza mwendo huo Muawiyah bin Abi Sufian, akisema: “Ee ninyi watu punguzeni riwaya kutoka kwa Mtume, na ikiwa munahadithia hadithieni zilizokuwa zinahadithiwa zama za Umar.”[28]

Kwa mujibu huo kuacha kuandika Hadithi kunakuwa ni Sunna ya kufuatwa, na kuiandika kukahesabika kuwa ni kitu cha munkari.

Kudhalilishwa na kupotoshwa kama huku kwa njia ya habari kulikokuwa kunafanywa na mamlaka tawala juu ya kuandika hadithi, si kwa jingine ila ni kwa ajili ya kuzificha fadhila za Ahlul-Bayt na kuzuia zisienee. Hii ndio sababu ambayo walio wengi hawaridhiki, lakini ndio ukweli mchungu ambao anagongana nao mfuatiliaji katika historia na aliyeyasoma matukio yake.

---

25 *Tadhkiratul-Hufadh* Jalada 1, Uk. 5.

26 *Musnad Ahmad* Jalada, 3, Uk. 12 -14.

27 *Kanzul Ummal*, Juz.10, Uk. 295, Hadith namba 2949.

28 *Kanzul Ummal*, Juz.1, Uk. 291, Hadith namba 29413.

Baada ya hali hiyo ni Sunna gani ambayo Mtume (s.a.w.w) aliamrisha ifuatwe?! Je ni ile aliyoifutilia mbali Umar? Au aliyoiunguza Abu Bakr?!

Ikiwa kulikuwa na amri ya kuifuata Sunna basi ni kwa nini hawakuitii amri hii hawa makhalifa waongofu, kwa kukithirisha riwaya zake na kutilia hima ya kuziandika?!

Afanyeje atakaye kushikamana na Sunna baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w)?!
Tufanye mfano mtu huyo aliishi na Swahaba, je awe anawatafuta maswahaba wote ili achukue Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kutoka kwao hali kati yao kuna maliwali, mahakimu, viongozi, na askari wakiwa kwenye msitari wa mbele?!

Je awatafute wote ili awaulize hali ya analotaka kulijua miongoni mwa hukumu, au atosheke na kurejea kwa wanaopatikana, na yeye haijuzishi hiyo – Sunnah - kwa tazamio la kutokea *Naasikhu*[29] au *Muqayyadu*[30] au *Mukhaswasu*[31] kwa kule kuhudhuria mmoja au wawili miongoni mwa ambao hawapo Madina? Na hoja kama asemavyo Ibnu Haazim: ‘Haiwi ila kwa wao.’

Na ikiwa tatizo ni kama hili kwa aliyewakuta maswahaba, hali wao ni wachache, basi vipi itakuwa baada ya dola ya kiislamu kupanuka na kukithiri kwa nchi zilizopatikana kwa ushindi, na kukithiri kwa maswali kuhusu matukio na mabadiliko. Nini watajibiwa?

Na pia Hadithi nyingi na hukumu zimepotea, na hili ndilo lililolengwa na njama. Umar alilieleza hilo bayana wakati wa zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), pale aliposema karibu na kifo chake Mtume

29 *Naasikhu:* Iliyofuta hukumu fulani.
30 *Muqayyadu*: Iliyofungika kwa kadhia fulani.
31 *Mukhaswasu*: Iliyofanya hukumu mahsusi kwa kadhia fulani.

aliposema: “Nileteeni karatasi na kidau cha wino niwaandikieni maandishi ambayo kwamba hamtopotea kabisa baada yangu.” Umar akasema: “Kwa kweli yeye anaweweseka, kitabu cha Mwenyezi Mungu kinatutosha.”[32]

Hivyo basi lengo lililozuia karatasi na wino visiletwe kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ili awaandikie maandiko yatakayowazuia wasipotee ni lilelile liliwaziwia wasizikusanye Hadithi na kuziandika. Basi vipi ielezwe baada ya hayo kuwa “Shikamaneni na Sunna zangu?”

Maswahaba hawakushikamana nazo wala makhalifa, bali walitangaza kinyume na hivyo, kama alivyoeleza Dhahabi katika kitabu *Tadhkiratul’hufaadh*, amesema: “Kwa hakika Sidiq (Abu Bakr) aliwakusanya watu baada ya kutawafu Nabii wao, na akasema: ’Kwa kweli ninyi mnahadithia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) Hadithi nyingi, mnatofautiana humo, na watu baada yenu watakuwa wenye kutofautiana sana, hivyo basi msihadithie kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kitu chochote, na atakayewauliza semeni: Kati yetu na ninyi kuna kitabu cha Mwenyezi Mungu, halalisheni halali yake na haramisheni haramu yake.”’[33]

Ni kitu cha kawaida pasiwajibishwe chanzo chochote cha kisheria juu ya umma maadamu haijasajiliwa na kuwekewa mpaka wa ufahamu, au kuwa na mbeba jukumu la kuwa yeye ndiye rejea wa hiyo sheria.[34]

Umma umeafikiana kuwa Sunna haikuwa imesajiliwa zama za Mtume (s.a.w.w) wala zama za makhalifa na haikuwa imesajiliwa ila baada ya karne na nusu tokea kutawafu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.). Hivyo ni kwa sababu zipi aseme msemaji: “Ni juu yenu kuishika Sunna yangu”.

32 *Al-Bukhari*, kitabul’ilmi, Jalada 1, Uk. 30.

33 *Adhuwaau Ala Sunnati Muhammadiyya*, Muhammad Abu Rayyah, Uk. 53.

34 *Usulul’fiqhi*, li Muhammad Taqiyyu al Hakii, Uk. 73.

Hadithi nyingine:

Tamko lake:

تركت فيكم أمرين لن تضلوا ما إن تمسكتم بهما كتاب الله وسنّة نبيّه

“Nimeacha kati yenu mambo mawili ambayo hamtopotea endapo mtashikamana nayo: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Nabii wake.”

Hadithi hii ni dhaifu mno haina haja ya kuijadili, na lolote laweza kusemwa kuhusiana nayo, ukiachilia mbali yaliyotangulia ni kuwa:

a) Kwa hakika Hadithi hii hawakuieleza waandishi wa *Sahih-Sita* za Ahlu Sunna. Na hilo latosha kuifanya iwe dhaifu, basi vipi jamani wameshikamana na Hadithi isiyokuwa katika vitabu vyao Sahihi wala vitabu vyao vya rejea. Na mwangalizi wa nafasi ya Hadithi kwa Ahlu Sunna haimuingii shaka kuwa je, Hadithi hii imeelezwa na vitabu Sahihi, na vilivyo msitari wa mbele ni *Bukhari* na *Muslim*, hali ukweli wa mambo ni kuwa haipo kabisa.

b) Kwa kweli vyanzo vya mwanzo kabisa ambavyo vimeitaja Hadithi hii ni *Muwatau* ya Imam Malik, na *Siira* ya Ibnu Hisham, na *Sawa’iqu* ya Ibnu Hajar. Sikukipata kitabu kingine kilichoeleza Hadithi hii kisichokuwa hivyo. Na vitabu hivi vimeshirikiana katika kunakili Hadithi mbili hizi isipokuwa *Muwatau*.

c) Riwaya ya Hadithi hii ni isiyo na nyororo ya wapokezi (mursalah) katika *Sawa’iqu*, na yenye Sanad iliyo pungufu katika *Siira* ya Ibnu Hisham.[35] Na Ibin Hisham anadai kuwa yeye ameichukua Hadithi hii kutoka katika *Siira* ya Ibnu Is’haqa, na nilitafuta katika Siira ya Ibnu Is’haqa sikuikuta Hadithi

35 *Siirat Ibnu Hisham* chapa ya zamani Juz. 2, Uk. 603. Chapa ya pili Juz. 4, Uk. 185 na chapa ya mwisho ni Juz. 2, Uk. 221.

hii katika chapa zote, basi ni wapi ameitoa Ibnu Hisham jamani?!

d) Ama riwaya ya Malik ya Hadithi hii, ni habari isiyo na nyororo ya wapokezi, haina Sanad. Mpokezi wa *al-Muwatau* amesema: “Amenisimulia kutoka kwa Malik kuwa zilimfikia habari kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema:…….”[36]

Kama uonavyo Hadithi hii haina sanad, haiwezi kutegemewa. Kwa nini Malik amekuwa wa pekee kuieleza Hadithi hii na wala ustadhi wake Abu Hanifa hakuieleza au mwanafunzi wake Shafiiy na Ahmad bin Hanbali? Lau Hadithi ingekuwa sahihi kwa nini maimamu wa madhehebu na maimamu wa Hadithi wameikwepa?!

e) al-Haakim ameiandika Hadithi hii katika *Mustadrak* yake[37] kwa njia mbili: Ya kwaza yumo Zaydu Ad-Daylisiy akinukuu kutoka kwa Ikrimah kutoka kwa Ibnu Abbas. Wala hatuwezi kuikubali Hadithi hii kwa kuwa katika sanad yake kuna huyu Ikrimah muongo,[38] na yeye ni miongoni mwa maadui wa Ahlu-Bayt (a.s.) na ni miongoni mwa ambao walitoka dhidi ya Ali na walimkufurisha.

Ama njia nyingine yenyewe yumo Swaleh bin Musa al-Talhiy akinukuu kutoka kwa Abdul-Azizi bin Rafiiu kutoka kwa Ibnu Swaalih kutoka kwa Abu Hurayra. Na Hadithi hii pia haiwezi kukubaliwa, kwa kuwa Hadithi hii kwa mujibu wa riwaya ya Abu Said al-Khidriy, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliitamka akiwa amelala katika tandiko la ugonjwa

36 *Al-Muwatau* cha Imam Malik aliyefariki 179 A.H. Jalada 2, Uk. 46, amekisahihisha, na kukiweka namba, kuzitoa Hadithi zake na kuzitolea maelezo Muhammad Abdul Baaqiy.

37 *Mustadrak* Jalada 1, Uk. 93, usimamizi wa Dr.Yusuf Abdur Rahman al-Mar’ashiy, chapa ya Darul’maarifa, Beiruth – Lebanon.

38 Yatakujia hivi punde maneno ya wanazuoni wa jarhu na taadiil kuhusu Ikrimah.

aliotawafu nao, na muda huu Abu Hurayra alikuwa Bahrayni, alitumwa pamoja na Al-Alaa Al-Hadhramiy mwaka na nusu kabla hajatawafu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Hivyo ni wakati gani alimsikia Nabii akiwa mgonjwa mahututi juu ya tandiko?!

f) *Sunanul-Kubra* ya al-Bayhaqiy Juz. 1, Uk. 4, chapa ya Darul-Maarifah, Beirut – Lebanon. Imeinakili Hadithi ya Muslim: "Nimewaachieni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu watu wa nyumba yangu." Kisha inazinakili Hadithi mbili za *Mustadrak* kwa tamko.

g) Kitabu *Al-Faqiihul-Mutafaqihu* cha Al-Khatiib Al-Baghdady Jalada la 1. Uk. 94 kilichosahihishwa na kutolewa maelezo na mstahiki Sheikh Ismail Al-Answariy, yeye ni mwanachama wa baraza la fat'wa –Darul-Kutubil-Ilmiyah – Beirut – Lebanon. Amezinakili Hadithi mbili, ya kwaza ni Hadithi ya *Al-Mustadrak*, (kutoka kwa Abu Swalih kutoka kwa Abu Hurayra). Ama ni Hadithi mpya ambayo aliinakili. Alisema: Seifu bin Umar amenihadithia kutoka kwa Abu Is'haqah Al-Asadiy kutoka kwa As-Swabahi bin Muhammad kutoka kwa Abu Haazim, kutoka kwa Abu Said Al-Khudriy…..

Na sanad hii haiwezi kukubaliwa kulingana na ushahidi wa wanavyuoni wa *Jarhu na Taadil* kumhusu Seifu bin Umar, wameafikiana kuwa ni muongo na mzushi, itakujia hivi punde kauli ya wanachuoni kumhusu yeye.

h) Kitabu *Al-Ilmaau ila Maarifati Usuulir-Riwayah Wataqdiisu Sumaai* cha Kadhi Iyadh (479 – 544 A .H.) kilicho hakikiwa na Sayyid Ahmad Swaqiir, chapa ya kwanza, mchapishaji akiwa ni Darur-Rasun-Naaswira – Maktaba ya Al-Atiiqah – Tunis, Uk. 9. Amenukuu tamko la Hadith kutoka katika kitabu *Al-Faqiihul-Mutafaqihu*, ambayo sanad yake kuna Seifu bin Umar.

Mbali na tulivyovitaja hakuna kitabu kilichonakili Hadith: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.” Hivyo basi Hadith hii haijapatikana ila kwa njia tatu: Kutoka kwa Ibnu Abbas, Abu Said al-Khudriy na Abu Huraira. Na njia hizi pamoja na udhaifu wake hazikujitokeza ila katikati ya karne ya tano ya Hijria, yaani baada ya al-Haakim, na hakijakuja kitabu cha zamani kuliko hicho kikitaja njia hizi. Hilo ni la kwanza.

Pili, kwa kweli maswahaba hawa watatu: Abu Huraira, Ibnu Abbas, na Abu Said al-Khudriy, wameieleza Hadith ya “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu.” katika karne ya pili ya Hijriya kama alivyoeleza *Muslim*, je, ni ipi kati ya hizi mbili tuikubali?[39]

Kwa mujibu huo riwaya hii si zaidi ya kuwa ni riwaya miongoni mwa riwaya za mpokezi mmoja, zisizo na nyororo ya wapokezi au zisizo na sanadi.

Na miongoni mwa sababu zinazojulisha kuwa riwaya hii ni ya kuzua, ni kuwa Hadith mfano wa Hadith hii ni ya muhimu mkubwa nayo ni kanuni ambayo umma utatakiwa uende nayo baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kwani “Hamtopotea endapo mtashikamana na viwili hivi: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Nabii wake.” Hivyo yapaswa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) awe ameirudia rudia mahali pengi, na maswahaba waichukue kuieleza na kuihifadhi kama ilivyo katika Hadithi “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu.”

Haiwezekani Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) awe ametufanyia Hadithi hii kuwa chimbuko la kisheria baada yake, kwa kuwa ni Hadith isiyojulikana, haina dalili, achia mbali ile dhana ya chimbuko lake.

39 Hakika amenipa faida sana Samahatu Allamah Sayyid Ali Badriy katika matoleo yake ya Hadith “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.”

MAONGEZI NA MWANAHADITHI WA DAMASCUS, ABDUL-QADIR AL-ARNUTIY

Ilinitokea nilipokuwa naishi Sham, kukutana na Sheikh Abdul Qadir Arnutiy, naye ni katika wanazuoni wa Sham (Syria) naye ana ijaza[40] katika elimu ya Hadith.

Mkutano huu ulifanyika bila ya maandalizi yangu, bali ulikuwa kwa tukio la bahati. Nilikuwa na mmoja wa marafiki zangu wa Sudan jina lake Adil, nilifahamiana naye katika kitongoji cha As-Sayyidatu Zaynab (a.s.), na Mwenyezi Mungu alikuwa ameung'arisha moyo wake kwa nuru ya Ahlil-Bayt (a.s.), na amekuwa mfuasi wao, na alikuwa kijana huyu apambanuka kwa sifa njema, ni haba uweze kuzipata kwa mtu mwingine. Alikuwa mwenye tabia nzuri, mwanadini na mnyenyekevu. Hali duni ya maisha ilimlazimu afanye kazi kwenye shamba mojawapo katika kitongoji kiitwacho *Al'Adiliyah* karibu kilomita tisa Kusini mwa Sayyidat Zaynab (a.s.). Karibu na shamba alilokuwa akifanya kazi kulikuwa na shamba lingine la mtu wa makamu, mwanadini alikuwa akijulikana kwa jina la Abu Sulayman. Huyu jirani alipojua kuwa Msudani afanyaye kazi jirani yake ni Shia, alikuja kwake na kuzungumza naye, akasema:

'Ewe ndugu yangu! Wasudani ni masunni wazuri, wewe huu Ushia unatoka nao wapi?! Je katika familia yako kuna Shia yeyote?'

Adil alijibu: 'Hapana, lakini dini na kukinai havijengeki juu ya kuiiga jamii na familia.'
Akasema: 'Kwa kweli Shia wanadanganya na wanawahadaa watu wa kawaida.'

40 Hati maalumu ya ruhusa ya kunukuu hadithi.

Adil akasema: ‘Mimi sijaliona hilo kwao.’

Akasema: ‘Ndio sisi tunawajua vizuri.’

Adil akasema: ‘Ewe alhaji, je waiamini *Bukhari, Muslim,* na vitabu sahihi vya kisunni?’

Akasema: ‘Ndio. ‘

Adil akasema: ‘Kwa kweli Shia huitolea dalili itikadi yeyote wanayoiamini kutoka vyanzo hivi, sembuse vyanzo vyao.’

Akasema: ‘Kwa kweli wao wanadanganya wanazo *Bukhari* na *Muslim* zilizopotoshwa.’

Adil akasema: ‘Wao hawakunilazimisha mimi kitabu mahsusi, bali waliniomba nitafute kutoka maktaba yoyote katika ulimwengu wa Kiarabu.’

Akasema: ‘Huu ni uwongo, na ni wajibu wangu nikurudishe mara nyingine kwenye Usunni. “Mwenyezi Mungu akimwongoza mtu mmoja kupitia wewe ni bora kwako kuliko vyote vinavyochomozewa Jua.”’
Adil akasema: ‘Sisi ni watafutao haki na mwongozo, tunaelemea ielemeako dalili.’

Akasema: ‘Mimi nitakuletea mwanachuoni mkubwa wa Damascus, ni Allama Abdul-Qadir Arnutiy, ni mwanachuoni mtukufu, msimulizi na muhifadhi wa Hadithi. Shia walijaribu kumrubuni kwa mamilioni ili awe pamoja nao, lakini yeye alikataa.’

Ndugu Adil aliafiki wazo hili, na Abu Sulayman akamwambia: “Ahadi yetu ya kukutana ni siku ya Jumatatu, wewe na Wasudani wote ambao wameathiriwa na fikra za kishia.”

Adil alikuja kwangu, na alinipa habari ya yaliyojiri, na aliniomba niende pamoja naye. Kwa furaha kubwa nilikubali pendekezo hili na niliahidiana

naye tukutane saa sita adhuhuri, siku ya Jumatatu 8 Swafar 1417 A.H.

Siku hiyo ilikuwa ya joto kali, tulikutana kwenye ahadi na tulikwenda kule kondeni tukiwa na Wasudani watatu, na tulipofika ndugu Adil alikuwa mpokezi wetu kwenye konde janibichi inayozungukwa na miti ya matunda mbalimbali ambayo mengi hayapo kwetu Sudan.

Na baada ya hapo tuliendelea na safari kwa jirani yake Sunni, alitupokea kwa hamu kubwa. Na baada ya muda kidogo wa kupunga hewa mahali pale pazungukwapo na majani kibichi kila upande, nilikwenda kuswali Dhuhuri na katika hali ile ya Swala msafara ulikuja ukitanguliwa na gari inayombeba Sheikh Arnutiy. Mahali palikuwa pamejaa watu, na walitoka nje waliokuwa ndani ya gari. Nyuso za swahiba zangu Wasudani zilifunikwa na mshangao kutokana na haiba ya mahali hapo, kwa kuwa walikuwa hawakutazamia kuwa mambo yatakuwa makubwa kwa kiwango hiki. Na baada ya kila mmoja kutuwama nafasi yake, nilichagua mahali karibu na Sheikh.

Na baada ya wote kutambulishana, bwana mwenye konde aliongea na Sheikh akisema: “Hawa ni ndugu zetu kutoka Sudan na wameathirika na fikra ya Kishia huko Sayyidat Zaynab, na kati yao kuna Shia anafanya kazi kwenye konde lililoko jirani yetu.”

Sheikh akasema: “Yuwapi huyu Shia?”

Walimwambia: “Amekwenda kwenye konde lake atarejea baada ya muda tu. “

Akasema: “Basi tungoje, maongezi yaanze baada ya kurejea kwake.”

Mmoja kati ya Wasudani alimwendea na alimleta kwenye kikao, na Sheikh aliitumia nafasi hii kwa kusoma Hadithi nyingi anazozihifadhi kwa moyo, na maudhui yake yalikuwa ubora wa baadhi ya nchi kuliko nyingine na

hasa Syria na Damascus, na maudhui hii ilichukuwa karibu nusu saa, nayo ni maudhui haikuwa na maana. Nilistaajabishwa naye sana vipi haitumii fursa hii, hali watu wote wamemwazima akili zao ili wapate Hadithi itakayowanufaisha katika dini yao na dunia yao, hatimaye akasema: “Kwa kweli dini ya Mwenyezi Mungu haichukuliwi kwa usharifu, Mwenyezi Mungu amejaalia sheria yake kwa watu wote, hivi ni kwa haki gani tuichukue dini yetu kutoka kwa Ahli’bayt?! Hali Mtume wa Mwenyezi Mungu ametuamuru kushikamana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna zake, na hii ni Hadithi sahihi hawezi yeyote kuidhaifisha, na hatuna njia nyingine isiyokuwa njia hii.” Na alipiga kwa kiganja chake mgongoni kwa Adil na kumwambia: “Ewe mwanangu, yasikughuri maneno ya Shia.”

Nilimsimamisha nikisema: “Mstahiki Sheikh, sisi twaitafuta haki, na mambo yametuchanganya na tumekuja ili tufaidike kutoka kwako, hasa tulipotambua kuwa wewe ni mwanachuoni mtukufu, mwanahadithi na muhifadhi wake.”

Akasema: “Ndio.”

Nikasema: “Ni miongoni mwa mambo yaliyo wazi, ambayo haghafiliki nayo isipokuwa kipofu, kuwa waislamu wamegawanyika katika makundi na madhehebu yasio na idadi, na kila kikundi kinajigamba kuwa ndicho cha haki na kingine mbali na chao ni batili. Hivyo vipi nitaipata njia, nami nikiwa nakalifishwa na sheria za Mwenyezi Mungu nitambue ukweli kati ya vikundi hivi vyenye kupingana?! Je Mwenyezi Mungu alitutakia tuwe tumefarakana, au alitaka tuwe mila moja tunamfanyia Mwenyezi Mungu ibada kwa sheria moja?! Na ikiwa ndio, basi ni dhamana gani Mwenyezi Mungu na Mtume wake wametuachia ili umma uhifadhike mbali na upotovu? Kwani yajulikana kuwa tofauti ya kwanza ilitokea kati ya waislam mara tu baada ya kutawafu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) palepale, na sio jaizi kwa majukumu ya Mtume auache umma wake bila ya mwongozo waongokao nao.”

Sheikh akasema: “Dhamana ambayo ameiacha Mtume wa Mwenyezi Mungu ili umma uzuilike mbali na kutofautiana ni kauli yake (s.a.w.w):

إنّي تارك ما إن تمسكتم به لن تضلوا كتاب الله وسنّتي

“Mimi ni mwenye kuacha kile ambacho endapo mtakishika hamtopotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.”

Nilisema: “Kwa kweli ulisema muda mchache uliopita, katika maneno yako huenda ikawa kuna Hadithi haina asili yaani haikutajwa katika vitabu vya Hadithi.”

Akasema: “Ndio.”

Nikamwambia: “Hadithi hii haina asili katika *Sahihi Sita*, vipi waiongelea na wewe ni bingwa katika taaluma ya Hadithi?”

Hapo moto wake ulilipuka, akawa anakoroma akisema: “Unakusudia nini, wataka kuifanya Hadithi hii ni dhaifu?”

Nilishangazwa na njia yake hii, na sababu ya kuchemka kwake, ingawaje mimi sikusema kitu. Nilisema: “Pole pole, swali langu ni moja na lenye mpaka. Je Hadithi hii ipo ndani ya *Sahihi Sita*?”

Akasema: “Sahihi sio sita, na vitabu vya Hadithi ni vingi, na Hadithi hii ipo katika kitabu *Al-Muwatau* cha Imam Malik.”

Nikasema: (nikiwaelekea waliohudhuria): “Vyema, Sheikh amekiri kuwa Hadithi hii haipo katika Sahihi sita, na kuwa ipo katika *Al-Muwatau* ya Malik.

Alinikata kauli (kwa lahaja ya ukali) akisema: “Nini! *Al-Muwatau* sio kitabu cha Hadithi?”

Nikasema: “*Al-Muwatau* ni kitabu cha Hadithi, lakini Hadithi hii: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu” katika *Al-Muwatau* haina nyororo ya wapokezi, haina sanad, hali hadithi za *Al-Muwatau* zote zina sanad (ila hii).

Hapo Sheikh alikoroma baada ya hoja yake kuanguka, akawa ananipiga kwa mkono wake na ananitikisa kushoto kulia: “Wewe unataka kuidhoofisha Hadithi hii, wewe ni nani ufikie kuidhoofisha Hadithi hii?!” Kiasi kwamba alitoka nje ya mipaka ya kiakili. Wote walianza kushangazwa na harakati zake na matendo yake haya.

Nikasema: “Ewe Sheikh! Hapa ni mahali pa mjadala na dalili, na mwenendo huu wa ajabu unaokwenda nao haufai, mimi nimekaa (vikao) na wengi katika wanavyuoni wa Shia, wala sikuona utaratibu kama huu kabisa. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema:

﴿ وَلَوۡ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ ٱلۡقَلۡبِ لَٱنفَضُّواْ مِنۡ حَوۡلِكَۖ ﴾

“Na lau ungekuwa mkavu na mgumu wa moyo wangetawanyika kukukimbia.” (*Sura al-Imran*: 153).

Hapo kidogo ulipoa mhemko wake. Nikasema: “Nakuuliza Sheikh, je riwaya ya Malik katika Hadithi hii “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu” katika *Al-Muwatau*, ni dhaifu au sahihi?!”

Alisema (kwa masikitiko makubwa): “Ni dhaifu.”

Nikamuuliza: “Kwa nini basi, ulisema Hadithi iko katika *Al- Muwatau* nawe wajua kuwa ni dhaifu?”

Akasema (kwa sauti ya juu): “Hadithi hii ina njia zingine.”

Nikasema kwa waliohudhuria: “Sheikh ameachana na riwaya ya *Al-*

Muwatau, na amesema kuwa Hadithi hii ina njia zingine, hebu tuzisikilize njia hizo kutoka kwake."

Hapo Sheikh alihisi kuhemewa na aibu, kwa kuwa Hadithi hii haina njia iliyo sahihi, na wakati huo huo, mmoja kati ya waliohudhuria aliongea, Sheikh alinibonyeza kwa mkono wake, na aliniambia huku akiishiria kwa muongeaji: "Msikilize." Na aligeuka akiwa ataka kulikimbia swali linalosumbua nililomuuliza. Nilihisi hali hii kwake lakini nilisisitiza nikasema: "Tusikilize ewe Sheikh njia zingine za Hadithi hii?"

Akasema (kwa lahaja ya kunyongea): "Sikuzihifadhi, nitakuandikia."

Nikasema: "Subhanallah!, wewe wahifadhi hadithi zote hizi kuhusu ubora wa nchi na vitongoji wala hauhifadhi njia ya Hadithi muhimu mno miongoni mwa Hadithi ambayo ndio ngome ya Ahlu Sunna, na ni Hadithi ambayo yauhifadhi umma huu usipotee, kama ulivyosema!"

Alibaki kimya. Na waliohudhuria walipohisi kuwa ameaibika, mmoja wao aliniambia: "Wamtaka nini Sheikh na amekuahidi kuwa atakuandikia?"

Nikasema: "Mimi nakusogezea njia, kuwa Hadithi hii pia ipo katika Siira ya Ibnu Hisham bila ya sanad."

Sheikh Arnutiy akasema: "Kwa kweli Siira ya Ibnu Hisham, ni kitabu cha siira sio cha Hadithi."

Nikasema: "Kwa hiyo waiona dhaifu riwaya hii?"

Akasema: "Ndio."

Nikasema: "Umenitosheleza mzigo wa kuijadili."
Na niliendelea na maneno yangu nikisema: "Na pia ipo katika kitabu *Ilmau* cha Kadhi Iyyadh, na katika kitabu *Al-Faqiihul-Mutafaqihu* cha al-Khatib

al-Baghdad. Je wazichukua riwaya hizi?”

Akasema: “Hapana.”

Nikasema: “Hivyo basi Hadithi ya “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu” ni dhaifu kwa ushuhuda wa Sheikh. Mbele yetu hapajabaki dhamana ila moja tu itakayouzuia umma usitofautiane, nayo ni Hadithi mfululizo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Na imeelezwa na vitabu vya Hadithi vya kisunni, na *Sahih-Sita* isipokuwa *Bukhari*. Nayo ni kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w):

إنّي تارك فيكم الثقلين ما إن تمسكتم بهما لن تضلوا بعدي كتاب الله حبل ممدود ما بين السماء والأرض، وعترتي أهل بيتي، فإنّ العليم الخبير أنبئني أنّهما لن يفترقا حتى يردا عليّ الحوض

“Kwa hakika mimi ni mwenye kukuachieni katika ninyi viwili vya thamani, endapo mtashikamana navyo hamtopotea baada yangu kamwe: Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni kamba iliyovutwa kati ya mbingu na ardhi, na kizazi changu watu wa nyumba yangu. Kwa kuwa mjuzi mwenye habari, amenipa habari kuwa hivyo havitotengana hadi vitakaponijia kwenye dimbwi.”

Kama ilivyo katika riwaya ya Ahmad bin Hanbal, wala hapana kimbilio lingine mbali na njia hii kwa muumini autakaye Uislamu ambao Mwenyezi Mungu na Mtume wake wameamrisha. Nayo ni njia ya Ahlul-Bayt (a.s) waliotoharishwa mbali na uchafu na maasi katika Qur’ani tukufu.

Na nilitaja jumla ya fadhila za Ahlul-Bayt (a.s.). Sheikh alikuwa amenyamaa hakutoa neno muda wote huu, na si kawaida yake kwani hapo kabla alikuwa akiyakata mazungumzo yangu kati ya neno na neno. Na wapenzi wake walipoona hali ya kushindwa ya Sheikh wao walifanya ghasia na fujo.

Nikasema: “Watosha udajali, unafiki na hadaa dhidi ya ukweli. Mpaka lini kujingikiwa huku?! Ukweli alama zake ziko wazi, ubainifu wake uko dhahiri, na nimesimamisha hoja kwenu, kuwa hapana dini bila ya Kitabu na kizazi kilichotoharika ambacho ni Aali Muhammad (s.a.w.w).”

Sheikh alibaki kimya wala hakunipinga japo neno moja. Alisimama akijipangusa huku akisema: “Mimi nataka kwenda, nina darasa.” Na hali ikiwa yajulikana kuwa alikuwa amealikwa kwenye chakula cha mchana hapa!!.

Mwenyeji alimuomba abakiye, na baada ya kuletwa chakula cha mchana kikao kilitulia. Sheikh hakusema neno lolote katika maudhui nyingine yoyote muda wote wa chakula cha mchana, na hali hapo kabla alikuwa yeye ndiye mwenye kikao na ndiye msemaji namba moja.

Hali ni kama hii kwa kila ambaye anafanya hadaa na kuuficha ukweli, hapana budi afedheheke mbele ya watu.

TATIZO LA MASUNNI HALITANZUKI KWA HADITHI MBILI:

Tukiyafumbia macho yote hayo na tusalimu amri kimjadala, ilimradi tu mjadala uchukue nafasi yake kuwa Hadithi mbili hizi: “Ni juu yenu Sunna yangu” na “Kitabu cha Mwenyezi Munguu na Sunna yangu” ni sahihi, bado hali hiyo haiwaokoi Masunni wala kuondoa taabu yao, bali kwa kila njia na mwelekeo yatilia nguvu na kuyaunga mkono madhehebu ya Ahlul-Bayt (Ushia), hiyo ni kwa sababu zifuatazo:

Hadithi ya kwanza:

عليكم بسنّتي وسنّة الخلفاء الراشدين المهديين من بعدي؛

Ni juu yenu kuishika Sunna yangu na Sunna ya makhalifa waongofu wenye kuongoza baada yangu."

Makhalifa ni wao Maimam wa Kiahlul-Bait:

Kwa kweli neno 'Makhalifa' hapa lina maana ya jenasi sio mahsusi kwa kikundi maalumu. Hivyo basi Sunni kulitafsiri kwa maana ya makhalifa wanne tu ni tafsiri isiyo na asili wala dalili, kwa kuwa kadhia ni kubwa zaidi kuliko madai. Bali dalili za tamko zaonyesha kinyume na madai hayo, kwa sababu makhalifa au makhalifa waongofu ni maimamu kumi na wawili katoka Ahlul-Bayt. Hiyo ni kulingana na dalili zilizothibiti na riwaya thabiti kuwa makhalifa baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ni makhalifa kumi na wawili.

Al-Qunduziy al-Hanafiy katika kitabu *Yanabii'ul-Mawaddah*, amesema: "Yahya bin Hasan amesema katika kitabu *Al-Umdah* kupitia njia ishirini kuwa makhalifa baada ya Nabii (s.a.w.w.) ni makhalifa kumi na wawili, wote ni makuraishi. Ndani ya *Bukhari* ni kwa njia tatu. Na katika *Muslim* ni kwa njia tisa. Na katika *Abu Daudi* ni kwa njia tatu. Na katika *Tirmidhiy* ni kwa njia moja na katika *Al-Hamidiy* ni kwa njia tatu.

"Hivyo katika *Bukhari* imetoka kwa Jabir ameisimulia akiwa ameacha nyororo ya wapokezi: 'Baada yangu watakuwa maamiri kumi na wawili.' Na akasema neno sikulisikia, hivyo nilimuuliza baba yangu: Je amesema nini? Alijibu: 'Wote kutoka kwa makuraishi.'

"Na katika *Sahih Muslim* ni kutoka kwa Aamir bin Saad, amesema: Nilimwandikia Ibnu Samrah: Nipe habari ya kitu ulichosikia kutoka kwa Nabii (s.a.w.w), kwa hiyo aliniandikia: 'Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akisema siku ya Ijumaa jioni, siku ya kupigwa mijeledi

Al-Aslamiy:

لا يزال الدين قائما حتى تقوم الساعة ويكون عليهم إثنا عشر خليفة كلهم من قريش

‘Dini itaendelea imara mpaka kije Kiyama, na wawe juu yao makhalifa kumi na wawili, wote kutoka kwa wakuraishi.’”[41]

Baada ya hivyo haiwezekani mtoa hoja atoe hoja kwa hadithi ya “Na Sunna ya makhalifa...” akiibebesha riwaya hiyo makhalifa wanne, hiyo ni kwa ajili ya kuwepo riwaya mutawatiri ambayo imefikia njia ishirini na zote hizo zikibainisha kuwa makhalifa ni kumi na wawili. Wala hatuwezi kuipata tafsiri ya riwaya hizi kwa ukweli wake wa kivitendo isipokuwa kwa Maimamu wa madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) kumi na wawili.

Kwa hiyo Shia wanakuwa ndiyo kikundi pekee ambacho imepatikana maana ya kivitendo ya Hadithi hizi, kwa sababu ya kumtawaza kwao Imam Ali (a.s.) na baada yake Hasan na Husein, na baada ya Hasan na Husein Maimamu tisa kutoka dhuriya ya Imam Husein, idadi inakuwa baada ya hivyo ni Maimamu kumi na wawili.

Japokuwa neno ‘Kurayshi’ katika riwaya hizi ni jumuishi la wazi lisilo na mipaka, ambalo linaruhusu kuingia Makurayshi wengine ambao si katika Ahlul-Bayt, lakini kwa kuambatanisha na riwaya kadhaa na vielelezo vingine, yaani ishara zingine, inabainika kuwa makusudio ya hizo riwaya ni Ahlul-Bayt. Hivyo ni kwa sababu ya kupatikana riwaya kadhaa zinazosaidiana zikithibitisha uimamu wa Ahlul-Bayt (a.s.). Tutazipitia baadhi yao katika utafiti ujao.

41 *Yanabiiul-Mawaddah* cha al-Qunduziy al-Hanafiy Uk.104 - manshuratu Muasasatil Aalamiy lilmatbuati, Beirut – Lebanon .

Na hapa mwaweza kutosheka na riwaya:

إنّي تارك فيكم ما إن تمسكتم بهما لن تضلوا بعدي، كتاب الله وعترتي أهل بيتي.

“Kwa hakika mimi ni mwenye kukuachieni katika ninyi ambalo endapo mtashikamana nalo hamtopotea baada yangu: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu watu wa nyumba yangu.”[42]

Madam kuimarika kwa dini ni kwa wilaya ya makhalifa kumi na wawili kama zilivyobainisha riwaya hizo zilizotangulia, na wakati huo huo kuna riwaya zinatilia mkazo wa kuambatana na Ahlul-Bayt na Kitabu, kwa hiyo ni dalili bora kuwa makusudio ya ‘Makhalifa kumi na wawili’ ni Maimamu wa Ki-Ahlul-Bayt.

Ama ibara isemayo: ‘Wote kutoka kwa wakuraishi’ si chochote ila ni kubadilisha na kughushi katika Hadithi, imewekwa ili dalili iliyo wazi iwajibishayo kuwafuata Ahlul-Bayt ipotoshwe, kwa kuwa ibara sahihi ni: “Wote ni kutoka kizazi cha Hashim.” Lakini mkono mdanganyifu na wa khiyana ulizifuatilia fadhila za Ahlul-Bayt ukazificha miongoni mwazo kiasi cha uwezo wake, na ukabadilisha ulichoweza kukibadilisha.[43]

Na riwaya hii ni mojawapo ya riwaya zilizokuwa muhanga wa kugeuzwa na kubadilishwa. Lakini Mwenyezi Mungu anakataa mpaka aidhihirishe nuru yake. Al-Qunduziy Al-Hanafiy mwenyewe amenakili ndani ya kitabu *Yanabiul-Mawaddah*: “Na katika mawada ya kumi katika kitabu *Mawadatulqurba* cha Sayyid Ali al-Hamdaniy, Mwenyezi Mungu aitukuze

42 Kwa hakika Ali (a.s.) ni wa kwanza miongoni mwa maimamu kumi na wawili. Linalojadiliwa na kitabu hiki hapa ni nadharia mbili: Je hivi wao ni makhalifa wanne au makhalifa kumi na wawili? Hawa kumi na wawili ni akina nani na wanaungana na nani?

43 Rejea mlango wa wasimulizi wazibadili hadithi

siri yake na atububujishie baraka zake, amenukuu kutoka kwa Abdul Malik kutoka kwa Umayr kutoka kwa Jaabir bin Samrah kuwa amesema: 'Mimi na baba yangu tulikuwa kwa Nabii (s.a.w.w) naye (s.a.w.w.) alikuwa anasema: 'Baada yangu kutakuwa makhalifa kumi na wawili.' Halafu ali-hafifisha sauti yake, na nilimuuliza baba yangu: Alisema nini alipohafi-fisha sauti yake? Akajibu: Wote kutoka kizazi cha Hashim."[44]

Bali Al-Qunduziy ameeleza Hadithi zenye uwazi zaidi kuliko hiyo, ameeleza kutoka kwa Abayah bin Rab'iy kutoka kwa Jabir, amesema: "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): 'Mimi ni bwana wa manabii na Ali ni bwana wa mawasii na hakika ya mawasii wa baada yangu ni kumi na wawili, wa kwanza wao ni Ali na wa mwisho wao ni al-Qaim al-Mahdiy."'[45]

Al-Qunduziy Al-Hanafiy hakupata njia nyingine baada ya kuitaja Hadithi hii, ila ni kukiri na akawa anasema: "Kwa kweli Hadithi zinazojulisha kuwa makhalifa baada yake (s.a.w.w) ni makhalifa kumi na wawili, zimekuwa mashuhuri kwa njia nyingi, kwa hiyo kwa ufafanuzi wa zama na utambulisho wa ulimwengu na mahali, imejulikana kuwa makusudio ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) katika Hadithi hii ya maimamu kumi na wawili, ni kutoka Ahlul-Bayt wake na kizazi chake. Kwa sababu hatuwezi kuibebesha Hadithi hii juu ya wafalme wa kizazi cha Umayyah, kwa sababu ya kuzidi idadi yao kumi na wawili na dhulma yao mbaya, isipokuwa Umar bin Abdul-Azizi.

"Na kwa sababu wao si kizazi cha Hashim, kwa kuwa Nabii (s.a.w.w) alisema: "Wote kutoka kizazi cha Hashim," katika riwaya ya Abdul-Malik kutoka kwa Jabir. Na kitendo cha (s.a.w.w) kuihafifisha sauti yake katika kauli hii, kinaipa uzito riwaya hii, kwa kuwa wao hawaufanyii vyema ukhalifa wa kizazi cha Hashim. Na wala hatuwezi kuibebesha juu ya wafalme wa kizazi cha Abbas kwa sababu ya kuzidi kwao idadi iliyotajwa,

44 Chanzo kilichopita, Uk.104.

45 Chanzo kilichopita, Uk.105.

na kwa kutochunga kwao Aya hii “Sema sikuombeni ujira ila upendo kwa karaba wangu.” Na pia Hadithi ya Kishamia.

“Kwa hiyo hapana budi ibebeshwe Hadithi hii juu ya Maimamu kumi na wawili kutoka Ahlul-Bayt wake na kizazi chake (s.a.w.w), kwa kuwa wao walikuwa wataalamu zaidi kuliko watu wote wa zama zao na watukufu mno na wanadini mno na wacha Mungu mno, na ni wenye nasaba ya juu mno na wabora wa jamii yao, na wenye heshima mno kwa Mwenyezi Mungu. Elimu yao ilikuwa kutoka kwa baba zao na yaungana na ya babu yao (s.a.w.w). Kwa hiyo kuibebesha Hadithi: “Ni juu yenu kuishika Sunna yangu na Sunna ya makhalifa waongofu wenye kuongoza baada yangu,” juu ya Maimamu kutoka Ahlul-Bayt ni karibu mno kuliko kuibebesha juu ya makhalifa wanne, kwa ubainifu uliopatikana kuwa makhalifa baada ya Mtume (s.a.w.w) ni kumi na wawili na ni kutoka kizazi cha Hashim.”

Ahlul-Baiyt ndio njia ya kushikamana na Kitabu na Sunna:

Ama kuhusu hadithi:

إنّي تركت فيكم ما إن تمسكتم به لن تضلوا بعدي أبدا، كتاب الله وسنّتي

“Mimi nimekuachieni kati yenu kile ambacho endapo mtakishika hamtopotea baada yangu kamwe: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.”

Hii haipingani na hadith “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu.” Wala hatukimbilii kwenye maamuzi ya kuwa zinapingana, isipokuwa kama kupingana kumeimarika na kuoanisha kati ya hadithi mbili kumeshindikana, lakini ikiwa yawezekana kuoanisha kati ya hadithi mbili basi hapo hakuna kupingana asilan.

Ibnu Hajar ametutosheleza juhudi ya kutafuta uwezekano wa kuoanisha kati ya mbili hizo, kwa kuwa amesema katika *Swawaiq* yake: “‘Mimi ni mwenye kuacha katika ninyi mambo mawili hamtopotea mkiyafuata. Navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahlul-Bayt wangu, kizazi

changu.’ Tabraniy amezidisha: ‘Kwa hakika mimi nimewaombea hilo kwa Mwenyezi Mungu, hivyo basi msiwatangule mtahiliki, wala msizembee mbali nao mtahiliki, wala msiwaelimishe kwa kuwa wao ni wajuzi mno kuliko ninyi.’ Na katika riwaya nyingine: ‘Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu.’ nayo ndiyo iliyokusudiwa katika hadithi zinazoishia na kitabu peke yake, kwa sababu Sunna hukifafanua, kwa hiyo kukitaja (Kitabu) kumetosheleza haja ya kuitaja (Sunna). Matokeo yake ni kuwa, mkazo umekuja katika kushikamana na Kitabu na Sunna na kushikamana na wanavyuoni wa Kitabu na Sunna miongoni mwa Ahlul-Bayt. Tija ipatikanayo kwa jumla ya hayo yote ni kubakia kwa mambo matatu mpaka Kiyama kitakaposimama….”[46]

Na kwa ibara ya kina zaidi kuliko aliyoisema Ibnu Hajar ni kuwa: Hakika amri ya kushikamana na Sunna haiwezi kutekelezeka ila kupitia wahifadhi wake, nao ni Ahlul-Bayt, na Ahlul-Bayt ni wajuzi mno wa yaliyo ndanimwe, kama ambavyo riwaya imelithibitisha hilo na historia imelitolea ushahidi. Hivyo basi himizo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) limekita kwenye kushikamana na Kitabu na Ahlul-Bayt, hivyo basi kushikamana na Sunna huwa ni jambo la kawaida linalazimiana na kushikamana na Ahlul-Bayt, wala si kama alivyosema Ibnu Hajar kuwa: “Himizo limekita juu ya kushikamana na Sunna.” Kwa kuwa riwaya zilizokuja za ulazima wa kushikamana na kizazi ambao ni Ahlul-Bayt zimefikia kiwango cha tawatur.

Ukiongeza juu ya hilo ni kuwa umekwishajua yaliyojiri kuihusu Sunna, ikiwemo kuunguzwa, kuificha na kuipotosha. Kwa hiyo Ahlul-Bayt ni njia pekee ya kuijua Qur’ani na Sunna, kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): “Wala msiwatangulie mtahiliki, wala msizembee mbali nao mtahiliki, wala msiwaelimishe kwa kuwa wao ni wajuzi mno kuliko ninyi.” Kama alivyoiandika Hadithi hii Tabaraniy, hivyo inakuwa hakuna upenyo baada ya hayo, wa kuukwepa wajibu wa kushikamana na Ahlul-Bayt.

[46] *Al- Swawaiqul-Muhrriqah.* Uk. 150.

MLANGO WA TATU

HADITHI: “KITABU CHA MWENYEZI MUNGU NA KIZAZI CHANGU” KATIKA REJEA ZA KISUNNI

Kuthibitisha hadithi: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu”:

Imekuwia wazi katika uchambuzi uliotangulia, ule udhaifu wa hadithi ya kushikamana na Sunna, ambayo yazingatiwa kuwa ni nguzo ya msingi ya kusimama jengo la Usunni, na kutikisika kwa msingi huu latikisika jengo lote la Usunni. Na hii ndio tafsiri ya ile pupa ya wanachuoni wao ya kuificha riwaya ya: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu,” kiasi kwamba imefunika mawazo ya watu walio wengi kufikia daraja mimi niitajapo Hadiithi ya kizazi kwenye kikundi chochote kile, hali ya kuduwaa hujichora kwenye nyuso zao.

Kwa ajili hiyo ili hoja itimie nilipenda kuthibitisha ‘Hadithi ya kizazi’ katika mlango huu kutoka katika vitabu vya Ahlu Sunna, kwa njia zake zote, na ufuatao ni ufafanuzi wake:

Kwanza: Sanad ya Hadith:

Idadi ya wapokezi katika maswahaba:

Kwa kweli Hadithi hii imekuja mfululizo (***mutawatir***) kutoka kundi la maswahaba, na yafuatayo ni baadhi ya majina yao:

1. Zayd bin Arqam
2. Abu Said al Khudry
3. Jabir bin Abdullah
4. Hudhayfa bin Asid
5. Khuzaymah bin Thabit
6. Zayd bin Thabit
7. Suhayl bin Saad
8. Dhumiratul al-Asadiy
9. Amiru bin Abi Layla (al-Ghafariy)
10 Abdur Rahman bin Aufi
11.Abdullah bin Abbas
12. Abdullah bin Umar
13. Uddiy bin Hatim
14. Uqba bin Amir
15. Ali bin Abi Talib
16. Abu Dharr alGhafariy
17. Abu Raafi'i
18. Abu Shariih al-Khuzaiy
19. Abu Qudama al Ansariy
20. Abu Huraira
21. Abul Haythami bin Tihani
22. Umu Salmah
23. Umu Hani'i bint Abi Talib
24. Warjalu min Quraysh

Idadi ya wapokezi katika Tabiina:

Na kunakili huku kumekuwa mfululizo pia katika zama za Tabiina na wafuatao ni baadhi ya walionakili hadithi: "Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu":

1. Abu Tufail Aamir bin Wathilah
2. Atyatu bin Said al Aufiy
3. Hunshu bin Al-Muutamar

4. Al-Harithu Al-Hamdaniy
5. Hubaybu bin Abi Thabit
6. Ali bin Rabiiah
6. Al-Qasim bin Hasan
8. Huswinu bin Sibra
9. Amru bin Muslim
10. Abu Dhwahiy Muslim bin Swabiih
11. Yahya bin Juudah
12. Al-Asbagh bin Nabata
13. Abdullah bin Abi Rafi'i
14. Al-Muttalib bin Abdillah bin Hantab
15. Abdur Rahman bin Abi Said
16. Umar bin Ali bin Abu Talib
17. Fatumah bint Ali bin Abu Talib
18. Al-Hasan bin Al-Hasan bin Ali bin Abi Talib
19. Zaynul-Abidiin Ali bin Al-Husein ..... na wengineo

Idadi ya wapokezi katika karne kadhaa:

Ama kuhusu walioieleza baada ya Swahaba na Tabiina miongoni mwa walio mashuhuri katika umma huu, na mahafidhu wa Hadithi na walio mashuhuri miongoni mwa maimamu, karne na karne ni kundi kubwa, nafasi haituruhusu kutaja majina yao na riwaya zao. Na baadhi ya watafiti na wanavyuoni wameorodhesha idadi yao, hivyo ukitaka kupata ufafanuzi zaidi rejea kitabu *Abaqatul-An'war*, juzuu ya kwanza na ya pili.

Natosheka na kutaja idadi yao katika kila tabaka la wakati fulani, kutokea karne ya pili mpaka karne ya kumi na nne:

Karne ya pili: Idadi ya wapokezi ni 36
Karne ya tatu: Idadi ya wapokezi ni 69
Karne ya tatu: Idadi ya wapokezi ni 69
Karne ya nne: Idadi ya wapokezi ni 38

Karne ya tano: Idadi ya wapokezi ni 21
Karne ya sita: Idadi ya wapokezi ni 27
Karne ya saba:Idadi ya wapokezi ni 21
Karne ya nane: Idadi ya wapokezi ni 24
Karne ya tisa: Idadi ya wapokezi ni 13
Karne ya kumi: Idadi ya wapokezi ni 20
Karne ya kumi na moja: Idadi ya wapokezi ni 11
Karne ya kumi na mbili: Idadi ya wapokezi ni 18
Karne ya kumi na moja: Idadi ya wapokezi ni 11
Karne ya kumi nambili: Idadi ya wapokezi ni 18
Karne ya kumi na tatu: Idadi ya wapokezi ni 12
Karne ya kumi na nne: Idadi ya wapokezi ni 13

Kwa hiyo inakuwa jumla ya wapokezi wa hadithi katika karne ya tatu mpaka karne ya kumi na nne ni 323.

Hadithi ya 'Kitabu na Kizazi' ndani ya vitabu vya Hadithi:

Ama kuhusu vitabu vilivyoeleza Hadithi hii ni vingi, tunataja miongoni mwavyo:
***Sahih Muslim*:** Juz. 4 Uk. 123, chapa ya Darul-Maarif, Beirut, Lebanon. Muslim ameeleza ndani ya Sahih yake kuwa: "Ametusimulia Muhammad bin Bakar bin al-Tiryan: Ametusimulia Hasan (yaani Ibnu Ibrahim), kutoka kwa Said (na yeye ni Ibnu Masruq), kutoka kwa Yazid bin Hayyan, kutoka kwa Zayd bin Arqam. Alisema: Tuliingia kwake na tulimwambia: 'Kwa kweli umeyaona mengi na ulikwa swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) na uliswali nyuma yake. Ewe Zayd kwa kweli umekutana na mengi mengi. Tusimulie ewe Zayd uliyoyasikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w).'

"Alisema: 'Ewe mwana wa ndugu yangu! Wallahi umri wangu umekuwa mkubwa na ahadi yangu imewadia na nimesahau baadhi niliyokuwa nayaelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), hivyo basi

nitakayowasimulia yakubalini na ambayo nitashindwa msinikalifishe nayo.'

"Halafu akasema: 'Alisimama Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kati yetu akitoa hotuba mahali kwenye maji paitwapo Khum, kati ya Makka na Madina, alimhimidi Allah (s.w.t.) na kumsifu, aliwaidhi na kukumbusha hatimaye akasema: 'Ama baad, enyi watu! Kwa kweli mimi ni mtu yakaribia mjumbe wa Mola wangu akaja na nitamjibu. Na mimi nimeacha kwenu vizito viwili, cha kwanza ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mwenye enzi na utukufu, nayo ni kamba ya Mwenyezi Mungu mwenye kuifuata atakuwa katika uongofu na mwenye kuiacha atakuwa katika upotovu.' Hatimaye akasema: 'Na Ahlul-Bayt wangu, ninakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuwahusu Ahlul-Bayt wangu. Nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuwahusu Ahlul-Bayt wangu. Nakukumbusheni Mwenyezi Mungu kuwahusu Ahlul-Bayt wangu.''

"Tuliuliza: Ahlul-Bayt wake ni wakeze? Akasema: 'Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwa kweli mwanamke huwa pamoja na mwanaume muda katika zama, kisha humtaliki naye hurejea kwa baba yake na watu wa kaumu yake. Ahlul-Bayt wake ni asili yake na nasaba yake. wale walioharamishi-wa swadaka baada yake."'

Pia Muslim ameieleza kutoka kwa Zahir bin Harbi na Shujai bin Mukhalid, wote kutoka kwa Ibnu Ulyata. Zahiru akasema: "Ametusimulia Isma'ili bin Ibrahim: Amenisimulia Abu Hayyan: Amenisimulia Yazid bin Hayyan akasema: Alisema: Nilitoka….." Hatimaye aliieleza Hadithi.

Na Muslim aliieleza kutoka kwa Abu Bakr bin Abi Shayba: Ametusimulia Muhammad bin Fudhwail na alitusimulia Is'haqa bin Ibrahim: Ametupa habari Jarir wote wawili kutoka kwa Abu Hayyan kuwa…..... Kisha akaitaja Hadithi.

Na riwaya zote za Muslim zarejea kwa Abu Hayyan bin Said Tamimiy, na Dhahabi alikwishasema kumuhusu: “Yahya bin Said bin Hayyan Abu Hayyan Tamimiy. Thauriy alikuwa anamtukuza na kusema kuwa yu mwaminifu. Ahmad bin Abdullahi Al-Ujaliy amesema: Ni mwaminifu, mwema, mwenye kujitokeza mshika Sunna.”[47]

Na Dhahabi pia amesema katika *Al-Ibar*, Juz.1, Uk. 205: “Na humo mna Yahya bin Said Tamimiy, ni huria wa Taymu Rubab al-Kufiy, na alikuwa mwaminifu imam mshika Sunna. Shaabiy na aliye mfano wake wameeleza hadithi kutoka kwake.”

Na Al-Yafii amesema: “Ndani yake kuna Yahya bin Said Tamimiy Al-Kufiy, alikuwa mwaminifu na imam mshika Sunna.”[48]

Na Asqalaniy amesema: “Abu Hayyan Tamimiy Al-Kufiy ni mwaminifu mchapa ibada….amekufa mwaka wa arobaini na tano.”[49]

Na wengine miongoni mwa wanavyuoni wa *jarhu na taadiil*. Kama ambavyo ni wazi kuwa Hadithi ikiwa imeelezwa katika *Sahih Muslim* ni mwamuzi tosha wa kusihi kwake, kwa ijmai ya waislam (masunni) inayozizingatia riwaya zake zote kuwa ni sahihi.

Na Muslim mwenyewe amebainisha kuwa zote zilizomo katika Sahihi yake kuna ijmai ya kusihi kwake, achia mbali ule usahihi wake kwa mtizamo wake (Muslim), kama alivyosema Al-Hafidh Suyutiy: “Muslim amesema: ‘Sio kila kitu sahihi kwa mtizamo wangu tu ndio nimeweka humu, bali nimeweka humu kile kilichokuwa na ijmai ya usahihi wake.”’ Kama ilivyo katika *Tadribur-Rawiy*.

47 *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 2, Uk.348.

48 *Mir’atul-Janan* Jalada.1, Uk. 301.

49 *Taqriibut-Tahdhiib* Juz. 2, Uk. 348.

Na amesema Nawawiy katika kitabu wasifu wa Muslim: “Muslim ametunga vitabu vingi katika elimu ya hadiith, miongoni mwavyo ni kitabu hiki *Sahih Muslim* ambacho Mwenyezi Mungu Mtukufu kwacho amewafanyia hisani waislam, na imfike yeye shukrani, neema, fadhila na ihsani.”[50]

Na wengine…nafasi haitoshi kutoa maelezo yao, na kwa sababu ya uwazi wa madai haya.

Al-Mustadrak: Riwaya ya hadithi kwa Imam Al-Hafidh Abu Abdillahi Al-Haakim Nisaburiy katika *Mustadrak* yake ya *Bukhari* na *Muslim*, Jalada 3, Uk. 27, kitabu maarifatus-Swahaba, chapa ya Darul-Maarifa, Beirut – Lebanon.

Abu Awanati ameieleza Hadith kutoka kwa Aamash: Ametusimulia Habib bin Abi Thabit kutoka kwa Abi Tufaili kutoka kwa Zaydu bin Arqam, amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alipokuwa anarudi kutoka Hijja ya kuaga, na alisimama Ghadir Khum, alitoa amri ya kutengenezwa minbari ya dharura kwa seti za wanyama, nazo zilisimamishwa, akasema: ‘Kana kwamba nimekwishaitwa na nimeitika. Kwa hakika mimi ni mwenye kuwaachieni vizito viwili, kimoja ni kikubwa zaidi kuliko kingine, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, basi angalieni jinsi mtakavyonifuata kuhusu viwili hivi, kwa kuwa hivyo havitotengana mpaka vitakaponijia kwenye hodhi.’ Hatimaye akasema: ‘Kwa hakika Allah mwenye nguvu na utukufu ni walii wangu na mimi ni walii wa kila muumini.’ Kisha akaushika mkono wa Ali na akasema: ‘Ambaye mimi ni walii wake basi huyu ni walii wake.’ Kwa hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anasisitiza kuwa wa kwanza na ni mkuu katika Ahlul-Bayt wake ambaye amewajibisha afuatwe ni Ali (a.s.).”

50 *Tahdhibul-Asmai Wal-Lughati* Juz. 2, Uk.91.

Kama alivyoeleza pia kutoka kwa Hisan bin Ibrahim Al-Kirmaniy. Ametusimulia Muhammad bin Salma bin Kahiil kutoka kwa baba yake kutoka kwa Abu Tufail kutoka kwa Ibnu Wathilah kuwa yeye alimsikia Zayd bin Arqam akisema:…….

Aliisimulia hadithi kwa mfano uliopita isipokuwa yeye amezidisha: “Mnajua kuwa mimi ni bora kwa waumini kuliko nafsi zao?” mara tatu. Wakasema: “Ndio.” Akasema: “Ambaye mimi ni walii wake Ali ni walii wake.”

Pia Al-Hakim ameieleza kwa njia mbili zingine, lakini kwa ajili ya kuchunga kutorefusha tumetosheka kwa kuzithibitisha njia mbili.

Na ambalo lajulisha usahihi wa Hadithi hii na kuwa ni katika hadithi mutawatir ni kwa sababu Al-Hakim ameieleza na ameihukumu kuwa ni sahihi kwa sharti ya Bukhari na Muslim.

Musnad Ahmad: Riwaya ya Hadithi kwa mujibu wa Ahmad bin Hanbal: Juz. 3, Uk.17 – 26- 14- 59 – chapa ya Daru Swadir Beirut, Lebanon.

“Ametusimulia Abdullahi: Amenisimulia baba yangu: Ametusimulia Abu Nadhar: Ametusimulia Muhammad, yaani Ibnu Abu Talha, kutoka kwa Al-Aamash kutoka kwa Atiyyah Al-Aufiy, kutoka kwa Abu Said Al-Khudriy, kutoka kwa Nabii (s.a.w.w) amesema: ‘Kwa hakika mimi imekaribia nitaitwa na nitaitika na mimi ni mwenye kuacha kwenu vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ni kamba iliyovutwa toka mbinguni mpaka ardhini, na kizazi changu Ahlul-Bayt wangu, kwa hakika Mwenyezi Mungu ambaye ni Latifu mwenye habari amenipa habari kuwa wao hawatotengana hadi waje kwangu bwawani, hivyo basi angaliyeni jinsi mtakavyonifuata katika viwili hivi!”’

Pia ameeleza: “Ametusimulia Abdullah: Baba yangu alinisimulia: Ametusimulia Ibnu Numayri: Ametusimulia Abdul Malik, yaani Ibnu Abu

Sulayman kutoka kwa Atiyyah, kutoka kwa Abu Said Al-Khudriy, akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: 'Kwa hakika mimi nimeacha katika ninyi vizito viwili kimoja ni kikubwa zaidi kuliko kingine, Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mwenye enzi na utukufu, ni kamba iliyovutwa kutoka mbinguni hadi ardhini. Na kizazi changu Ahlul-Bayt wangu, kwa kweli hawatofarikiana hadi watanijia kwenye bwawa."'

Na ameieleza kwa njia nyingi ambazo sio hizi zilizotangulia.

Sahih Tirmidhiy: Riwaya ya Hadithi kwa mujibu wa Tirmidhiy Juz. 5 Uk. 663 – 662 – chapa ya Daru Ihyau Turathul Arabiy.

"Na ametusimulia Ali bin al-Mundhir al-Kuufiy: Ametusimulia Muhammad bin Fudhwaili, amesema: Ametusimulia al-Aamash kutoka kwa Atiyyah na Abu Said, na pia al-Aamash amesimulia kutoka kwa Habib bin Abu Thabit kutoka kwa Zayd bin Arqam, wamesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): 'Kwa hakika mimi nimeacha katika ninyi vizito viwili, kimoja ni kizito zaidi kuliko kingine, Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kamba iliyovutwa kutoka mbinguni hadi ardhini. Na kizazi changu Ahlul-Bayt wangu, kwa kweli havitofarikiana hadi vitakaponijia kwenye bwawa, basi angalieni ni jinsi gani mtakavyobaki navyo baada yangu."'

Ametusimulia Nasru bin Abdur Rahman al-Kuufiy: Ametusimulia Zayd bin al-Hasan, naye ni al-Anmaatiy kutoka kwa Jafar bin Muhammad kutoka kwa baba yake kutoka kwa Jabir bin Abdillahi akasema: "Nilimwona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) katika Hijja yake siku ya Arafa akiwa juu ya ngamia wake akihutubu, hivyo nilimsikia akisema: 'Oh ninyi watu!! Kwa hakika mimi nimeacha katika ninyi ambacho lau mtashikamana nacho hamtapotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Ahlul-Bayt wangu."'

Kanzul-Ummal: Kama alivyoiandika Hadithi hii al-Allama Alaudin Ali al-Mutaqiy bin Hasamud-Din al-Hindiy, aliyefariki mwaka 975 katika kitabu *Kanzul-Ummal Fii Sunanil-Aq'wali Wal-Af'ali*, Jalada ya kwanza, mlango wa pili – Katika kichwa cha habari kinachozungumzia: Kushikamana na Kitabu na Sunna – Uk. 172. chapa ya Muasasatu risala – Beirut, chapa ya 5, Mwaka 1985 – nayo ni hadithi namba 810 na 871 na 872 na 873.

Lau tukifuatilia katika mlango huu hali tukitaka kuvileta vitabu ambavyo vimeielezea Hadithi hii, nafasi ingekuwa ndefu na kingehitajika kitabu cha peke yake. Na hapa tutawataja baadhi ya wanahadithi na wanachuoni ambao walioiandika Hadithi hii, ni mfano tu sio kuwataja wote. Na kwa maelezo zaidi rejea kitabu: *Ihqaqul-Hhaqi* cha Asadullahi Tastariy, Juz. 9, Uk. 311.

Na miongoni mwa ulamaa na wanahadithi hao ni:
Hafidh Tabraniy aliyefariki mwaka 340. Angalia katika kitabu *Muujamus-Swaghiir*.
Allamah Muhibbu Din Tabariy. Angalia katika kitabu *Dhakhairul-Uqba*.
Allamah Sheikh Ibrahim bin Muhammad bin Abi Bakr al-Hamuweyniy. Angalia katika kitabu *Faraidus-Samtain*.
Miongoni mwao ni Ibnu Saad. Angalia katika kitabu *Tabaqatul-Kubra*.
Hafidh Nuru-Din al-Haythamiy. Angalia katika kitabu *Majmauz-Zawaidi*.
Hafidh Suyutiy. Angalia katika kitabu *Ihyaul-Mayit*.
Hafidh Asqalaniy. Angalia katika kitabu *al-mawahibu alladuniyyah.*
Allamah Nabhaniy. Angalia katika kitabu *Anuwaru Muhammadiyah*.
Allamah Daramiy. Angalia katika *Sunan* yake.
Hafidh Abu Bakr Ahmad bin al-Husein bin Ali al-Bayhakiy. Angalia katika kitabu *Sunanul-Kubra*.
Allamah al-Baghawiy. Angalia katika kitabu *Maswabiihus-Sunnah*.
Hafidh Abul Fidai bin Kathiyr al-Damishqiy. Angalia katika kitabu *Tafsirul-Qur'ani*.
Ibnu Athir. Angalia katika kitabu *Jaamiul-Usuul*.
Al Muhadithu al-Shahir Ahmad bin Hajar al-Haythamiy al-Makkiy,

aliyefariki mwaka 914 A.H. Angalia katika kitabu *Swawaiqul-Muhriqah Fii Radi Ala Ahlil-Bidai Wa Zindiqah*, chapa ya pili mwaka 1965, chapa ya Maktabatul Qahirah – Shirkatu Taba'a Al-Faniyyah ASl-Mutahidah.

Na baada ya kuileta Hadithi ya Vizito Viwili akasema: "Halafu jua kuwa Hadithi ya kushikamana ina njia nyingi, imeletwa na maswahaba ishirini na kitu, na ina njia za utata kumi na moja zilizotatuliwa, na katika baadhi ya njia hizo ni kuwa aliitamka hiyo akiwa Arafa katika hija ya kuaga. Na katika nyingine ni kuwa aliitamka hiyo katika Ghadir khum. Na katika nyingine ni kuwa yeye alisema hayo alipokuwa amesimama akitoa hotuba mara tu alipotoka Taifu kama ilivyotangulia. Habari hizo hazipingani kwa kuwa yawezekana kuwa yeye (s.a.w.w) alikariri usemi huo kwao katika sehemu hizo na zingine, kwa sababu ya umuhimu wa suala la Kitabu na Kizazi kitakatifu.

"Na katika riwaya kutoka kwa Tabaraniy kutoka kwa Ibnu Umar ni kuwa, la mwisho alilosema Nabii (s.a.w.w) ni: "Nifuateni katika Ahlul-Bayt wangu." Na katika nyingine kutoka kwa Tabaraniy na Abu Sheikh ni: "Allah Mtukuka ana heshima tatu mwenye kuzihifadhi Mwenyezi Mungu ataihifadhi dini yake na dunia yake, na asiyezihifadhi Mwenyezi Mungu hatoihifadhi dini yake wala akhera yake." Nikauliza ni nini hizo? Akasema: "Heshima ya uislamu, heshima yangu na heshima ya kizazi changu."

"Na katika riwaya ya Bukhari kutoka kwa al-Swadiqu kuhusu kauli yake: 'Enyi watu!! Hivi Muhammad anawapenda watu wa nyumba yake!!?' yaani muhifadhini kupitia wao, musiwaudhi.

"Na Ibnu Saad na al-Malau katika kitabu chake cha Syra amesema kuwa: "Yeye (s.a.w.w) akasema: 'Nausia kheri kwa Ahlul-Bayt wangu, kwa hakika mimi nitakuwa hasimu wenu kwa niaba yao kesho, na ambaye nitakuwa hasimu wake nitamgomba na nitakayegombana naye ataingia motoni."'

“Na kuwa yeye alisema: “Mwenye kunihifadhi mimi katika Ahlul-Bayti wangu amechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu.”

“Na ameandika pia: “Mimi na Ahlul-Bayt wangu ni mti upo ndani ya Jannah na matawi yake yapo duniani, mwenye kutaka na aichukue njia kuelekea kwa Mola wake.”

“Pili ni Hadithi: “Katika kila wanaorithishwa katika umma wangu kuna waadilifu miongoni mwa Ahlul-Bayt wangu, wananiondolea dini hii upotoshaji wa wapotevu na madai ya wabatilifu na tafsiri ya majahili. Tambueni kwa hakika Maimamu wenu ni msafara wenu uelekeao kwa Allah Mtukuka, hivyo basi angalieni mtakayefuatana naye.”

Halafu akasema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliiita Qur’ani na watu wa famili yake kuwa ni ‘Vizito Viwili’, nao ni utukuzo wa hali ya juu wa ahali na kizazi na jamaa wa ukoo wa karibu. Kwa kuwa kizito ni kila kilicho na thamani na hatari chenye kuhifadhiwa, na hawa wawili ni hivyo hivyo – Qur’ani na Ahlul-Bayt – kwa kuwa kila kimoja chao ni mahali pa elimu ya dini, siri na hekima ya juu na hukumu za kisheria. Kwa minajili hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alihimiza kuwafuata na kushikamana nao na kujielimisha kwao wao na amesema: ‘Alhamdu lillahi ambaye amejaalia hekima katika sisi Ahlul-Bayt.’

“Na kuna kauli isemayo: Wameitwa Vizito Viwili kwa sababu ya uzito wa wajibu wa kuchunga haki zao. Halafu ambao himizo limetuka juu yao ni wenye kukitambua Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake, kwa kuwa wao ndio ambao hawatofarikiana na Kitabu mpaka walifike bwawani. Na wanaungwa mkono na habari iliyotangulia, nayo ni “Wala msiwaelimishe kwa kuwa wao wana elimu zaidi yenu.” Kwa hilo wamepambanuka mbali na wanavyuoni wengine, hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwaondolea uchafu wa kimatendo na kiitikadi na kuwatoharisha safi…”

Ewe Ibnu Hajar je umechunga haya yote na kumhifadhi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) katika Ahlul-Bayt wake na umewafanya mawalii wako na kuchukua dini kwao tu?! Au mwasema kwa midomo yenu ambayo hayapo myoyoni mwenu **“Chuki imekuwa kubwa kwa Mwenyezi Mungu mseme ambayo hamyatendi.”**

Imam Swadiq (a.s.) amesema kweli aliposema: “Wanajigamba kutupenda hali wanatuasi.” Hivyo Ibnu Hajar na walio mfano wake wanajigamba kuwapenda Ahlul-Bayt hali wanawafanya mawalii na kuichukuwa dini yao kutoka kwa waliowadhulumu Ahlul-Bayt. Huyu Ibnu Hajar mwenyewe anapothibitisha fadhila za Ahlul-Bayt na anatambua ulazima wa kushikamana nao, bado hapo hapo anafanya shambulizi lake dhidi ya Shia katika *Swawaiqu* yake na kuwaweka safu moja na vikundi vipotovu, na anawamwagia tuhuma mbaya na matusi machafu mno.

Ewe Ibnu Hajar nini dhambi yao?! Je ni kwa sababu wao wamewapenda Ahlul-bayt na kushikamana nao kwa kuchukua dini kwao?!

HOJA DHIDI YA HADITHI YA “VIZITO VIWILI”

Ibnu Al-Jawziy ameitia dosari katika kitabu chake *Al-Ilalul-Mutanaahiya Fil-Hadithil-Waahiyah*. Alipoitaja Hadithi ya kushikamana na vizito viwili: “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu” Amesema: “Hadthi hii haisihi. Ama kuhusu Atiya, ni kuwa Ahmad, Yahya na wengine wamemfanya kuwa yu dhaifu. Ama Ibnu Abdul-Qudus, Yahya amesema: ‘Si chochote yeye ni Rafidhi khabithi.’ Ama Abdullahi bin Daahir, Ahmad na Yahya wamesema: ‘Si kitu, haandiki toka kwa mtu aliye na kheri.’”

Kujibu hoja husika:

Hadithi ya vizito viwili haiishii kwenye sanad hii, kwa kweli imeelezwa kwa sanad nyingi kama ilivyotangulia.

Kwa hakika Muslim ameieleza katika Sahihi yake, kwa njia nyingi, ni wazi kuwa kuieleza Muslim riwaya hii japo kwa njia moja yatosha kuithibitishia ukweli wake, hili halina tofauti kati ya waislamu masunni.

Kama alivyoieleza At-Tirmidhiy ndani ya Sahihi yake kwa njia nyingi. Kutoka kwa Jabir, na Zayd bin Arqam, Abu Dharr, Abu Said na Hudhayfa.

Maneno ya Ibnu Al-Jawziy mwenyewe ndani ya kitabu chake *Al-Mawdhuuati* Juz.1, Uk. 99 tamko lake ni kama ifuatavyo: "Ukiona Hadithi imetoka nje ya usajili wa kiislam (*Al-Muwatau*, *Musnad* ya Ahmad, *Sahihayni*, *Sunan Abi Daud*, *Tirmidhiy* na mfano wa hizo) basi ichunguze, ikiwa kuna mfano wake katika vitabu Sahih (*Sahih-Sita*) na vizuri basi jambo lake lipo karibu mno…" Na yeye kwa usemi huu anajipinga mwenyewe kwani imeelezwa Hadithi hii katika vitabu ambavyo ameviita usajili wa kiislam, kama ilivyokwisha kupitia!

Kwa kweli maneno ya Ibnu Al-Jawziy kumhusu Atiyah hayakubaliki, kwa kuwa Ibnu Saad amemhesabu kuwa ni mwaminifu wa hadithi, kwani Ibnu Hajar Al-Asqalani amesema: "Ibnu Saad amesema: 'Atiyyah alitoka pamoja na Ibnu Al-Ash'ath, ndipo al-Hajjaj alipomwandikia Muhammad bin al-Qasim amwambie amtukane Ali, na endapo hatofanya hivyo mpige mijeledi mia nne na nyoa ndevu zake. Alimwita, na alikataa kumtukana Ali, hivyo alitekeleza hukumu ya al-Hajjaj kwake. Hatimaye alikwenda Khurasani alibakia huko mpaka Umar bin Habiir alipokuwa liwali wa Iraq, akaenda Iraq na alibaki huko mpaka alipokufa mwaka wa mia na kumi, alikuwa mwaminifu inshaallah na alikuwa na Hadithi njema."'[51]

Yajulikana kuwa Ibnu Saad ni miongoni mwa *Nawasibu*[52] ambao wanawafanyia uadui Ahlul-Bayt kiasi cha kumfanya Imam Jafar bin Muhammad Swadiq (a.s.) kuwa ni dhaifu. Hivyo kule kumfanya kwake Atiyah kuwa ni mwaminifu kunamtosha hasimu.

51 *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 2, Uk. 226.

52 *Nawasibu:* Ni watu wanaowafanyia uadui Ahlul-Bayt.

Kwa kweli Atiyah ni katika wapokezi wa Ahmad bin Hanbali, na Ahmad haielezei riwaya ila kutoka kwa waaminifu, kama ijulikanavyo, hivyo Ahmad alieleza riwaya nyingi mbalimbali kutoka kwake. Hivyo basi kunasibisha kuwa Ahmad alimuona Atiya kuwa ni dhaifu ni uwongo wa dhahiri. Kwani Taqiyu al-Sabakiy amesema: "Ahmad - Mwenyezi Mungu amrehemu - alikuwa haelezi riwaya ila kutoka kwa mwaminifu. Hasimu amesema wazi (anamkusudia Ibnu Taymiyya) hilo katika kitabu alichokitunga kumpinga al-Bakriy baada ya kurasa kumi za kitabu hicho, amesema: 'Kwa hakika wazungumziao *Jarhu* na *Taadiil* miongoni mwa wanavyuoni wa Hadith wako aina mbili: Miongoni mwao kuna ambaye haelezei hadithi ila kutoka kwa aliye mwaminifu kwake, kama vile Malik, na Ahmad bin Hambal.....' Hivyo basi kwa usemi huu hasimu ametutosheleza kazi ya kubainisha kuwa Ahmad huwa hapokei ila toka kwa mwaminifu, hapo basi hatobaki wa kumkebehi katika Hadithi."**53**

Sibtu Ibnu Al-Jawziy anathibitisha uaminifu wa Atiya: Kwa kweli amebainisha uaminifu wa Atiyyah na amekanusha kumfanya kuwa yeye ni dhaifu, pale aliposema baada ya kuleta kauli ya Nabii (s.a.w.w) kumhusu Ali (a.s.): "Si halali kwa yeyote asiye kuwa mimi au wewe awe na janaba ndani ya msikiti huu." "Kama itasemwa Atiyyah ni dhaifu, watasema na dalili ya udhaifu wa Hadithi ni kuwa Tirmidhiy amesema: 'Na nimeisimulia Hadithi hii au ameisikia kutoka kwangu Muhammad bin Ismail – yaani Bukhari – naye akajitenga nayo.'

"Najibu: Kwa kweli Atiyyah al-Aufiy amekuwa mpokezi kutoka kwa Ibnu Abbas na kwa Swahaba na alikuwa mwaminifu. Ama kauli ya Tirmidhiy kutoka kwa Bukhariy alijitenga nayo kwa sababu ya kauli yake (s.a.w.w): "Simhalalishii ila aliye tohara, si mwenye hedhi wala mwenye janaba." Na imepatikana kutoka kwa Shaafiy: 'Ni halali kwa mwenye janaba kuvuka msikitini.' Na kutoka kwa Abu Hanifa: 'Si halali mpaka aoge, kwa sababu ya kuwepo kwa tamko linaloharamisha. Na Hadithi ya Ali huchukuliwa

53*Shifaul-Asqam* Juz.10, Uk. 11.

kuwa yeye ilikwa ni mahsusi kwake hilo, kama ilivyokuwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), kwani vitu kadhaa vilikuwa mahsusi kwake."'[54]

Nasibisho la Ibnu Al-Jawziy kuwa Yahya bin Muiyn kamdhaifisha Atiyyah halikubaliki, kwa sababu ya nukuu ya Dawriy kutoka kwa Ibnu Muiyn kuwa yeye (Atiyyah) ni mtu mwema. Bila shaka al-Hafidh Ibn Hajar amesema katika wasifu wa Atiyyah usemi ambao tamko lake ni: "Dawriy amesema kutoka kwa Ibnu Muiyn: 'Ni mwema."' Hivyo basi kikaporomoka alichokinasibisha Ibn al-Jawziy kwa Yahya bin Muiyn.[55] Zingatia.

Na linalojulisha kutoijua kwa Ibnul Jawziy Hadithi ya Vizito Viwili ni dhana yake kuwa kwa kumdhaifisha Atiyyah peke yake ni hoja tosha ya kuidhaifisha Hadithi ya Vizito Viwili. Hali yajulikana kuwa kuthibiti kwa uaminifu wa Atiyyah au kuthibiti kwa udhaifu wake hakuitii dosari Hadithi ya Vizito Viwili. Kwa kuwa hadithi ya Atiyya aliyoieleza kutoka kwa Abu Said pia Abu Tufail ameieleza kutoka kwa Abu Said, naye Abu Tufail yuahesabika katika tabaka la Swahaba.

Lau tukiachana na hilo ni kuwa kwa kweli usahihi wa Hadithi ya Vizito Viwili hautegemei riwaya ya Abu Said sawa iwe kwa njia ya Atiyya au Abu Tufail. Na hata tukikubali tu kimjadala kuwa riwaya ya Abu Said ni dhaifu katika njia zake zote, hilo haliidhuru kitu Hadithi hii, kwa sababu ya riwaya zake na njia zake kuwa nyingi na mbalimbali.

Kumkanusha Ibnu Al-Jawziy kule kumdhaifisha kwake Ibnu Abdul-Qudus:

1. Ama kumtia dosari kwake Abdullah bin Abdul-Qudus hakukubaliki, kwa sababu al-Hafidh Muhammad bin Isa amemthibitisha kuwa ni

54 *Khulaswatul- Abaqaatul-Anwar*. Juz. 2, Uk. 45.

55 *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 7, Uk. 225.

mwaminifu. Al-Hafidh Al-Muqdisiy amesema katika wasifu wa Abdullah aliyetajwa: “Ibnu Udiyi amenena kutoka kwa Muhammad bin Isa kuwa yeye amesema: ‘Yeye ni mwaminifu.”’[56]

Na al-Hafidh Ibn Hajar al-Asqalaniy amesema: “Na imeelezwa kutoka kwa Muhammad bin Isa kuwa yeye amesema: ‘Ni mwaminifu.”’[57]

Na Muhammad bin Isa yeye ni kama alivyosema al-Hafidh Dhahabi katika wasifu wake: “Abu Hatim amesema: ‘Ni mwaminifu mwenye kuaminika. Sijamuona katika wasimulizi wa hadithi mwenye kuhifadhi zaidi milango kuliko yeye. Na Abu Daud amesesma: Ni mwaminifu.”’

2. Muhammad bin Hayyan amemuweka miongoni mwa waaminifu, na akasema Ibnu Hajar kwenye wasifu wake: “Ibnu Hayyan amesema yu katika waaminifu.”[58]

3. Haythamiy amenakili kwenye *Majmauz-zawaaid*, amesema: “Bukhari na Ibnu Hayyan wamemzingatia kuwa ni mwaminifu.”

4. Asqalaniy amesema kwenye wasifu wake: “Bukhari amesema: ‘Yeye katika asili ni mkweli ila tu ni kwamba ni mpokezi kutoka kwa kaumu ya watu dhaifu.’”

Kwa hiyo Bukhari kumshakia Ibnu Abdul-Qudus baada ya kumthibitisha kuwa ni mpokezi wa madhaifu, shaka hiyo haielekezwi kwenye hadithi hii, kwa sababu Ibnu Abdul’Qudus ameieleza Hadithi ya Vizito Viwili ambayo ameileta Ibnu Al-Jawziy kutoka kwa Aamash, naye ni mwaminifu.

---

56 *Khulaswatul- Abaqaatul-Anwar*. Juz. 2, Uk. 47. Nukuu kutoka kwenye *Al-Kamal Fi Asmair-Rijal*.

57 *Tahdhibut-Tahdhib*, Juz. 5, Uk. 303.

58 *Tahdhibut-Tahdhib*, Juz. 5, Uk. 303.

5. Abdullah bin Abdul-Qudus ni miongoni mwa wapokezi wa Bukhari katika Sahihi yake katika maelezo ya ziada, kama ilivyo katika *Tahdhib*, Juz. 5, Uk. 303, na *Taqribut-Tahdhib*, Juz. 1, Uk. 430. Na kitendo cha Bukhari kumweka Bwana huyu – Abdullahi bin Abdul'Qudus - japo iwe amemuweka katika maelezo ya ziada, ni dalili ya kuthibitisha uaminifu wake.

Ibnu Hajar al-Asqalaniy amesema katika utangulizi wa *Fat'hul-Bariy Fii Sharhi Sahih Al-Bukhariy*, pale anapojibu kule kukebehiwa kwa wapokezi wa wa Bukhari:

Na kabla ya kuingia humo inambidi kila mwenye insafu ajue kuwa kumuweka mpokezi yeyote yule ndani ya Sahihi – yaani Al-Bukhari – yalazimu uadilifu wake kwake, udhibiti wake na kutokuwa kwake na mghafala. Na khaswa hilo laongezewa na kule kuafikiana kwa jamhuri ya maimamu kuviita vitabu viwili hivi kuwa ni Sahih mbili. Na maana hii haipatikani kwa asiyetoka katika Sahih mbili."

6. Abdullah bin Abdul-Qudus ni katika wapokezi wa Tirmidhiy.

7. Kama ambavyo dosari ya Abdullahi bin Abdil-Qudus haiudhuru usahihi wa Hadithi hii. Hata kwa riwaya ya Al-Aamash kutoka kwa Atiyyah kutoka kwa Abu Said, kwa sababu ya Abdullah bin Abdul-Qudus kutopokea yeye peke yake riwaya hiyo kutoka kwa al'Aamash. Kwani kwa hakika wameielezea kutoka kwa Al-Aamash: Muhammad bin Talha bin al-Misrafu al-Yaamiy, na Muhammad bin Fadhiil bin Ghazawan al-Dhwabiy ndani ya *Musnad*, na *Tirmidhiy*, kama ilivyo kupitia. Na hii ni dalili ya ukweli wa riwaya.

Kama ambavyo Al-Aamash hakuipokea yeye pekee riwaya hii kutoka kwa Atiyyah. Al-Aamash ameelezea kutoka kwa Abdul-Malik bin Abu Sulayman Maysariy Azramiy na Abu Israil Ismail bin Khalifa Al-Absiy, kama ilivyo katika *Musnad* ya Ahmad kama ilivyo kupitia. Na kutoka kwa

Harun bin Saad Al-Ajaliy na Kathiyr bin Ismail At-Taymiy, kama ilivyo ndani ya *Muujamut-Tabraniy*.

Kumdhoofisha kwake Abdullah bin Daahir kwa sura ya jumla:

Kufanya hivyo ni kinyume na asili na kanuni za *Jarhu na Taadiil* kwa kuwa kumtia dosari isiyo wazi, haikubaliwi kutoka kwa yoyote awaye.

Hapakuwa na sababu yenye maana ya kumtia dosari, ila tu ni kwa ajili ya riwaya yake ya fadhila za Jemedali wa waumini, kama alivyosema Dhahabi: “Ibnu Adiy amesema: ‘Aghlabu riwaya zake huzungumzia fadhila za Ali, naye ni mwenye kutuhumiwa kwa hilo.’” Na kumfanya dhaifu kwa sababu hiyo hakukubaliki.

Na ni miongoni mwa maajabu na mabaya kumhusu Ibnu al-Jawziy kufanya vitimbi kwa kiwango hiki ili kuidhoofisha Hadithi hii, kwa kumwingiza Abdullah bin Daahir katika sanad ya Hadithi, hali yajulikana kuwa hajapata kuwa katika sanad yoyote miongoni mwa sanad za Hadithi hii kabisa! Hebu rejea riwaya za mwanzo na ambazo hatukuzitaja, je wamkuta katika sanadi zake Abdullahi bin Daahir?! Wala siipati maana ya kufanya hivyo ila ni uadui wake kwa Ahlul-Bayt na utashi wake wa kuzifukia haki zao. Lakini “Mwenyezi Mungu anakataa ila aitimize nuru yake japo makafiri wachukie.” Zingatia.

Sibtu Ibnu al-Jawziy baada ya kuileta Hadithi ya Vizito Viwili kutoka kwenye *Musnad Ahmad bin Hanbal* amesema: “Ikisemwa: Babu yako amesema katika kitabu al-Wahiyah:…… - Na hapo akayaleta maneno ya Ibnu Al-Jawziy katika kuidhoofisha Hadithi kama ilivyotangulia. Nitasema: Hadithi tuliyoieleza ameiandika Ahmad katika *Al-Fadhail*, wala katika sanad yake hakuna yoyote aliyedhoofishwa na babu yangu. Na Abu Daud ameiandika katika Sunan yake na Tirmidhiy pia na wanahadithi wote. Razinu ameitaja ndani ya *Al-Jam’u Bayna Swihahi*. La ajabu ni vipi yalifichika kwa babu yangu aliyoeleza Muslim ndani ya Sahihi yake mion-

goni mwa hadithi za Zaydu bin Arqam."[59]

Alilosema Sibtu Ibnu Al-Jawziy si chochote ila ni kumtetea Ibnu Al-Jawziy, kwani kama si hivyo basi yeye haghafiliki na Hadithi hii iliyoshuhudiwa na vyanzo vya waislamu pamoja na wingi wa mitizamo yake na uelewa, lakini yeye alitaka kufanya hadaa na vitimbi, na ndipo Mwenyezi Mungu akamfanyia vitimbi na akalifedhehesha jambo lake.

SHAKA YA IBNU TAYMIYAH

Ama shaka ya Ibnu Taymiya kuihusu Hadithi ya Vizito Viwili katika kitabu chake *Minhajus-Sunnah*, ni duni mno si kiasi cha kujadiliwa, lakini tutataja katika njia ya kuzipinga fikra hizi zisizo na maana, ambazo hazi-julishi ila ubaya wa uelewa na kuchanganyikiwa na kukithiri kwa dhana zisizo na msingi. Ibnu Taymiyya aliposhindwa kuidhoofisha Hadithi ya Vizito Viwili upande wa sanad kama ilivyo kawaida yake, ya kudhoofisha kila linalokuja na fadhila za Ahlul-Bayt, ndipo kwa makusudi kabisa alielekea kwenye utaratibu mwingine ambao hatujauona kwenye jambo lingine, nao ni usemi wake: "Kwa kweli Hadithi hii haijulishi wajibu wa kushikamana na Ahlul-Bayt, isipokuwa yajulisha wajibu wa kushikamana na Qur'ani tu."

Je ni nani mwenye akili anayepata maana hii na uelewa kama huu kutoka katika tamko hili la wazi? Na dhahiri ya Hadith yakata shauri na kutilia nguvu ulazima wa kushikamana na viwili vya thamani: Kitabu na Kizazi. Kama si hivyo basi nini maana ya vya thamani viwili? "Hakika mimi ni mwenye kuacha kati yenu vizito viwili". Na ni nini maana ya kauli yake (s.a.w.w): "Endapo mtashikamana navyo viwili"?! Lakini chuki binafsi inapofusha nyoyo.

Na ametoa dalili – yaani Ibn Taymiyya – kwa hadithi moja katika *Sahih Muslim* kutoka kwa Jabir, na Hadithi zingine zilizobaki amezipiga ukutani

59 *Tadhkiratu Khawasul-Umma.*

au amejighafilisha mbali nazo japokuwa riwaya zake ni nyingi na zina njia mbali mbali. Nayo ni hadithi inayoonyesha kwa mwenye kuzingatia kuwa ni hadithi iliyokatika sanadi yake kwa kuilinganisha na Hadithi zilizobaki zilizokuja katika mlango huu huu. Hadithi yenyewe ni: “Nimeacha katika ninyi ambalo hamtopotea baada yake, endapo mtashikamana nalo, Kitabu cha Mwenyezi Mungu..” Na hadithi hii kukatika na kupotoshwa kwake kupo dhahiri, kwani hadithi ya Jaabir mwenyewe imekuja katika riwaya ya Tirmidhiy, na humo mna amri ya wazi ya wajibu wa kushikamana na Ahlul-Bayt. Na tamko la Hadithi kama ilivyotangulia katika riwaya ya Tirmidhiy ni: “Enyi watu! Hakika mimi nawaachieni kati yenu ambalo mkilichukua hamtopotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu watu wa nyumba yangu.”

Kama ambavyo shaka hii hii pia yamrejelea Ibnu Taymiyya, kwa kuwa yeye anasema: “Ni wajibu kushikamana na Kitabu na Sunna.” Ni lazima amri kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) iwe moja, ima inayolazimisha kushikamana na Kitabu tu, au Kitabu na Sunna. Na Ibnu Taymiyya alipochagua wajibu wa kushikamana na Qur’ani tu, hapo wajibu wa kushikamana na Sunna unaanguka kwa mujibu wa maneno yake. Na hiyo ni kinyume na mwendo wa Ibnu Taymiyya, kama ilivyo dhahiri katika madhehebu yake ya Ahlu Sunna, kama ambavyo amekiita kitabu chake ambacho ndani yake ameitaja Hadithi hii *Minhajus-Sunnah*, wala hakukiita *Minhajul-Qur’ani*!

Na ikiwa katika itikadi yake ni kuwa Hadithi hii aliyoitaja haibatilishi Hadithi yakushikamana na Kitabu na Sunna, basi pia haibatilishi wajibu wa kushikamana na Kitabu na Kizazi.

Ibnu Taymiyya hakuishia katika kiwango hiki, hivyo basi akasema kuhusu: “....Na kizazi changu, kwa hakika havitoachana mpaka vinifikie katika bwawa”: “Hii ameieleza al-Tirmidhiy. Ahmad aliulizwa kuhusu hii. Na wameidhoofisha wanavyuoni zaidi ya mmoja, wamesema kwa kweli si sahihi.”

Najibu: Utahisi katika kauli yake kuwa tamko hili la Hadithi halijaelezwa na yoyote ila Tirmidhiy. Na ulikwishajua kama ilivyotangulia kuwa hiyo imeelezwa na zaidi ya mmoja miongoni mwa ulamaa wa kisunni na wanahadithi wao.

Basi nini anakusudia kwa kauli yake: Ameipokea Tirmidhiy?! Je kupokewa na Tirmidhiy ni dalili ya udhaifu wake?! Na nani ambaye alimuuliza Ahmad?! Na alimjibu nini?! Na kauli hii ilikuwa mahali gani?! Au Ahmad mwenyewe hakuieleza na hakuizingatia kuwa ni sahihi?! Na nani alimdhoofisha hata aseme: Si mmoja ?! Basi ni kwa nini hakuwataja?!

Na yasiyo hayo miongoni mwa maswali ambayo yaweza yakaelekezwa kwa Ibnu Taymiyya, akiyajibu kwa maneno thabiti tutaikubali shaka yake, wala haiwezekani tuikubali hovyo hovyo tu, nayo iko katika sura ya jumla. Lakini hii ni tabia ya Ibnu Taymiyya akipania kuupotosha umma na kuufunika ukweli.

Hizi ndizo shaka muhimu zilizokuja katika mlango huu na wala sijapata kumuona kulingana na ufuatiliaji wangu ambaye anaiponda Hadithi ya Vizito Viwili iliyothibiti kwa mfululizo na ambayo wamekiri kuwa ni sahihi watu maarufu katika umma miongoni mwa mahafidhu na wanahadithi, na wala hathubutu kuikebehi isipokuwa mwenye moyo muele uliojaa chuki na hasira kuwaelekea Ahlul-Bayt. Na baada ya kuthibiti kwetu kwa wazi kabisa ukweli wa Hadithi hii, ni wajibu sasa juu yetu kuiweka wazi dalili na baada ya hivyo kujiambatanisha nayo.

HADITHI HII NI DALILI YA UIMAMU WA AHLUL-BAYT

Hadithi kujulisha ustahiki wa uimamu kwa Ahlul-Bayt ni katika mambo yaliyo wazi na dhahiri mno kwa kila mwenye insafu, kwa kuwa inafidisha wajibu wa kuwafuata katika itikadi na hukumu na rai na kutofanya kinyume nao, kwa kauli au kitendo, kwa sababu kazi yoyote itakayotoka nje ya wigo wao itazingatiwa kuwa imetoka nje ya Qur'ani, na kwa hilo inakuwa iko nje ya dini. Na wao kwa hilo wanakuwa ndio kipimo thabiti ambacho kwacho hujulikana njia iliyonyooka na njia iliyo sawa, kiasi kwamba uongofu hauwi ila kwa njia yao na upotovu hauwi isipokuwa kwa kufanya kinyume na wao: "Mkishikamana na viwili hivi hamtopotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu." Kwa kuwa kujiambatanisha na Qur'ani maana yake ni kufanya kwa mujibu wa yaliyo ndani yake, yaani kuamrika na amri zake na kujikataza makatazo yake, na ni hivyo hivyo inakuwa katika kushikamana na Kizazi. Hiyo ni kulingana na kanuni ya: Kipatikanacho kwa sharti hakitopatikana ila kwa kutimia sharti. Kama ambavyo nomino katika (viwili) inarejea kwenye Kitabu na Kizazi. Sidhani mwarabu mwenye kupewa ufahamu wa lugha ya kiarabu japo kidogo atakuwa kinyume na hilo.

Kwa mujibu huo inakuwa kuwafuata Ahlul-Bayt baada ya Mtume (s.a.w.w) ni wajibu kama ilivyo kuifuata Qur'ani ni wajibu, na hilo liko mbali na maudhui ya 'Je Ahlul-Bayt ni nani?' kwa kuwa huu ni udadisi wa baadaye, la muhimu hapa ni kuthibitisha kuwa amri, katazo, kufuatwa, na kuigwa ni haki ya Ahlul-Bayt, na wao ni mfano wa kuigwa. Ama kuainisha utambulishi wao kwenyewe kupo nje ya wigo wa mazungumzo haya, kama wasemavyo wanavyuoni wa misingi ya sheria: "Hakika kadhia haithibitishi maudhui yake." Kwa hiyo kwa dharura tija inakuwa Ahlul-Bayt wao ndio makhalifa baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w).

Na kauli yake (s.a.w.w): “Hakika mimi nawaachieni kati yenu” ni tamko linalobainisha wazi kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amewafanya makhalifa na ameusia umma uwafuate, na amesisitiza hilo kwa kauli yake (s.a.w.w): “Angalieni jinsi mtakavyonifuata katika viwili hivi.” Hivyo ukhalifa wa Qur’ani uko wazi, na ukhalifa wa Ahlul-Bayt hauwi ila kwa uimamu wao. Na kwa hivyo Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi cha Mtume wake (s.a.w.w) ndio sababu inayofikisha kwenye radhi za Mwenyezi Mungu, kwa sababu wao ni kamba ya Mwenyezi Mungu ambayo Mwenyezi Mungu ametuamuru kushikamana nayo: **“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu.....” (*Sura Ali Imran*: 103)**

Na Aya hapa ni jumuishi haijaainisha na kuiwekea mpaka kamba ya Mwenyezi Mungu, au lolote liwezalo kubainika kutoka humo ambalo ni wajibu kushikamana nalo. Ndipo Sunna ikaja na Hadithi ya Vizito Viwili na hadithi zingine, kubainisha kuwa kamba ambayo ni wajibu tushikamane nayo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu pamwe na kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w).

Na hilo limesemwa na kundi la wafasiri: Ibnu Hajar amewataja katika kitabu chake *Swawaiqul-Muhriqah* katika mlango wa yale yaliyoteremshwa kuwahusu Ahlul-Bayt. Rejea huko.

Na Al-Qunduziy ameitaja katika kitabu chake *Yanabiul-Mawaddah* amesema katika kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): **“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu.....”**: “Tha’alabiy ameandika kutoka kwa Aaban bin Taghlabi kutoka kwa Jafar Swadiq (a.s.) akasema: ‘Sisi ndio Kamba ya Mwenyezi Mungu ambayo Mwenyezi Mungu Mwenye enzi na utukufu amesema: **“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu wote na wala msifarakane.” (*Surat Aali Imran*: 103)** Na pia ameandika mwandishi wa kitabu *Al-Manaqib* kutoka kwa Said bin Jubair kutoka kwa Ibnu Abbas kutoka kwa wawili hawa, amesema: ‘Tulikuwa kwa Mtume (s.a.w.w.), punde si punde alikuja bedui na akasema: “Ewe Mtume wa

Mwenyezi Mungu nimekusikia unasema: Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu, hivyo kamba ya Mwenyezi Mungu ni ipi, ambayo tushikamane nayo?" Hapo Nabii (s.a.w.w) aliupiga mkono wake juu ya mkono wa Ali na akasema: 'Shikamaneni na huyu, ndiyo kamba madhubuti ya Mwenyezi Mungu."'[60]

Ama usemi wake (s.a.w.w): "Hawatofarakana mpaka wanijie kwenye bwawa." yajulisha sababu kadhaa:

Kwanza: Kuthibiti umaasumu kwao wao, kwa kuwa kuambatana kwao na Kitabu ambacho hakiwezijiwa na batili mbele yake wala nyuma yake, ni dalili ya elimu yao ya yaliyomo ndani ya Kitabu na kuwa wao hawafanyi kinyume na Kitabu kwa kauli wala kitendo. Kwani ni wazi kuwa kutokea lolote kwao kinyume na Kitabu sawa iwe kwa makusudi au kusahau ni kuthibitisha kufarakana kwao na Qur'ani, na hali Hadithi yaeleza wazi kutofarakana kwa wawili hawa mpaka wafike kwenye bwawa wakiwa pamoja, vinginevyo itakuwa ni kumkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), kama ambavyo ufahamu huu unaungwa mkono na dalili kutoka katika Qur'ani na Sunna. Tuahirishe utafiti katika hilo mpaka mahali pengine.

Pili: Kwa kweli (*Lan*) inafidisha: "*Abadan*", hivyo inakuwa kushikamana na wao wawili – Kitabu na Kizazi – ni kizuizi cha upotovu daima na abadan, na hilo halitimii ila kwa kushikamana na wote wawili pamoja, sio kushikamana na mmoja wao peke yake kama ilivyotangulia, na usemi wa Mtume (s.a.w.w) katika riwaya ya Tabaraniy: "Msiwatangulie mkaja mkaangamia na wala msiwaelimishe kwa kuwa wao wana elimu zaidi yenu." unasisitizia maana hii.

60 *Al-Yanaabiul-Mawaddah*, Uk.118. Manshuratu muasasatul'a'alamiy. Beirut-Lebanon.

Tatu: Kubakia kwa kizazi pembeni ya Kitabu mpaka Siku ya Kiyama, hivyo hapana zama itakuwa bila ya wao. Na maana hii ameileta karibu Ibnu Hajar ndani ya *Swawa'iq* yake: "Na katika hadithi za himizo la kushikamana na Ahlul-Bayt kuna ishara ya kutokatika kwa mwenye kustahiki miongoni mwao kushikamana naye mpaka Siku ya Kiyama, kama ambavyo Kitabu kitukufu nacho ni hivyo hivyo. Kwa ajili hiyo wao ni amani kwa watu wa ardhini, kama itakavyokuja, na hilo linashuhudiwa na habari zilizotangulia: 'Katika kila kizazi cha umma wangu kina waadilifu miongoni mwa Ahlul-Bayt wangu.' Kisha mwenye haki zaidi ya kushikamana naye miongoni mwao ni imamu wao, na mwanachuoni wao Ali bin Abu Talib, kutokana na tuliyotanguliza miongoni mwa kuzidi elimu yake na fatwa zake za kina."[61]

Nne: Kama ambavyo yajulisha kupambanuka kwao na elimu yao ya ufafanuzi wa sheria, na hivyo ni kwa sababu ya kuambatana kwao na Kitabu ambacho hakiachi dogo wala kubwa, kama alivyosema (s.a.w.w): "Wala msiwafundishe kwani wao ni wajuzi mno kuliko ninyi."

Muhtasari: Hapana budi apatikane lau mmoja kutoka Ahlul-Bayt katika kila zama mpaka Kiyama kitakapowadia, kauli yake na kitendo chake hakihitilafiani na Qur'ani, ili asiwe mbali nayo, na maana ya hatofautiani na Qur'ani kwa kauli na kitendo ni kuwa yeye ni maasumu kikauli na kivitendo, na ni wajibu kumfuata kwa kuwa yeye ni dhamana ya kutoingia kwenye upotovu. Na maana hii haisemwi isipokuwa na Shia, kwa sababu wao wanasema kuwepo Imam kutoka miongoni mwa Ahlul-Bayt, ambaye ni maasumu dhidi ya kukosea na kuteleza, ambaye ni wajibu kumtawalisha na kumtambua, hiyo ni kulingana na maana hii ya kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu: "Ambaye atafariki dunia bila ya kumjua Imamu wa zama zake atakuwa amekufa kifo cha kijahili (yaani muda kabla ya Uislamu). Na imejulisha maana hii kauli yake (s.w.t): **"Siku ambayo tutawaita kila watu kupitia Imamu wao."**

61 *Swawaiq* Uk. 151.

MLANGO WA NNE

JE AHLUL-BAYT NI NANI?

Je Ahlul-Bayt ni nani?:

Utafiti huu ni miongoni mwa tafiti za wazi mno, kwa kuwa mtu hawezi kujifanya hawajui Ahlul-Bayt, ila yule mkaidi ambaye hajapata upenyo wa kuzikimbia dalili za kata shauri za kuwajibika kuwafuata. Hivyo basi mtu kama huyu huwa anageukia kwenye mbinu za kuwatilia shaka. Na hili ni ambalo nimelishuhudia mimi mwenyewe nilipokuwa nikijadiliana na baadhi ya ndugu na jamaa, basi pindi mmoja wao anapokosa upenyo wa kuikwepa lazima ya kuwafuata Ahlul-Bayt utamkuta moja kwa moja analeta maswali yasiyofahamika: Ahlul-Bayt ni nani? Je wake zake sio ahali zake?! Je Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hajasema: Salman ni miongoni mwetu Ahlul-Bayt?! Bali je Abu Jahli pia sio miongoni mwa ahali wake (s.a.w.w)?!

Wala hakusudii lolote kwa maswali yote haya isipokuwa kukanusha ukweli wa Hadithi ya Vizito Viwili kuwa ni miongoni mwa hadithi zinazojulisha uimamu wa Ahlul-Bayt, akidhania kwa maswali haya ya kuduwaza yasiyo wazi anaweza kuinyamazisha akili yake na wito wa dhamiri yake, lakini umbali ulioje hoja ipo hadhiri sawa akanushe au asikanushe.

Nilikuwa ninasema kwa baadhi yao mtu anapouliza maswali kama haya: Kwa nini ninyi mnataka kila kitu kiwe kimekwisha andaliwa mkipate bila ya taabu wala kutafiti?! Kwa kweli fikra zilizowekwa kwenye mkebe hazifai. Mimi naweza kujibu na ninyi mwaweza kupinga majibu yangu na mkayakanusha na mkayapinga kwa kuwa ninyi hamjaonja uchungu wa utafiti na wala hamjavumilia mashaka ya kujibu. Halafu je hivi mimi ni peke yangu ndiye nilazimikae kujibu? Je Mtume wa Mwenyezi Mungu

(s.a.w.w) ameniamuru kushikamana na Ahlul-Bayt mimi tu khususan?! Sisi sote ni mukalafu na ni wajibu juu yangu na juu yenu kujibu, kwa sababu hoja imethibiti kwetu kuwa ni wajibu kuwafuata Ahlul-Bayt, na kuichukuwa dini kutoka kwao, kwa hiyo yalazimu kuwatambua na halafu kuwaiga wao?!

Na mimi pia hapa, sitoi dalili na uthibitisho kwa upana, ila tu natosheka na baadhi ya ishara za wazi, na mwenye kutaka ziyada ni juu yake kujipanua.

Ahlul-Bayt katika Aya ya tohara:

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema:

﴿ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرًا ﴿٣٣﴾ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa.” (Sura Ahzab:33).

Kwa kweli kuteremka kwa Aya hii iliyobarikiwa kuwahusu Ali, Fatima, Hasan na Husein, ni miongoni mwa mambo yaliyo wazi mno kwa mwenye kufuatilia vitabu vya hadithi na tafsiri.

Ibnu Hajar anasema kwa lengo hili: “Kwa kweli wafasiri wengi wanasema kuwa hii Aya ilishuka kuwahusu Ali, Fatima, Hasan na Husein.”**62** Na Aya hii kwa dalili yake iliy wazi juu ya umaasumu wa Ahlul-Bayt haina uwiano ila na wao, kwa lile ambalo tumeliwadhihisha hapo kabla, kwa sababu wao ni thamani ya umma huu. Na ni maimamu waongozi baada ya Mtume (s.a.w.w), na kwa sababu hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliamuru kuwafuata. Na ufidishaji wa umaasumu kutokana na Aya hii ni wa wazi kwa mwenye moyo wa kuelewa au akapewa usikivu akiwa

62 *Swawaiq* Uk. 143.

hadhiri. Hiyo ni kwa sababu ni muhali kulikosa kusudio ikiwa mkusudiaji ni Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Na zana ya kifungo ya kilugha iliyotumika ni shahidi juu ya hilo. La muhimu kwetu hapa ni kuthibitisha kuwa Aya hii khususan iliteremka kwa ajili ya Ali, Fatma Hasan na Husein (a.s.).

Hadithi ya Kishamia ni kiainishi cha utambulisho wa Ahlul-Bayt:

Dalili zilizo karibu mno na za wazi mno ni yale yaliyokuja katika tafsiri ya Aya hii miongoni mwa riwaya, khususan ile iliyojulikana kwa wanahadithi kuwa ni Hadithi ya Kishamia, usahihi wake na kufululiza kwake sio kuchache kwa kuilinganisha na Hadithi ya Vizito Viwili.

A) Al-Hakim ameeleza ndani ya kitabu chake cha A*l-Mustadrak Alas-Swahihayni Filhadithi*: “Kutoka kwa Abdullah bin Ja’far bin Abu Talib kuwa yeye amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alipoangalia rehema inashuka alisema: ‘Niitieni, niitieni.’ Safiyya akasema: ‘Nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema: ‘Ahlul-Bayt wangu, Ali, Fatima Hasan na Husein.’ Hatimaye wakaletwa. Nabii (s.a.w.w) aliwafunika shuka yake, halafu alinyanyua mikono yake na akasema: ‘Ewe Allah hawa ni ahali wangu. Mtakie rehema Muhammad na Aali Muhammad.’ Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu akateremsha

﴿ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرًا ﴿٣٣﴾ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa.” (Sura Ahzab: 33).”[63]

Al-Hakim amesema: “Hadithi hii sanad yake ni sahihi.”

B) Na Al-Hakim ameeleza riwaya nyingine mfano wa hii, kutoka kwa Ummu Salamah akasema: “Nyumbani mwangu iliteremka: **“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba”**

63 *Mustadrakul-Hakim,* Juz. 3, Uk. 197 – 198.

ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akatuma waitwe Ali, Fatima, Hasan na Husein, akasema: 'Ewe Allah! Hawa ndio Ahlul-Bayt wangu.'"[64]

Halafu al-Hakim akasema: "Hii ni sahihi kwa sharti ya Bukhari." Na ameieleza mahali pengine kutoka kwa Wathilah akasema: "Ni sahihi kwa sharti ya wawili, Bukhari na Muslim."

C) Muslim ameieleza ndani ya *Sahih* yake kutoka kwa Aisha akasema: "Alitoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) asubuhi akiwa na shuka ya manyoya meusi, punde alikuja Hasan bin Ali akamwingiza halafu alikuja Husein akamwingiza halafu alikuja Fatima akamwingiza halafu alikuja Ali akamwingiza halafu akasema: 'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa."'[65]

Na habari hizi zimekuja ndani ya riwaya nyingi katika vitabu Sahihi na vitabu vya Hadithi na Tafsiri.[66] Nazo ni katika habari zilizo sahihi zilizofululiza, hakuna yeyote aliyezidhaifisha miongoni mwa wa mwanzo na wa mwisho. Tukizitaja riwaya hizi zote nafasi itatuwia ndefu, hivyo mimi nimezihesabu miongoni mwazo riwaya ishirini na saba, zote ni sahihi.

Na miongoni mwa riwaya zilizo wazi mno ndani ya mlango huu katika kuwaainisha Ahlul-Bayt mbali na wengine miongoni mwa wake wa Nabii (s.a.w.w), ni riwaya aliyonakili Suyuti iliyomo ndani ya *Durul-Manthur* kutoka kwa Ibnu Mardawayhi kutoka kwa Ummu Salama akasema:

64 *Mustadrakul-Hakim*, Juz. 3, Uk. 197 – 198.

65 *Sahih Muslim*, mlango wa fadhila za Ahlul-Bayt.

66 *Sunanul-Kubra*, mlango wa kubainisha Ahlul-Bayt, na ambao ndio ahali zake. *Tafsirut Tabariy* Juz. 22, Uk. 5. *Tafsir Ibni Kathiyr* Juz. 3, Uk. 485. *Tafsir Durul-Manthur* Juz. 5, Uk.198 – 199. *Sahih Tirmidhiy*, mlango wa fadhila za Fatima. Na *Musnad Ahmad* Juz. 6, Uk. 292 – 323 na vingine.

“Iliteremka Aya hii chumbani mwangu: **“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa,”** hali ndani ya chumba mkiwa waheshimiwa saba: Jibril, Mikail, Ali, Fatima, Hasan, na Husein, hali mimi nikiwa kwenye mlango wa chumba. Nilisema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi si katika Ahlul-Bayt?!’ Alisema: ‘Kwa hakika wewe uko katika kheri, kwa hakika wewe ni miongoni mwa wake wa Nabii.”’[67]

Na katika riwaya ya Al-Hakim katika *Mustadrak* yake ni kuwa Ummu Salamah alisema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi si katika Ahlul-Bayt?!” Akasema (s.a.w.w): “Kwa hakika wewe uko katika kheri kwa hakika wewe ni miongoni mwa wake wa Nabii. Ewe Mwenyezi Mungu wangu Ahlul-Bayt wangu ni wenye haki zaidi.”’[68]

Na ilivyo katika riwaya ya Ahmad ni: “Nikainua Kishamia ili niingie akakivuta toka mkononi mwangu na akasema: ‘Kwa hakika wewe u katika kheri.”’[69]

Katika hayo inatosha kuthibitisha kuwa Ahlul-Bayt wao ndio watu wa kishamia kwa ibara za wazi mno na matamshi safi sana. Kwa hiyo wao wanakuwa kizito ambacho ni pacha wa Qur’ani ambacho Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ametuamrisha katika Hadithi ya Vizito Viwili kushikamana nacho.

Na mwenye kusema kuwa al-Itrah (kizazi) maana yake ni karaba ili aigeuze maana, usemi wake huu haukubaliwi, kwa kuwa hilo halijasemwa na yeyote miongoni mwa maimamu wa lugha ya kiarabu. Ibnu Mandhur amenakili katika *Lisanul-Arab:* “Kwa kweli Al-Itrah wa Mtume ni watoto wa Fatima (r.a).” Hii ni kauli ya Ibnu Sayida.

---

67 *Ad - Durul-Manthur*. Juz 5 Uk. 198.

68 *Mustadrakul-Haakim*. Juz. 2. Uk. 416. Tafsir ya Aya toka ***Surat Ahzab***.

69 *Musnad Ahmad*. Juz.3, Uk. 292 – 323.

Na Al-Azhariy amesema: “Na katika hadithi ya Zayd bin Thabit amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w):..... - na anaitaja Hadithi ya Vizito Viwili – akajaalia al-Itrah kuwa ni Ahlul-Bayt. Na Abu Ubaida na wengineo wakasema: ‘Al-Itrah wa mtu na familia yake na jamaa zake ni watu wake wa karibu. Ibnu Al-Athir amesema: Itrah wa mtu ni jamaa mahsusi wa karibu mno wa mtu. Na Ibnu Al-Arabiy amesema: Al-Itrah ni mtoto wa mtu na dhuria wake na wajukuze wa kutoka mgongoni mwake. Kwa hiyo Al-Itrah wa Nabii (a.s.) ni watoto wa Fatima al-Batul (a.s).”’[70]

Kutokana na maana hii inabainika kuwa Ahlul-Bayt sio ndugu wote wa karibu walio kwenye maana ya jumla ya neno Ahlul-Bayt, bali wao ni ndugu wake wa karibu mahsusi. Kwa minajili hiyo Zaid bin Arqam alipoulizwa kulingana na riwaya ya Muslim, wakasema: “Ahlul-Bayt wake ni nani, ni wakeze?” Alisema: “Hapana namuapa Mwenyezi Mungu, kwa hakika mwanamke huwa na mtu muda katika zama halafu anamtaliki na atarejea kwa baba yake na kaumu yake....Ahlul-Bayt wake (s.a.w.w) ni asili yake na ndugu zake wa kiumeni, ambao kwamba wameharamishiwa sadaka baada yake....”

Kama ambavyo utukufu wa kunasibika na Ahlul-Bayt hakuudai mtu yoyote miongoni mwa jamaa wa karibu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), wala wakeze. Kama si hivyo historia ingetuhadithia hilo, wala hapana katika historia wala Hadithi kuwa wake wa Nabii (s.a.w.w) walitoa hoja kwa Aya hii na kudai utukufu huu, kinyume na Ahlul-Bayt, kwani huyu hapa Jemedari wa waumini (a.s.) anasema: “Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mwenye enzi na utukufu ametufanya bora sisi Ahlul-Bayt. Na vipi isiwe hivyo hali Mwenyezi Mungu mwenye utukufu na enzi anasema kitabuni mwake: **“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa.”** Kwa kweli ametutoharisha Mwenyezi Mungu kwa kutuweka mbali na yasiyopendeza, yaliyo dhahiri miongoni mwayo na yaliyofichika. Hivyo sisi tuko katika njia ya haki.”

70 *Lisanul-Arab* Juz. 9, Uk. 34.

Na mwanawe Hasan (a.s.) amesema: “Enyi watu, mwenye kunijua amenijua na asiyenijua basi mimi ni Hasan bin Ali, na mimi ni mtoto wa mbashiri, mwonyaji, mlinganiaji wa Mwenyezi Mungu kwa idhini yake, na ambaye ni taa itoayo nuru. Mimi ni katika Ahlul-Bayt, ni katika jumla ya watu wa nyumba ambayo ndani yake Jibril alikuwa anateremka na anapanda, na mimi ni katika Ahlul-Bayt ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatoharisha kabisa.”

Na mahali pengine anasema: “Na ninasema enyi viumbe sikieni, na nyinyi mna nyoyo na masikio, fahamuni kuwa sisi ni Ahlul-Bayt, Mwenyezi Mungu ametupa heshima kwa Uislamu, ametuchagua na kututeua, hivyo akatuondolea uchafu na ametutoharisha kuwa safi kabisa.”

Hoja ya Ibnu Kathiir kuwa kuna ulazima wa kuwaingiza wake wa Nabii (s.a.w.w) katika Aya hii kulingana na muktadha wa muundo wa sentensi, haina nafasi hapa. Kwa kuwa hoja ya udhahiri hutegemea umoja wa maneno, na yajulikana kuwa usemi umebadilika kutoka dhamiri ya kike katika Aya zilizoitangulia Aya hii, na kuwa ya kiume, hivyo basi ikiwa makusudio ya Aya hii ni wakeze usemi utakuwa:

إنما يريد الله ليذهب عنكنّ الرجس أهل البيت ويطهركنّ تطهير ا

kwa sababu Aya ziko mahsusi kwa wanawake, kwa ajili hiyo ameanza tena Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kauli yake baada ya Aya hii:

وذكرن ما يتلى في بيوتكن من آيات الله والحكمة.....

Wala hajapata kusema yoyote kuwa Aya ya tohara iliteremka kuwahusu wake wa Nabii (s.a.w.w) ila Ikrimah na Muqatil. Kwa hiyo Ikrima alikuwa akisema: “Mwenye kutaka nitaombeana naye laana, bila shaka yenyewe iliteremka ikiwahusu wake za Mtume (s.a.w.)”**[71]** Maneno haya ya Ikrima hayakubaliki kwa kupingana kwake na riwaya zilizo sahihi na safi, kama ilivyotangulia kuwa Ahlul-Bayt ndio watu wa Kishamia.

71 *Durul-Manthur* Juz.5, Uk.198.

Pili: Ni jambo gani lilimtikisa Ikrima na kuichochea ghadhabu yake kiasi cha kufikia anadi sokoni kutaka kulaaniana? Ni kwa sababu ya kuwapenda wake wa Nabii au ni chuki dhidi ya waliofunikwa na Kishamia? Ni haja ipi inapelekea kulaaniana ikiwa kweli inakubalika kuwa iliteremka kwa ajili ya wake wa Nabii (s.a.w.w.)?! Au rai ya walio wengi na iliyotawala ni kuwa iliteremka kumhusu Ali, Fatima, Hasan na Husein?! Na ndivyo ilivyokuwa, na lijulishalo hivyo ni maana iliyo kwenye usemi wake: “Si hilo mnaloliendea, bali ni wakeze Mtume.” hii inamaanisha kuwa Aya ilikuwa wazi kwa taabiina na wengineo kuwa iliteremka kwa ajili ya Ali, Fatima, Hasan na Husein (a.s.).

Kama ambavyo sisi hatuwezi kumkubali Ikrima kuwa hakimu wala shahidi katika jambo hili kutokana na lile ambalo limekwishajulikana kuhusu yeye, nalo ni uadui wake mkali dhidi ya Jemedari wa waumini (a.s.). Yeye ni miongoni mwa Makhawariju ambao walimpiga vita Ali, kwa hiyo ilikuwa juu yake aseme kuwa iliteremka kwa ajili ya wake za Nabii (s.a.w.w), kwa kuwa lau angekiri kuwa iliteremka kwa ajili ya Ali (a.s.) itakuwa amejitolea hukumu mwenyewe binafsi dhidi ya madhehebu yake na kutikisa misingi ya itikadi yake ambayo imemhalalishia yeye na wenzake kutoka kivita dhidi ya Ali (a.s.), na yasiyo hayo miongoni mwa mambo ambayo ni mashuhuri kwa Ikrima, kama vile kumsemea uwongo Ibnu Abbas mpaka Ibnu Al-Musayib alikuwa anamwambia huria wake aliyeitwa kwa jina la Burdu: “Usinisemee uwongo kama Ikrima alivyomsemea uwongo Ibn Abbas.” Na katika *Mizanul-Itidal* ni kuwa Ibnu Umar alisema hilo pia kumwambia mhuria wake Naafiu.

Na Ali bin Abdullah bin Abbas alijaribu kumzuia Ikrima na kumtoa katika tatizo hilo, na miongoni mwa nyezo alizozitumia ni kumsimamisha chooni ili aache uwongo dhidi ya baba yake. Abdullah bin Abil Harth anasema: “Niliingia kwa Ibnu Abdullah bin Abbas na Ikrima akiwa amedhibitiwa

kwenye mlango wa choo. Nikasema: Mwamtendea hivi huria wenu?" Akasema: 'Kwa kweli huyu anamsemea uwongo baba yangu.'"[72]

Ama Muqatil, yeye si wa chini kwa uadui wake dhidi ya Amirul-Mu'minina (a.s.) na umashuhuri wake kwa uwongo ukimlinganisha na Ikrima, kiasi kwamba Nasaiy amemhesabu katika jumla ya waongo walio maarufu wa kuzua Hadithi.[73] Na amesema Al-Jauzijaniy kama ilivyo katika wasifu wa Muqatil ndani ya *Mizanud-Dhahab*: "Muqatil alikuwa mwongo shupavu."[74]

Muqatil alimwambia Al-Mahdiy Al-Abbasiy: "Ukipenda nitakuwekea Hadithi kumhusu Abbas." Akasema: ''Sina haja nazo.''[75]

Na watu kama hao haifai tuchukuwe maneno yao, hiyo ni aina ya ghururi na ujinga, kwa kuwa Hadithi zilizo sahihi zilizofululiza ziko kinyume na hivyo, kama ilivyotangulia. Na hii ni kuachia mbali zile riwaya zisemazo kuwa baada ya kushuka kwa Aya hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alidumu miezi tisa akienda mlangoni kwa Ali bin Abu Talib (a.s.) wakati wa kila Swala na anasema: ''Amani iwe juu yenu, rehema za Allah na baraka zake, enyi Ahlul-Bayt. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa." Kila siku mara tano.[76]

Na katika *Sahih Tirmidhiy*, *Musnad Ahmad*, *Musnad Tayalisiy*, *Mustadrakul-Hakim Alas-Swahihayni*, *Usudul-Ghaba*, *Tafsiru-Tabariy*, Ibnu Kathir na Suyutiy: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akipita mlangoni kwa Fatima muda wa miezi sita, kila atokapo kwa ajili ya

72 *Wafayatul-Aayan* Juz.1, Uk. 320.
73 *Dalailus-Swidq* Jalada.2, Uk. 95.
74 *Kalimatul-Gharai* cha Sharafud-Din Uk. 217.
75 *Al-Ghadiir* Juz. 5, Uk. 266.
76 Tafsiri ya Aya kutoka kwa Ibn Abbas ndani ya kitabu *Durul-Manthur* Juz. 5, Uk. 199.

Swala ya alfajiri, na husema: ‘Swala enyi Ahlul-Bayt. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba, na kukutakaseni kabisa.”’[77]

Na zisizo hizo miongoni mwa riwaya zinazoshabihiana ambazo zimekuja katika mlango huu. Na kwa mujibu huo imetuwia wazi kuwa Ahlul-Bayt wao ni Ali, Fatima, Hasan na Husein, wala hakuna nafasi kwa mpingaji mwenye vitimbi, kuwa na shaka katika hili, kwani kufanya hivyo ni kama kuwa na shaka juu ya uwepo wa jua katikati ya mchana.

AHLUL-BAYT KATIKA AYA YA MUBAHALAH

Kwa kweli mapambano kati ya safu mbili, haki na batili kwenye uwanja wa vita ni jambo gumu, lakini ni gumu zaidi ikiwa katika medani ya Mihrabu, pindi kila mmoja anapong’amua mwenyewe binafsi kuwa yupo mbele ya Mjuzi wa ghaibu, na wanamfanya kuwa hakimu na mwamuzi kati yao, kwa hiyo katika hali kama hii hatofanikiwa mwenye shaka au wasiwasi moyoni mwake.

Ndio, inawezekana mtu akawa mpiganaji shupavu katika medani ya mapambano, kwa mantiki hiyo tunaona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) katika mapambano yake na makafiri alikuwa amuita kwenda kwenye jihadi kila mwenye uwezo wa kubeba silaha japo awe mnafiki. Lakini ilipobadilika aina ya mapambano kutoka yale ya vita na kuwa ya dua na kulaaniana na manaswara, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) hakumwita yoyote kwenye aina hii mpya ya mapambano miongoni mwa maswahaba wake, kwa sababu katika ngazi hii hawezi kuja mbele ya safu ila mwenye moyo uliosalimika, uliotoharika kwa kuwa mbali na uchafu na dhambi, nao ni chaguo lililochujwa. Na mfano wa watu kama hawa

[77] *Mustadrak Swahihayni* Juz. 3,Uk.158. Na amesema: Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za Muslim, japo hajaiandika.

hawawi wengi miongoni mwa watu, wao aghlabu huwa wachache, isipokuwa tu wao ni watu bora miongoni mwa walio ardhini.

Basi ni nani hawa chaguo lililochujwa?

Pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alipofanya mjadala na wanavyuoni wa kinaswara kwa ambalo ni jema, hakupata kutoka kwao ila ukafiri, upinzani na kuasi, na hapakuwa na njia nyingine ila ni kumsihi Mwenyezi Mungu, nako ni kila mmoja kati yao aombe kwa alilokuwa nalo na waijaaliye laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo. Muda huo amri ya Mwenyezi Mungu ilikuja:

﴿ فَمَنْ حَآجَّكَ فِيهِ مِنۢ بَعْدِ مَا جَآءَكَ مِنَ ٱلْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا۟ نَدْعُ
أَبْنَآءَنَا وَأَبْنَآءَكُمْ وَنِسَآءَنَا وَنِسَآءَكُمْ وَأَنفُسَنَا وَأَنفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل
لَّعْنَتَ ٱللَّهِ عَلَى ٱلْكَـٰذِبِينَ ﴿٦١﴾ ﴾

“Na mwenye kukuhoji katika hilo baada ya kukujia elimu sema: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, wanawake wetu na wanawake wenu, na nafsi zetu na nafsi zenu, halafu tumsihi Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na tuijaalie laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo.” (*Surat Aali Imran*: 61).

Hapo makasisi waliitikia pendekezo jipya la Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ili vita viwe vya kuamua hatima kati yao, hivyo basi makasisi walikusanya watu wao walio mahsusi kuiandalia siku hii. Na siku ya ahadi ilipowadia na umma ulijikusanya, manaswara walitangulia wakiwa na imani kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) naye pia atakuja na kundi la maswahaba wake na wanawake wake, yaani wakeze. Ikajitokeza Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akija mbele kwa hatua thabiti akiwa na nyota chache katika Ahlul-Bayt, Hasan akiwa kuliani kwake na Husein kushotoni kwake, Ali na Fatima wakiwa nyuma yake. Pindi

manaswara walipoziona nyuso zinazochomoza kwa mwanga wa ucha-Mungu, wao walitetemeka kwa hofu, wote walimgeukia askofu mkubwa wao: “Ewe Abu Haritha waonaje suala hili?” Askofu aliwajibu: “Naziona sura lau kwazo mtu atamwomba Mwenyezi Mungu ili jabali ling’oke kutoka mahali pake angeliondoa.” Mshangao wao ulizidi, na Askofu alipohisi hivyo akasema: ‘’Je hamumwoni Muhammad mwenye kuinua mikono yake akiangalia (mikono) inavyomjibu. Kwa haki ya Masihi akitamka neno hatutarejea kwa ahali wala mali.”[78]

Hapo basi waliamua kurudi na kutoendelea na dua. Waliridhia udhalili na kulipa jizya[79]. Kupitia hao watano Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliwashinda hao manaswara na aliwarudisha hali wakiwa wamenyongea. Kwa minajili hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akasema: ‘’Naapa kwa Ambaye nafsi yangu ipo mkononi Mwake, kwa hakika adhabu ni yenye kuwakurubia watu wa Najran, lau si msamaha wake wangepatilizwa na kuwa tumbili na nguruwe na wangekolezewa moto katika bonde na Mwenyezi Mungu angeifutilia mbali Najran na watu wake hata ndege mtini, na mwaka haungetimia wangepatilizwa manaswara wote.”

Lakini kwa nini Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliwaleta hawa wanne tu na yeye mwenyewe, wakawa waliohudhuria ni watano, wala hakuwaleta maswahaba wake na wakeze?

Ili kujibu hilo kwa neno moja, ni kuwa: Ahlul-Bayt ni viumbe walio bora mno kwa Mwenyezi Mungu baada ya Mtume, na ni wasafi mno na wako tohara sana, na sifa hizi hawakustahiki nazo watu wengine wasio kuwa wao, sifa ambazo Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amezithibitisha kwa Ahlul-Bayt katika Aya ya tohara kama ilivyotangulia. Kwa minajili hiyo tunamkuta Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) katika kuitekeleza Aya

78 *Al-Durul-Manthur* cha Suyutiy, Juz. 2, ***Surat Al Imran***: 61.

79 Kodi inayolipwa na makafiri wanaoishi katika nchi za kiislamu.

hii ni jinsi gani anavyogeuza mtazamo wa umma ili uielekee daraja ya Ahlul-Bayt. Kwa hiyo anaitafsiri kauli ya Mwenyezi Mungu: ‘Watoto wetu’ kwa maana ya Hasan na Husein (a.s.). Na ‘Wanawake wetu’ kwa maana ya Sayyida Fatima Zahrau (a.s.). Na ‘Nafsi zetu’ kwa maana ya Ali (a.s.). hiyo ni kwa sababu Imam haingii pamwe na wanawake wala pamwe na watoto, kwa hiyo kunabaki kuingia kwake ni katika neno ‘Na nafsi zetu, na ibara ya ‘Nafsi zetu’ ingekuwa mbaya lau tu wito ungekuwa umeelekezwa kwenye dhati yake tu.

Basi ni vipi aiite nafsi yake?.. Hilo latiliwa nguvu na kauli ya Mtume (s.a.w.w) :

أ نا و علي من شجرة وا حدة وسائر الناس من شجر شتى

“Mimi na Ali ni kutoka mti mmoja na watu wengine waliobaki wanatoka miti mingi tofauti.’’

Hivyo ikiwa Imam Ali (a.s.) ni nafsi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kwa hiyo yeye ana haki ile aliyonayo Mtume (s.a.w.w) katika uongozi na kuwa walii juu ya waislamu, isipokuwa daraja moja, nayo ni daraja ya unabii kama alivyosema Mtume (s.a.w.w), alivyonakiliwa na *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim*: “Ewe Ali nafasi yako kwangu ni sawa na ya Haruna kwa Musa, isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.”**80**

Kwa kweli kuitolea kwetu dalili Aya hii si mahali hapa, ila tu ni katika kubainisha Ahlul-Bayt ni watu gani, na Alhamdulillahi hapajakuwa na tofauti kuwa Aya hii iliteremka kuwahusu watu wa Kishamia. Na kuna habari na Hadithi katika uwanja huu.

Muslim na Tirmidhiy wote wawili wameieleza riwaya hii katika mlango wa fadhila za Ali (a.s.), kutoka kwa Saad bin Abu Waqqas akisema: “Ilipoteremka Aya hii: **“Sema: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto**

80 Rejea *Bukhari* kitabu cha fadhila. *Sahih Muslim* kitabu cha fadhila za sahaba. Na *Musnad* Juz.3, riwaya namba 1463.

wenu, wanawake wetu na wanawake wenu” Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alimwita Ali, Fatima, Hasan na Husein, akasema: “Ewe Mwenyezi Mungu hawa ndio Ahlul-Bayt wangu.”**81**

Na Suyutiy, Al-Hakim na Al-Bayhaki wameitaja. Na kauli yake: “Hawa ndio Ahlul-Bayt wangu.” yajulisha kuwaainisha Ahlul-Bayt ni hawa wanne.

81 *Sahih Muslim*, Juz.4, Uk. 360. Chapa ya, Isa al’Halabiy, na Juz.15, chapa ya Misri Uk. 176. *Sharhun–Nawawiy*. *Sahih Tirmidhiy* Juz. 4 Uk. 293. Hadithi namba 3085 Juz.5 Uk. 301 Hadith namba 3808. *Al-Mustadrak Alas-Swahihayni* Juz.3, Uk. 150.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda

28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n’amavuko by’ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur’an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili

93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Nne
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
113. Shiya N'abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Vikao vya Furaha
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas-ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
141. Azadari
142. Wanawake katika Uislamu na mtazamo mpya

BACK COVER

UKWELI ULIOPOTEA

Kitabu hiki ni utafiti uliofanywa na mwanachuoni wa Sudan, Sheikh M'utasim Sayyid Ahmad. Mwanachuoni huyo alikuwa ni wa madhehebu ya Sunni, aliamua kufanya utafiti juu ya madhehebu hizi mbili, yaani Sunni na Shia na utafiti wake huu ukazaa kitabu hiki ambacho amekiita, *Ukweli ukiopotea.*

Pia katika jitihada yake hii, amejaribu kuelezea kwa urahisi kabisa njia za kupunguza (kama si kuondoa kabisa) misuguano iliyopo baina ya Waislamu na baina ya madhehebu.

Nia kubwa ya mwandishi huyu ni kutafuta na kuugundua ukweli. Hata hivyo kusema ukweli na kuutafuta wakati mwingine huchukuliwa kama jinai isiyosameheka. Lakini msema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu; na mafunzo ya Uislamu yamejaa msisitizo wa kusema kweli hata kama ni mchungu, na hata kama unamhusu mpenzi wako au juu yako wewe mwenyewe. Ukweli siku zote huelea juu - kamwe hauzami.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info